Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

# UKRISTO NA UISLAMU:
# Mambo Muhimu—Sehemu ya Kwanza

**Mwandishi**

**Jonathan M. Menn**

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974**
**J.D., CornellLawSchool, 1977**
**M.Div., Trinity Evangelical**
**Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders-East Africa**
**3701 N. Gillett St., Appleton, WI54914**
**(920) 731-5523**
**jonathanmenn@yahoo.com**
**www.eclea.net**

2015; kimepitiwa Machi 2016; marekebisho Juni-Novemba 2016, Julai 2018; kimepitiwa Aprili 2019; marekebisho Mei 2019

Haya ni mafafanuzi ya Uislamu kutokana na mtazamo wa Kikristo na malinganisho ya mafundisho ya Kikristo na Kiislamu. Sehemu ya kwanza inajumuisha misingi ya awali ya mamlaka ya Uislamu, Imani, makundi, na historia kujadili vikwazo vya msingi vya Waislamu kwa kile Yesu alichofanya na Yesu ni nani, yaani, kwamba alisulubiwa, alifufuka, na ni Mwana wa Kiungu wa Mungu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

## 1. MTAZAMO WA MSINGI WA UISLAMU

I. Utangulizi……………………………………………………………………………………….3
A. *Ukubwa na ukuaji*……………………………………………………………………………....3
B. *Asili na takwimu*………………………………………………………………………...............3
C. *Makundi ya Uislamu*……………………………………………………………………….....3

II. Mambo ya msingi ya Uislamu ……………………………………………………………………...4
A. *Vyanzo vya mamlaka*……………………………………………………………………….....4
B. *"Nguzo tano" za Uislamu*…………………………………………………………………….....6
C. *Makala sita za imani ya Kiislamu* ………………………………………………………….....7
D. *Kalenda, sikukuu, siku takatifu na maeneo matakatifu*……………………………………….....8

III. Mohamedi na Historia ya Uislamu……………………………………………………………10
A. *Mohamedi*……………………………………………………………………………………...10
B. *Historia ya Uislamu*…………………………………………………………………………....10

## 2. YESU NA MOHAMEDI

I. Utangulizi…………………………………………………………………………………....11

II. Mtazamo wa Uislamu juu ya Yesu…………………………………………………………….11
A. *Yesu au Isa*……………………………………………………………………………………….11
B. *Ukoo na kuzaliwa kwa Yesu*…………………………………………………………………….12
C. *Kulingana na Uislamu, Yesu hakusulubiwa wala kufufuka*…………………………………...13
D. *Kulingana na Uislamu,Yesu ni nabii lakini siyo mwana wa Mungu*……………………………..16

III. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Utangulizi…………………………...............18

IV. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Kusulubiwa……………………………………19
A. *Mashahidi wengi*…………………………………………………………………………………...19
B. *Mwanzo wa imani ya Kikristo*………………………………………………………………….20
C. *Ushahidi wa kitabibu wa kifo*…………………………………………………………………...21
D. *Yesu kuzikwa Kaburini*…………………………………………………………………………21
E. *Mwitikio wa wanafunzi*………………………………………………………………………….22
F. *Uvumi ya kwamba alijidhuru mwenyewe*……………………………………………….......22
G. *Kuthibitishwa na maadui na vyanzo vingine visivyo vya Kikristo*………………………….....22
H. *Kushindwa kwa maelezo mengine*……………………………………………………….......23
I. *Hitimisho*…………………………………………………………………………………….....24

V. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Kufufuka ……………………………………....24
A. *Kaburi lilikuwa tupu* ……………………………………………………………………………....25
B. *Wakristo wa kwanza walianza kutangaza kufufuka kwa Yesu hata Yerusalemu*……………….26
C. *Mashahidi wengi*……………………………………………………………………………...26
D. *Maisha ya Wakristo wa kwanza yalibadilishwa kwa kile walichokiona*……………………….27
E. *Kuongoka ghafla kwa Paulo, adui wa Kristo*………………………………………………….28
F. *Kuongoka ghafla kwa Yakobo, aliyekuwa na mashaka juu ya Kristo*…………………………28
G. *Muundo na uwepo wa kanisa la Kikristo*…………………………………………………….29
H. *Kushindwa kwa maelezo mengine*………………………………………………………….......30
I. *Hitimisho*…………………………………………………………………………………….....33

VI. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Yesu ni "Mwana wa Mungu"………………...34
A. *Yesu alikuwa Mungu kamili: mwasisi na mtenda miujiza*…………………………………...36
B. *Yesu alijilinganisha na Mungu na kujitambulisha mwenyewe kuwa ni Mungu*……………...36
C. *Yesu alidai kuwa na uhusiano wa kipekee na Mungu Baba, Alimwita "Baba Yangu"*……….....38
D. *Matumizi ya Yesu ya neno "Mwana wa Adamu"ni kumbukumbu kwa Uungu wake* ……….........39
E. *Yesu alitumia neno "Mwana wa Adamu"sambamba na neno "Mwana wa Mungu" kuonyesha kwamba maneno yote mawili yana maana sawa*…………………………………………………………...40
F. *Yesu alijiita mwenyewe "Mwana wa Mungu" na alikubali aitwe "Mwana wa Mungu"na wengine*……..……41
G. *Maadui wa Yesu walitambua kwamba alidai kuwa yeye ni Mungu na walitafuta kumwua kwa kukufuru kwa sababu ya madai yake kwamba ni Mwana pekee wa Mungu* ………………………………….....41
H. *Watu humwabudu au kuomba kwa Yesu kama Mungu, na Yesu hukubali ibada hiyo* ……………................42

**I.** ***Yesu hasa aliitwa "Mungu" au "Bwana" kwenye matukio mengi ya Agano Jipya*** **……………………………...42**
**J.** ***Majina yale yale, vyeo, na sifa nyingine ambazo zilitumiwa na Mungu kwenye Agano la Kale au Agano Jipya zinatumiwa na Yesu kwenye Agano Jipya*** **…………………………………………………43**
**K.** ***Nabii na maandiko ambayo yanahusika kumtaja Mungu au Bwana kwenye Agano la Kale yamenukuliwa na kumtaja Yesu kwenye Agano Jipya*** **………………………………………………………………...44**
**L.** ***Hitimisho*** **…………………………………………………………………………………………………....44**

**VII.** **<u>Matokeo ya ukweli kwamba Yesu Kristo ni Mungu kamili na mwanadamu kamili</u>** **……..……………………45**
**A.** ***Mungu aweza kuwa kweli na kujulikana kibinafsi ndani ya Kristo*** **..………………………………..............45**
**B.** ***Kristo anatuonyesha sisi asili ya kweli ya Mungu ilivyo na hivyo pia ni mfano wetu wa kweli wa jinsi ya kuishi…*** **……………………………………………………………………………………………….....46**
**C.** ***Ukombozi kutoka kwenye dhambi zetu unawezekana tu kwa sababu Kristo ni Mungu kamili na mwanadamu kamili*** **…………………………………………………………………………………...46**

**ORODHA YA VYANZO……….………………………………………………………………….…………......47**

**MWANDISHI………..…………………………………………………………………………………….…..….47**

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

# 1. MTAZAMO WA MSINGI WA UISLAMU

## I. Utangulizi

*Uislamu* maana yake ni "kuwa mtiifu kwa Allah" (Darussalam 2002b: 332; Dirks 2008: 178; Emerick 2004: 402). *Muislamu* maana yake ni "mtu anayemtii Mungu" (Braswell 2000: 3; Emerick 2004: 405). Uislamu umeigawanya dunia kwenye maeneo makuu mawili: (1) *Dar al-Islam* ("nyumba ya Uislamu"), Ulimwengu wa amani, pale Uislamu unapofundishwa na Korani kuelezewa; na (2) *Dar al-Harb* ("nyumba ya vita"), ulimwengu wa mapambano na ujinga, ambao unamilikiwa na wasio Uislamu. "Utume wa Uislamu ni kuuleta ulimwengu huu wa pili chini ya Uislamu" (Braswell 2000: 3).

### A. *Ukubwa na ukuaji*

1. Ukristo na Uislamu ni dini kubwa mbili duniani. Sensa ya mwaka 2015, iliyoyahesabu madhehebu yote, vikundi, na makundi ndani ya kila dini, Idadi ya Ukristo ilifikia waumini wapatao bilioni 2.4 (takribani asilimia 33% ya watu wote Ulimwenguni) Idadi ya Uislamu ilifikia waumini wapatao bilioni 1.8 (takribani asilimia 24.1% ya watu wote Ulimwenguni) ("Orodha ya idadi ya waumini kwenye madhehebu" 2019: makisio ya waamini ya mwaka 2012; "Islam" 2019: Takwimu).
2. Uislamu ndiyo dini kubwa inayokuwa kwa kasi Zaidi Ulimwenguni (Emerick 2004: 3; "Ukuaji wa dini" 2019). Kwa karne iliyopita Uislamu ulikua kwa takribani asilimia 50% kwa haraka zaidi kuliko ukuaji wa Ukristo ("Ukuaji wa dini" 2019: Ukuaji wa kihistoria [jedwali]); kwa Zaidi ya miaka 40 iliyopita, Uislamu ulikua kwa kasi karibia mara mbili ya Ukristo ("Makundi makuu ya dini" 2019: Ukuaji wa waumini [jedwali]). Kwa hiyo, na kutoa nafasi ya kuongezeka kwa kasi ya idadi ya watu ulimwenguni kwa karne iliyopita, Uislamu wameongeza idadi yao kwa mara mbili kwenye idadi ya watu duniani wakati idadi ya Ukristo ikibaki ile ile kwenye ongezeko la watu duniani ("Ukuaji wa dini" 2019: Ukuaji kihistoria [jedwali]).[1]

### B. *Asili na takwimu*

1. Msingi na kuenea. Uislamu uliamzishwa na Mohamedi (AD 570-632), mzaliwa wa Maka Saudi Arabia ya sasa. Mohamedi na wafuasi wake waliishinda Arabia wakati wa uhai wake. Baada ya kifo cha Mohamedi, Gregory Davis anaeleza, "Uislamu ulienea kwa kasi kwenye himaya ya Byzantium, Persia, na Ulaya magharibi miaka mingi baada ya Mohamedi kufa. Baada ya kudhoofisha nguvu za Byzantine na Persian, walipambana wenyewe kwa wenyewe na kudhoofishana, kilichowapelekea kushindwa kukabiliana na mashambulizi ya maadui zao. Jeshi la Uislamu Waarabu liliingia Nchi takatifu, na kuzishinda nchi ambazo kwa sasa ni Iraki na Iran, walielekea magharibi na kuingia Afrika ya Kaskazini, Uhispania, na hatimaye kuingia Ufaransa. Mashambulizi ya Uislamu hatimaye yalisimamishwa na mapambano kati yao na wasafiri, siyo mbali sana kutoka Paris, mwaka 732 AD. Kwa upande wa mashariki, wenye itikadi kali walijiingiza Asia ya kati." (Davis 2014: sec.2.4.i)
2. Takwimu. Kwa sasa, wastani wa nchi 57 zina Waislamu wengi ("Islam" 2019: Takwimu). Kwa Ulimwenguni Waislamu wengi Zaidi wanaishi bara la Asia na Afrika, ambapo asilimia 62% wanaishi Asia (Ibid.). Nchi kumi zenye idadi kubwa ya Uislamu, wanaofikia Zaidi ya billion moja wameorodheshwa kwa wingi wao: Indonesia, Pakistan, India, Bangladesh, Nigeria, Misri, Iran, Uturuki, Algeria, Morocco ("Nchi kumi za juu" 2018: jedwali). Afrika ndilo bara pekee lenye Waislamu wengi (Ibid.). Warabu wanafanya asilimia 20% ya idadi ya Uislamu duniani ("Islam" 2019: Takwimu).

### C. *Makundi ya Uislamu*

Waislamu kimsingi wanajitambulisha kama jamii iliyoungana (*Ummah*) tofauti na madhehebu mengi ya makanisa ya Kikristo. Hii inatokana na ukweli kwamba, kama Muislamu wa awali Thabiti Anyabwile alivyoliweka, Uislamu ni "Utambulisho wa msingi"; hivyo, "jambo muhimu la *kwanza* ni kuwa Muislamu;

---

[1] Woodberry na Shubin wanatupa picha nyingine ya kupongezwa: "ukuaji wa Uislamu kwa kiwango cha asilimia 2.15 kwa mwaka unazidi kiwango cha ukuaji wa Ukristo ambao ni kiwango cha aslilimia 1.45. Anastahili kuonyesha hivyo, hata hivyo,hiyo asilimia 96 ya ukuaji wa Uislamu unachangiwa na watoto wanaozaliwa kwenye familia za Kiislamu. Uislamu umestawi sana Ulimwenguni hasa sehemu zile ambazo ongezeko la watu ni kubwa. Kuongezeka kwa Ukristo kumetawanyika, Una desturi ya kuwa kwenye sehemu za Ulimwengu ambazo ongezeko la watu ni dogo sana na pengine limefikia kusimama kabisa. Hivyo, kwa mtazamo wa jumla kuonyesha kuwa Uislamu unakua kwa kasi kuliko Ukristo.

Ongezeko la waumini ni pale ambapo tofauti kubwa inaonekana. Kulingana na toleo lililowasilishwa mwaka 2000 la itifaki ya Kikristo duniani, kila mwaka watu wapatao 950,000 hujiunga na Uislamu kutoka dini nyingine. Ukristo, kwa kulazimisha, angalia watu wapatao milioni 2.7 kila mwaka wanaungana na Ukristo na kufanya kila wawezalo kuyaunganisha maisha yao na Kristo toka kwenye dini nyingine." (Woodberry na Shubin 2001:"Dini zinazokua kwa kasi")

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

jambo la pili utaifa au kundi la desturi" (Anaybwile 2011: 89). Hata hivyo, "Pamoja na Waislamu kutumia Korani moja na Hadithi, Ulimwengu wa Waislamu ni mgumu/haueleweki. . . . Ukweli umetofautiana kati ya Waislamu wale wa kawaida na wale wenye itikadi kali, Uislamu wa desturi na wale wenye misimamo mikali wa Kikorani." (Garrison 2014: 232)

Kwa nyongeza, Mohamedi alisema, "Wayahudi waligawanyika kwenye makundi sabini na moja, au makundi sabini na mawili, na Wakristo kadhalika, na Ummah wangu utagawanyika makundi sabini na matatu" (at-Tirmidhi: 2640). Kati ya hayo "makundi sabini na matatu," Mohamedi aliongeza, "Makundi sabini na mawili kati yake wataenda kuzimu na moja litaenda Paradiso, na ni makundi yaliyo mengi" (Abi Dawud: 4597). *Kamusi ya Kiislamu* inaeleza kwamba idadi ya makundi hayo ya Uislamu kwa sasa "yameshazidi kile alichotabiri nabii, kwa sababu makundi ya Uislamu sasa ni mengi hata kuliko yale ya dini ya Kikristo" (Hughes 1895: 567). Yaliyo makuu ni pamoja na (angalia Braswell 2000: 59-70; Emerick 2004: 359-72; Nehls na Eric 2009: 66-80; Schirrmacher 2011: 51-59):

1. <u>WaSunnis ("Wenye njia," mfano, wale wanaofuata Sunnah).</u> WaSunni wanaunda asilimia 80% ya Waislamu wote. Mafundisho makubwa yahusuyo Uislamu "uliokubalika" ni WaSunni.
2. <u>WaShi'ah ("wafuasi").</u> Washia wanaunda asilimia 10% ya Waislamu (Iran na Iraki wengi wao ni WaShia). Washia wanaamini kuwa Khalifa (Viongozi wa Kiislamu waliomfuatia Mohamedi) ni lazima awe ana nasaba na ni lazima asiwe anatokana na Abu Bakr lakini awe anatokana na Ali, Shemeji wa mwana wa Mohamedi, na mwana wa Ali. Mauaji ya mmoja wa wana wa Ali yalipelekea mgawanyiko wa moja kwa moja kati ya Wasunni na Washia. Kundi moja la ndani ya Washia ni Waismailia ambao wapo Afrika ya mashariki ambao kiongozi wao wa kiroho ni Agha Khan.
3. <u>Wahhabi.</u> Hili ni kundi linalokubalika, Vuguvugu halisi la Uislamu wa Sunni. Lilianza miaka ya 1700 huko Saudi Arabia. Mwasisi wake alitaka kuurudisha Uislamu kwenye asili yake. Kundi hili lina ushawishi mkubwa huko Saudi Arabia na liliwashawishi Uislamu wa asili duniani kote.
4. <u>WaSufi.</u> WaSufi ni Waislamu wachawi. Waimeunda kundi lao kumzunguka Shaikh, ambaye ni kiongozi wao wa kiroho. Wameyakataa mambo ya dunia na kujitafutia kujifurahisha nafsi zao wenyewe kwa Mungu. Wao hutumia nyimbo, kucheza na kudansi wakati wote, na muziki ili kujaribu kupata mawasiliano ya moja kwa moja na Allah.
5.<u>Wa Ahmadiyya.</u> Kundi hili lilianzishwa India mwishoni mwa miaka ya 1800. Mwasisi wake alidai kuwa yeye ni Mahdi au Masihi. Ingawa Uislamu wote uanakataa kusulubiwa kwa Yesu, Wahmadiyya wanadai kuwa Yesu alikuwepo msalabani lakini alishushwa na kupatiwa huduma za kiafya. Wahmadiyya pia wanaamini kwenye ndoa ya mke mmoja. Wamejielekeza sana kwenye Umisioni na hawakubaliwi sana na Ulimwengu wa Waislamu wenzao.
6. <u>Uislamu wa desturi.</u> Uislamu wa desturi siyo kundi lililojitenga lakini ni idadi kubwa ya wale waliojiunga na dini ya asili pamoja na Uislamu. Hawa ni wale ambao, ingawa "nguzo tano"za Uislamu wanazitimiza (angalia hapo chini), wanaamini kwenye Ulimwengu wa roho (wachafu/wema), huwatii mababu, kusoma viganja, tasbihi, na talasimu, wanategemea uganga na uchawi ni mambo muhimu na ya kiutendaji kwa maisha ya kila siku ya dini.Mwandishi mmoja aliandika, "Ambapo Uislamu wa kawaida wanasisitiza kwa kina, taratibu za sheria na desturi, Uislamu wa desturi unatawaliwa na roho, mapepo, baraka, laana, uchawi na uponyaji" (Love 1994: 87; angalia pia Brown 2006a: 6-7). Watafiti mbalimbali wanakisia kuwa kati ya 70-85% ya Waislamu wote Duniani wameshawishika na Uislamu wa desturi (Brown 2006a: 6-7).

## II. <u>Mambo ya msingi ya Uislamu</u>

Kwa Muislamu aliyeamini, "dini siyo jambo la kufundishwa au kushawishiwa na elimu ya Ki Mungu. Siyo desturi ya nadharia. Ni *utambulisho* kutoka kwa familia yake, jamii, tamaduni, na nchi." (Houssney 2010: 82, fafanuzi imeongezwa; angalia pia ibid. at 103-11; Brown 2008: 19 ["Kwa Waislamu wengi, kuwa Muislamu ni jambo lisilowezekana kutenganishwa na utambulisho wao binafsi, makuzi yao, jamaa zao, jamii yao, na urithi wao wa asili, bila kujali wanaamini nini kumhusu Mungu"]. Malengo ya Uislamu ya kuendeleza Dar *al-Islam* ("Nyumba ya Uislamu") "hayafanyiki ili kufundisha nguzo tano za Uislamu lakini ili kuendeleza *sheria*, sheria za Uislamu" (Anyabwile 2011: 90).

### A. *Vyanzo vya mamlaka*

1. <u>Korani.</u> Korani ni kitabu kitakatifu cha Uislamu. Kikimaanisha "simulizi" au "kinachoeleweka." Kinaaminika kuwa ni neno kamili la Allah, likidumu milele huko mbinguni (**Q. 85:21-22**).[2] Inaaminika

[2] Kawaida, kwenye vitabu vyangu vya mafundisho ya ECLEA, Nimeweka nukuu za kwenye Biblia kwa **wino uliokolea** na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kuwa ilisimuliwa, kipinde kwa kipande, na malaika Gabrieli kwa Mohamedi kwa Zaidi ya miaka 23 (**Q. 17:106; 25:32**). Korani imegawanywa kwenye *sura* 114 . Mwanazuoni wa Kiislamu Mohamedi bin Abdullaah As-Suhaym anasema kuwa "korani ni mgawanyo wa maeneo matukufu ambayo yamebeba Ayas [*ayah*; kwa wingi = *ayat*] ambazo zaweza kuwa au kutokuwa na maana inayofanana. Baadhi ya watafsiri hutafsiri kama milango kitu ambacho siyo sahihi hata kidogo kwa sababu Mlango ni mkusanyiko wa vifungu ambavyo huzungumzia suala liletalo mwendelezo wa maana ile ile." (As-Suhaym 2006: 132n.1) Sura *hazijaandaliwa* kufuata kalenda wala somo husika" (Haleem 2005: xix; angalia Nyongeza A kwa mfuatano wa *kikalenda* wa sura). Zipo tofauti za wazi kwenye "asili" na somo husika baina ya sur za awali wakati ambao Mohamedi alikuwa dhaifu akiwa Maka na sura za baadaye Mohamedi alipokuwa kwenye mamlaka na utawala kule Medina (Haleem 2005: xvii-xviii; Michael na McAlister 2010: 17; Sell 1923: 187-95; Gilchrist 1995: ch.1.4). Tofauti hizo ni pamoja na mtazamo wa Korani (Mohamedi) juu ya Ukristo (al-Fadi 2003: 2).

2. <u>*Sunnah* ya Kinabii (maisha, maneno, na mifano ya Mohamedi).</u> Mifano ya maisha ya Mohamedi huitwa *Sunna yake* (mfano, mapito, njia, desturi za maisha). Suhaym anasema, "*Sunnah* ni chanzo cha pili cha dini ya Uislamu. Hii ina maana kwamba yote aliyoyanena Nabii –yaliunganishwa kwenye chanzo cha kweli na kuenezwa – kwa yale aliyoyasema, aliyoyatenda, na kuthibitishwa kwenye ubora. . . . *Sunnah* ni utekelezaji kwa vitendo wa taratibu/miongozo, imani, matendo ya ibada, aina za mahusiano na tabia ambazo Uislamu umeamriwa. . . . Kwakuwa *Sunnah,* inatazamwa kama utekelezaji kwa vitendo kwa Uislamu, inaielezea Korani pia kuitolea mafafanuzi, na kuelezea aya zile ambazo zina maana ya pamoja. . . . *Sunnah* inaweza, kwa maeneo mengine, kutoa maelezo huru ya baadhi ya miongozo na sheria ambazo hazipo kwenye Korani. Mtu ni lazima aamini Korani na *Sunnah* kwamba ndizo misingi ya dini ya kiislamu na kwama ni lazima zifuatwe na kuangaliwa. Kutii maamrisho yake, makatazo yake ni lazima yasiepukwe na kile kilichomo ndani kiaminiwe." (As-Suhaym 2006: 163-65; angalia pia Emerick 2004: 23)

Wakati wote Korani imewaagiza Waislamu*"kumtii Allah na Mjumbe wake"* (**Q. 3:32, 132; 4:13, 59, 69, 80; 5:92; 8:1, 20, 46; 9:71; 24:51, 52, 54, 56; 33:33; 47:33; 58:13; 64:12**). Kwenye hotuba yake fupi ya kuagana aliyoihubiri muda mfupi kabla ya kifo chake, Mohamedi alisema, "Nimewaachia nyuma yangu vitu viwili, Korani na mfano wangu, Sunah na kama mkivifuata hamtapotea kamwe" (Mohamedi 2014: n.p.). Suhaym alisema, "Mtu ni lazima aiamini Korani na *Sunnah* kwamba ndiyo misingi ya dini ya Uislamu ambayo yapaswa kufuatwa na kuangaliwa. Maamrisho yake ni lazima kuyatii, makatazo yake ni lazima yaepukwe na yaliyoandikwa yaaminiwe." (As-Suhaym 2006: 165) Emerick maelezo ya kufanana, "Kwa kusema kwamba Mohamedi ni Mjumbe wa mwisho wa Mungu, tunajiapisha wenyewe kutenda yale aliyoyahubiri, kufanya yale aliyoyafanya, na kumwangalia kama kielelezo chetu" (Emerick 2004: 130).

Chochote alichokisema Mohamedi, alichokifanya, au kukikubali kimya kimya kinaitwa *hadith* (kwa wingi = *ahadith*) (Emerick 2004: 241-44).Sunnah imeunda msingi wa Hadithi. Kwakuwa Sunnah na ahadith ni maalum na za kiutendaji, kwa njia nyingine zaweza kuwa za kimamlaka kuliko Korani ingawa kimsingi Korani ina mamlaka zaidi. Kama Muislamu mmoja alivyosema, "Kama *Korani* ni kitabu cha masomo ya msingi kwa mitihani ya maisha ya Waislamu, *Ahadith* . . . inawakilisha vitendo, vitabu vya kiada, vinavyoweza kukusaidia kuainisha kati ya kufaulu na kufeli mitihani yote muhimu" (Dirks 2008: 46).

Kila hadithi imeundwa kwenye sehemu mbili: "kwenye mtiririko wa usambazaji" au chanzo (*isnad*) na utoshelevu (*matn*). Mwanazuoni wa Kiislamu amezipanga shuhuda za Mohamedi kwenye madaraja ya kuaminiwa na kuchagua makundi sita ya ahadith za Mohamedi kama ya kutegemewa au kukubaliwa (zile za al-Bukhari, Muislamu, wa-Tirmidhi, Abi Dawud, an-Nasa'i, na Ibn Majah).[3] Kila

---

nukuu ndefu kwa *kiitaliki*. Nitatumia mfumo huohuo kuziheshimu nukuu kutoka kwenye Korani. Vinginevyo itaelezwa, nukuu toka kwenye Korani zitakuwa kutoka kwenye tafsiri ya Kiingereza ya Yusuf Ali, *Maana ya Korani inayoheshimiwa.* Matoleo mengine yatakayotumika ni pamoja na (i.e., Sahih International [inasema kama Sahih], Pickthall, Shakir, Sarwar, al-Hilali na Khan [inasema kama Hilali-Khan], na Arberry) yote yanapatikana kwenye wavuti ya Kiislamu iitwayo *Quranic Arabic Corpus* (http://corpus.quran.com/); iliyotafsiriwa na Mohamedi Asad na M. A. S. Abdel Haleem nukuu zao zitatumika. Vinginevyo maelezo yatatolewa, nukuu za Biblia zitatolewa kwenye Biblia ya kiingereza iitwayo New American Standard Bible.

[3] Haya na makusanyo mengine ya ahadith yanapatikana kwenye wavuti ya http://sunnah.com/. Kwenye kitabu hiki ninatumia neno "hadith" kwa misemo binafsi ya Mohamedi, "ahadith" kwa misemo mingine kama, na "Hadith" kwa misemo yote na makusanyo ya misemo ya Mohamedi. Namba za utambulisho ni kama zilivyo kwenye wavuti ya

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kundi lilikusanywa mwishoni mwa karne ya tisa na mwanzoni mwa karne ya kumi (miaka, 250-300 baada ya kifo cha Mohamedi).

3. <u>*Sheria* (Sheria za Kiislamu).</u> *Sheria* hii ni kurugenzi (kikundi) ya wasomi wa Kiislamu inayotunga na kupanga sheria (inayoitwa*'Ulema*). Georges Houssney anasema, "Korani haifundishwi ili kueleweka na watu wote. Inafundishwa ili msimuliaji aweze kupata kibali mbele za Mungu. Ni Sheria, na siyo Korani, ndiyo inayoyaongoza maisha ya kila siku ya Muislamu." (Houssney 2010: 89) Kusudi la Sheria "ni kutoa mwongozo wa kila jambo ambalo litamkabili Muislamu au jamii ya Kiislamu" (Emerick 2004: 55). Imeandaliwa kuyaongoza maisha yote ya Muislamu. Sheria inasimamia kila kitu kwa Muislamu kama ni *halal* (kinakubalika) au *haram* (kimekatazwa) (Ibid.: 264). Sheria ina misingi yake kwenye Korani na Sunna. Kama Korani na Sunna haizungumzii jambo husika, Mawazo ya Mohamedi hufuatwa kwa haraka (yanajulikana kama *sahaba*) ; kama hayo yote hayazungumzii suala husika, Wanazuoni hutumia uelewa wao na mambo yanayofanana na hayo kutolea maamuzi. Maamuzi ya kisheria huitwa *fatwa.* Zipo shule tano za sheria na desturi zilizoanzishwa na wanazuoni watano wa Kiislamu kwenye nusu ya pili ya karne ya 8th na nusu ya karne ya 9th AD. Wanne kati yao walikuwa ni WaSunni; mmoja ni Mshia. Mwandishi wa Kiislamu 'Abdus-Salam al-Basuni anasema Nia ya ndani ya Muislamu ni kuiangalia Sheria: "Nafasi ya muumini wa Kiislamu ni 'Sina wazo au mtazamo wangu mwenyewe juu ya kile ambacho Allah na Mjumbe wake wamekiagiza (Baraka na Amani ziwe juu yake),Nimesikia na nina tii'" (al-Basuni 2007: 16).

**B. *"Nguzo tano" za Uislamu*** (angalia As-Suhaym 2006: 167-75; bin Jamil Zino 2002: 282; Emerick 2004: 123-74; Nehls na Eric 2009a: 154-62)[4]

"Misingi ya Uislamu yote imeelezwa kwa msisitizo. . . . Mwiito wa maombi ni uleule siku zote, desturi ya kutawadha ni ileile vivyo hivyo siku zote muda wote Muislamu anapoenda Msikitini, na kila . . . mfumo wa maombi ni uleule na kwa uhakika marudia yaleyale ya kwanza. Desturi ya safari ya kuhiji Maka na utaratibu wa Mfungo wa Ramadhani ni kama ulivyoelezwa na haubadiliki milele. Asili ya marudio ya matendo yaleyale kwa Uislamu yametokana moja kwa moja na kutokana na amri ya kwanza iitwayo, *Iqra!* ["soma au simulia," neno la kwanza la Korani **Q. 96:1**, inayodhaniwa kuwa Aya ya kwanza aliyopewa Mohamedi], na Muislamu wa kweli anachokifanya ni kukariri kile kilichofunuliwa bila kukifikiria na bila kuruhusiwa kuuliza swali." (Gilchrist 1994: 91) Muislamu wa awali Thabiti Anyabwile anaongeza, "Mifumo ni muhimu kwa Uislamu kama Elimu ya theolojia. Uislamu umejengwa kwenye kuangalia mambo ya nje" (Anyabwile 2011: 90) "nguzo tano" za Uislamu ni hizi hapa:

1. <u>Shahadah.</u> *Shahadah* ni ukiri wa Imani ya Kiislamu. Kwa mujibu ya maombi ambayo Waislamu anapaswa kusema, shahadah inarudiwa angalau mara 17 kwa siku. Inasema, "Hakuna mungu isipokuwa Allah, na Mohamedi ni mjumbe wa Allah."

2. <u>Salat.</u> Uislamu wanaainisha maombi binafsi na maombezi (*du'a*) kutoka salat. *Salat* "ni desturi ya kidini ambayo kila Muislamu anapaswa kuitekeleza mara tano kila siku. . . . Hii ni pamoja na mfululizo wa mwili kuinama na kusujudu na kulala kifudifudi mara kadhaa pamoja na maombi na kukariri vifungu kwa kifupi." (Emerick 2004: 136) Mhusika anapaswa kuangalia Maka. Muda na idadi ya kurudia maombi pia kumeelezwa (ikiwa ni pamoja na idadi ya kuinama na kuinuka) : mapema asubuhi (kurudia mara mbili); mchana (kurudia mara nne); Adhuhuri (kurudia mara nne); jioni(kurudia mara tatu);usiku (kurudia mara nne). Kwa nyongeza, yapo "mahitaji saba yapaswayo kutimizwa"kabla ya maombi na mwanzoni mwa maombi, na salat ni lazima isemwe kwa lugha ya "kwa Kiarabu" (Ibid.: 138, 144).

3. <u>Zakat.</u> *Zakat* hii ni sehemu maalum ya utajiri ambayo inapaswa kutolewa/kulipwa kwa ajili ya kuinufaisha jamii maskini za Kiislamu. Inamtaka Muislamu mwenye umiliki wa aina yoyote yenye thamani ya vipande vitatu vya dhahabu. Zaka ni asilimia 2.5% ya kiwango cha utajiri wa Muislamu kwa

---

sunnah.com. Kwa sampuli za Misemo ya Mohamedi, angalia **NYONGEZA B—SAMPULI YA KILE MOHAMEDI NA UISLAMU WANACHOTAKA NA KUWAKATAZA WAISLAMU KUTENDA NA KUAMINI**.

[4] Anyabwile anaandika kwamba nguzo tano "zimeibuka kama makubaliano kuhusu kazi na Imani za *kidini*. Map ema kwenye historia ya Uislamu baadhi ya Waelewa na Wasomi wa Kiislamu walibishana juu ya *jihad* kuwa nguzo ya tano ya Uislamu kwa sababu *jihad,* au kupigana kwa sababu ya Allah, inaendana na kuitetea imani" (Anyabwile 2011: 89n.7). Nguzo tano zinazozungumziwa hapa ni kwa mujibu wa Uislamu wa Sunni. Georges Houssney anasema, "Nguzo tano za WaShia ni tofauti sana, zimeundwa kutokana na dhana zilizo wazi badala ya matendo" (Houssney 2010: 51n.1). Kwakuwa Wasunni wanawanafanya asilimia 80% ya Uislamu wote, Kitabu hiki kimsingi kitashughulikia Uislamu wa Sunni.angalia pia Makala iitwayo "Uislamu wa kweli kwa mtazamo wa Wakristo"linapatikana kwenye wavuti hii http://www.true-islam.info, ambalo linalinganisha "nguzo tano" za Uislamu na maneno yanayofanana nayo yanayopatikana kwenye Biblia.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwaka.
4. Saum. *Saum* ni mfungo wakati wa mwezi wa Ramadhani, ambao ni mwezi wa tisa kwenye kalenda ya Uislamu. Kutoka maawio ya jua mpaka machweo WAislamu wanapaswa kuepuka chakula, kinywaji, na kujamiiana. Hata hivyo, wanaweza kuwa huru kushiriki mambo hayo yote baada ya machweo hadi alfajiri. Wagonjwa, wasafiri, wanawake wajawazito, wamama wanyonyeshao, na wanawake waliojifungua watoto wachanga hawafungwi na sheria hiyo ya saumu.
5. Hija. Kila mtu mzima, mwenye afya njema, Muislamu mwenye uwezo wa kufanya hivyo anapaswa kuandaa kutembelea maeneo ya mababu zako (*hija*) kwenda kwenye Nyumba ya Allah—Msikiti mtakatifu wa Maka—angalau mara moja kwa kipindi cha uhai wake. Hija inapaswa kuwa kati ya siku ya nane hadi siku ya kumi ya mwezi wa kumi na mbili kwa kalenda ya Kiislamu. Wanaume wote wanaosafiri wanapaswa kuvaa vazi maalum jeupe, na wasafiri wote (waume kwa wanawake) hawaruhusiwi kujamiiana, kunyoa wala kukata kucha zao, kutumia marashi au vipodozi, kuwinda au kuua kiumbe chochote, au kupigana, au kubishana na ndugu yeyote kwa kipindi chote cha hija.

**C. *Makala sita za imani ya Kiislamu*** (angalia al-Athari 2005: 68-127; As-Suhaym 2006: 177-99; bin Baz 2002: 247-65; Houssney 2010: 59-63)

1. Kumwamini Allah. Kumwamini Allah ni pamoja na kuamini kuwa: Yeye ndiye muumbaji, mmiliki, na mwangalizi wa kila jambo; Ndiye mungu wa kweli na kwamba kila mungu mwingine tofauti naye ni mwongo. Kuamini pia ni pamoja na kuliamini jina na sifa zake. Zaidi ya yote, kumwamini Allah kunamaanisha kuamini kwenye upekee wake, kwamba hana mwenza kwenye Ubwana wake; Yeye pekee ndiye mwenye haki ya kuabudiwa. Fundisho hili la upekee wa Allah (ambao ni upekee ambao hauna wazo la utatu) ni fundisho la Uislamu la *tauhid.*
2. Kuwaamini Malaika. Kulingana na Uislamu, malaika waliumbwa nje ya mwanga na hawawezi kuonekana (ingawa wakati mwingine Allah huonyesha baadhi yao kwa manabii na wajumbe wake). Wana utendaji tofauti: Gabrieli inaaminiwa ndiye aliyemletea Mohamedi Korani; malaika wengine ni walinzi wa kuzimu na Paradiso, na wengine wanayo majukumu mengine. Kila mwanadamu amepewa malaika wawili, mmoja wa kuandika matendo mema, mmoja kuandika matendo maovu. Malaika ni wakubwa kwa umbo na wana mbawa. Kwa nyongeza, Huunganishwa na kila mtu wakati wa kuzaliwa kwake ni *qarina*, watu wanaofanana na mapepo, ambao kusudi lao ni kuwataabisha na kuwapofusha watu watoke kwenye njia iliyo sahihi. pia, viumbe walioumbwa kutoka motoni wanaitwa *jini* (wengi wao ila siyo wote ni waovu). Kiumbe mwovu siku zote ni *Shaytan* (Shetani).
3. Kuamini vitabu vya Allah. Uislamu unatambua vitabu vikuu vinne vitakatifu: *Tawrat* (Torati) alizopewa Musa; *Zabur* (Zaburi) alizopewa Daudi; *Injil* (Injili) alizopewa Yesu; na Korani *Qur'an* (Simulizi) aliyopewa Mohamedi. Waislamu wanadai kwamba Korani haikuumbwa bali ni ya umilele. Kwa sababu Korani inapingana na Biblia kwenye mambo mengi, Waislamu wanadai kuwa vitabu vyote vilivyotangulia havipo tena na kwamba waalimu na makuhani waliopewa jukumu la kuvilinda walishindwa kufanya jukumu lao la kuvilinda, Hivyo vilibadilishwa na kuharibiwa; hivyo,wanasisitiza kwamba Allah ameapa kuilinda Korani ili isiharibiwe, ili ibaki bila uharibifu uwao wote. Kama kitabu cha mwisho kutolewa kati ya vitabu vilivyotolewa kwa kuthibitisha vitabu vilivyotangulia (kabla havijaharibiwa) kabla ya kufutwa.
4. Kuwaamini Wajumbe (manabii). Uislamu wanadai kwamba Allah aliwatuma manabii na Wajumbe (Wanaosadikiwa kuwa wakuu Zaidi ya manabii) kwa mataifa yote kuwaonya watu kwa habari ya Sanamu, kutokumtii Allah, na *shirk* (dhambi ya asili ya kuwashirikisha watu kuwa Allah ana mwenzi), kuwaita watu wamsujudie Allah na dini ya kweli ya Uislamu. Baadhi ya Wanazuoni wa Kiislamu wanasema kuwa wajumbe 124,000 walitumwa. Korani inawataja wajumbe 25. Walio wakuu ni hawa wafuatao Adam, Nuhu, Ibrahim, Musa, Yesu, na Mohamedi. Wakati manabii wengine na wajumbe wakitumwa kwa taifa mojamoja, Mohameddi anasadikiwa kuwa mjumbe mkuu kati ya wote. Ndiye wa mwisho, alitumwa kwa majini na kwa wanadamu wote ni "*muhuri wa manabii*" (**Q. 33:40**).
5. Kuiamini siku ya mwisho (i.e., siku ya hukumu). Uislamu wanadai kuwa itakuwepo siku ya mwisho ya ufufuo na hukumu. Uislamu unafundisha kuwa matendo ya watu yatapimwa kwenye mizani. Daraja (*sirat*) la kutupeleka lenye wembamba kama wa wembe litawekwa juu ya shimo la kuzimu. Kila mmoja atapaswa kuvuka kupitia kwenye daraja hilo. Wale ambao hawataelekea Paradiso wataangukia kuzimu. Zipo ngazi saba za kuzimu na Paradiso. Kama watu waliopo kuzimu mungu mmoja Allah (*tauhid*) wataondolewa kuzimu baada ya muda uliowekwa. Wale watakaotenda dhambi ya asili ya kuwashirikisha watu kuwa Allah ana mwenzi watatupwa kuzimu milele.
6. Kuamini kwenye Utayarisho (Amri ya awali; hatima ya Ki Mungu). Uislamu wanafundisha kwamba

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kila kitu kinachotokea hapa Duniani, ikiwa chema au kibaya, Imani au kutokuamini, hutokea kwa mapenzi na amri ya Allah, na Allah hufaya chochote apendacho. Kila aamurucho hutokana na ufahamu wake, nguvu, na mapenzi yake, havitabadilika. Anajua kila kilichotokea, kinachotokea, na kitakachotokea kwenye umilele wote, na aliandika amri kuhusu uumbaji kwenye kitabu ambacho hakuna kitakachodharauliwa. Allah humlinda yeye ampendaye kwa huruma zake, na humpotosha yeyote apendaye kwa busara yake. Mapenzi ya Allah na amri zake hazijadiliwi. *"Bwana wako humwuumba yeyote ampendaye na kumchagua, hawana uchaguzi wowote (kwa jambo lolote). Utukufu una Allah, na kuinuliwa juu ya vyote vilivyoambatana naye kama washirika (pamoja naye)."* (**Q. 28:68,** Hilali-Khan)

**D. *Kalenda, sikukuu, siku takatifu, na maeneo matakatifu***

1. Kalenda ya Kiislamu ("Kalenda ya Kiislamu" 2019). Uislamu unafuata kalenda ya mwezi yenye miezi kumi na miwili, siyo kalenda ya jua. Kwa hiyo, mwaka wa Kiislamu unakadiriwa kuwa na siku 354 badala ya siku 365. Kwa sababu hiyo, Mwezi unapunguza siku 11 kwenye kalenda ya mwezi wa jua, hurudia kwenye mzunguko wake kila baada ya miaka 33.

Mwaka wa kwanza wa kalenda ya Kiislamu umeandaliwa kutokana na mapambano ya Mohamedi kutoka Maka kwenda Madina tarehe 17 Julai 622 (huu unaitwa *hegira*). Mwaka 639, Umar, ambaye ni kiongozi pili, aliutangaza hegira kama mwanzo wa kalenda ya Uislamu (Ibid.: 5). Hivyo, 622 mwaka wa kwanza 1 AH (baada ya hegira) kulingana na hesabu za Uislamu. 1440 AH unakisiwa kuanza kati ya 11 Septemba 2018 hadi 30 Agosti 2019. Haya ni majina ya miezi ya Kiislamu:

| Mwezi | Idadi ya siku |
|---|---|
| Muharram | 30 |
| Safar | 29 |
| Rabi I | 30 |
| Rabi II | 29 |
| Jumada I | 30 |
| Jumada II | 29 |
| Rajab | 30 |
| Sha'ban | 29 |
| Ramadan | 30 |
| Shawwal | 29 |
| Dhu'l-Qa'dah | 30 |
| Dhu'l-Hijjah | 29 or 30* (*mwaka mrefu) |

2. Siku takatifu na sikukuu za Kiislamu. Korani inasema, "*Idadi ya miezi machoni pa Allah ni kumi na mbili (kwa mwaka)-hivyo aliziweka wakfu siku alipoziumba mbingu na nchi; miongoni mwake mine ni mitakatifu*" (**Q. 9:36**). Miezi hiyo mine mitakatifu ni Muharram, Rajab, Dhu'l-Qa'dah, na Dhu'l-Hijjah. Zifuatazo ni sikukuu za kawaida za Uislamu (Braswell 2000: 40-41; Emerick 2004: 262-63; Nehls na Eric 2009: 231-34):

- *Siku ya Mwaka mpya (mwanzo wa Muharram):* Siku ya kukumbuka hegira.
- *Ashura (siku ya kumi ya Muharram):* Siku ya mfungo wa hiyari kuikumbuka siku inayosemekana Mungu aliwaumba Adamu na Hawa. Hii ni siku muhimu kwa Uislamu wa Shia, ikiwa ndiyo siku ambayo mtoto wa Ali Hussain aliuawa.
- *Maulid un Nabi (siku ya kumi na mbili ya Rabi I):* Siku ya kuzaliwa Mohamedi. Kisiwani Lamu huko pwani ya Kenya hili ni tukio kubwa na muhimu sana, kunakuwa na mashindano ya kukariri Korani yanayodumu kwa muda wa juma nzima.
- *Ramadan:* Kipindi cha Ramadhani Uislamu hufunga kula, kunywa, na kujamiiana kati ya wakati wa maawio hata machweo ya jua. Inaaminika kwamba kufunga kwa kipindi cha Ramadhani ni bora mara thelethini Zaidi ya kufunga wakati mwingine wowote na kwamba wale wanaofunga kwa moyo safi na wakiwa na nia njema husamehewa dhambi zao.
- *Lailatu'l-Qadr ("Usiku wa nguvu [au Utukufu]," siku ya ishirini na saba ya mfungo wa Ramadhani):* Ni siku inayokumbukwa ambayo inasadikiwa kuwa Malaika Gabrieli alimletea

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Mohamedi Aya ya kwanza ya Korani. Korani inasema, *"Usiku wa nguvu ni bora kuliko miezi elfu moja. Hapo alipokuja malaika na roho kwa ruhusa ya Allah, kwa kila kazi: Amani! . . . Mpaka wakati wa mapambazuko!"* (**Q. 97:3-5**).[5] Baadhi ya Uislamu hukesha usiku kucha wakiomba.

- *Eidu'l-Fitr ("Sherehe ndogo"au "sherehe ya kumaliza mfungo,"mwanzoni mwa mwezi wa Shawwal):* Hii ni sikukuu iliyo kuusana kwa Uislamu, kusherehekea kumaliza mfungo wa Ramadhani. Ni wakati wa kusherehekea, kuwatembelea jamaa na marafiki, kubadilishana zawadi, na vitamu huandaliwa.
- *Eidu'l-Adha ("Sikukuu kubwa" au "Siku ya kutoa sadaka,"siku ya kumi ya Dhu'l-Hijjah):* Hii ni kusherehekea kuhitimisha Hija (Safari ya Maka, Hii ni moja ya "nguzo tano za Uislamu" [angalia hapo juu]). Husherehekewa Duniani kote, hata Uislamu ambao hawakushiriki Hija. Ni wakati wa sherehe ya kutembeleana, Kula, kubadilishana zawadi, na kununua nguo mpya. Pia ni siku ya kutoa sadaka kama ilivyo kwenye Korani **Q. 22:34-37; Q. 37:100-110**. "Eid-ul-Adha ni kukumbukwa tendo la sadaka isiyo na ubinafsi lililofanywa na nabii Ibrahimu la kumtoa mwanae pekee Ishmaeli kwa Mungu pekee, Allah. . . . Lakini kwa muujiza wa ajabu, wakati Ibrahimu akiwa kwenye kumtoa sadaka Ishmaeli, Allah aliyaokoa maisha ya kijana kwa kumpatia mwana kondoo.[6] Na hicho ndicho alichokifanya Ibrahimu nyakati zote akitoa sadaka. Kwa kulikumbuka tukio hili la kipekee la kumtolea Mungu sadaka (qurbani) la nabii Ibrahimu, watu hudhabihu mwana kondoo, mbuzi, Kondoo au mnyama yeyote siku ya Eid-ul-Adha." ("Historia ya Eid-ul-Adha" 1988-2012: n.p.)

3. <u>Maeneo matakatifu ya Uislamu (angalia Emerick 2004: 161-74, 298-99; "Maeneo matakatifu ya Uislamu wa Sunni" 2019; Nehls na Eric 2009a: 241-42; "Qibla" 2019).</u> Kulingana na Hadithi, Mohamedi alisema, "Usiandae safari yako isipokuwa kwa Misikiti mitatu, i.e. Al-Masjid-AI-Haram, Msikiti wa Aqsa (uliopo Yerusalemu) na Msikiti wangu" (al-Bukhari: 1197). Alisema pia, "Ombi moja kwenye Msikiti wangu ni bora kuliko maombi elfu kwenye Misikiti mingine yoyote isipokuwa tu misikiti ya Al-Masjid-AI-Haram" (Ibid: 1190).

- *Kab'ah ulioko Maka.* Eneo takatifu sana la Uislamu ni Maka, eneo alikotoka Mohamedi. Hata hivyo, Eneo takatifu sana huko Maka ni Kab'ah ("mchemraba"). Kab'ah limejengwa kwa tofali zenye ukubwa wa mita 14x18, na mita 12 kwenda juu. Ni eneo takatifu kwa sababu Waislamu wanaamini kuwa lilijengwa na Ibrahimu na Ishmaeli kama mahali pa kuabudia (**Q. 2:127**). Kab'ah imefunikwa na nguo nyeusi na kuzungukwa na mawe meusi yaliyojengwa kwa upande wa pembe ya mashariki, inaaminika malaika Gabrieli alimpa Ishmaeli. Ni kuelekea Kab'ah kwamba Waislamu wanatakiwa kuomba mara tano kwa siku. Kab'ah ya asili iliharibiwa mara kadhaa na kujengwa tena kama eneo la kuabudia sanamu. Mohamedi alijitwisha jukumu la kulijenga tena na kulitakasa kutokana na sanamu. Kab'ah imezungukwa na Msikiti wa Masjid al-Haram ("Msikiti mtakatifu").
- *Al-Masjid an-Nabawi ("Msikiti wa Nabii") uliopo Madina.* Hili ni eneo la pili takatifu kwa Uislamu. Mohamedi alijihushisha kulijenga. Kilicho cha muhimu sana kwenye eneo hili ni paa la kijani katikati ya Msikiti, mahali lilipo kaburi la Mohamedi.
- *Msikiti wa Al-Aqsa ("Msikiti ulio mbali sana") upo Yerusalem.* Msikiti huu unaaminiwa kuwa mahali ambapo Mohamedi alichukuliwa usiku mmoja na Malaika Gabrieli na kiumbe afananaye na farasi aliyeitwa *Buraq*. Kutoka hapo alipaa mbinguni kabla ya kurudishwa Maka (angalia **Q. 17:1, 60; 53:1-18**). Yerusalemu ulikuwa mwelekeo ambao Waislamu kwa asili walipaswa kuelekea wakati wa maombi mpaka hapo Mohamedi alipopokea "ufunuo" mpya na kubadilisha mwelekeo kuelekea Kab'ah uliopo Maka (**Q. 2:142-144**). Msikiti huu upo eneo la mlima wa Hekalu uliopo Yerusalemu na ni maarufu kwa paa lake kubwa la dhahabu.

---

[5] "Roho" kwa ujumla inaeleweka na Uislamu kwamba ni malaika Gabrieli, siyo Roho mtakatifu (angalia Ali 2006: Q. 97:4 n.6219; Haleem 2005: Q. 97:3n.a; Dirks 2008: 197). Haya ni maelezo ambayo hayakuwekwa wazi kwenye Korani.Kwa maelezo Zaidi ya haya angalia n.72, hapo chini.

[6] Hili ni tofauti na maelezo kwenye **Mwanzo 22:1-19** mahali ambapo Mungu alimwambia Ibrahimu kumtoa sadaka (na kasha kumwokoa) *Isaka,* siyo Ishmaeli. **Q. 37:100-110** haielezi hasa ni mwana yupi ambaye Ibrahimu aliambiwa amtoe sadaka. Mwanahistoria Muislamu Abu Ja'far Mohamedi ibn Jarir al-Tabari (839-923) anaonyesha, "Hekima ya awali ya nabii wa taifa letu haikubaliana kuhusiana na ni yupi mwana wa Ibrahimu kati ya wawili ambaye aliamriwa kumtoa sadaka. Baadhi wanasema alikuwa Isaka, wakati wengine wanasema alikuwa Ishmaeli. Mitazamo yote miwili yanawezeshwa na maelezo yaliyoliyotolewa na mamlaka ya Mjumbe wa Mungu." (al-Tabari 1987a: 82) Kisha alitumia kurasa 14 kuandika na kunukuu mamlaka ya awali ya Uislamu kwa masuala yote kwa pande zote mbili. *Tafsir al-Jalalayn* anaashiria mkanganyiko huu kwenye maoni yake kwenye **Q. 37:107**: "Kisha tulimtoa sadaka mmoja yule ambaye aliamriwa kumtoa akiitwa Ishmael au Isaka — mawazo mawili tofauti — Kwa sadaka iliyo kuu na kwa kondoo aliye mkuu toka Paradiso."

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

## III. Mohamedi na Historia ya Uislamu

**A. *Mohamedi*** (angalia Emerick 2004: 291-312; "Mohamedi" 2019; Nehls na Eric 2009a: 3-66)

Maisha ya Mohamedi yanaweza kugawanywa kwenye makundi matatu: (1) Ujana wake na maisha ya ndoa hadi kwenye "wito wake" kuwa nabii wa Allah (AD 570-609); (2) Unabii wake wakati akiwa Maka (AD 610-622); na (3) Maisha yake akiwa Madina hadi kifo chake (AD 622-632).

1. Maisha yake kabla ya wito (AD 570-609). Mohamedi alizaliwa AD 570 huko Maka wazazi wake wakiwa ni Abdullah na Amina, wa ukoo wa Hashim wa kabila la Quraish. Baba yake alikufa kabla hajazaliwa, na Mama yake alikufa wakati akiwa na miaka sita. Mwanzoni alikulia kwa Babu yake, Abdu'l Muttalib, na baadaye mjomba wake, Abu Talib. Mohamedi alitokea kwenye familia ya wafanya biashara na kama kijana alisafiri sana akiwa na magari ya biashara. Alipokuwa na umri wa miaka 25 alimuoa Khadijah aliyekuwa mwajiri wake na alikuwa na miaka 15 zaidi ya Mohamedi. Kwa kila wakati ilikuwa ndoa yenye furaha, walijaliwa watoto wawili wa kiume na wane wa kike. Khadijah alifariki baada ya miaka 25 ya ndoa yao.

2. "Wito wake" na unabii wakati akiwa Maka (AD 610-622). Mohamedi alikuwa na tabia ya kujificha mapangoni mara kwa mara. Alipokuwa na umri wa miaka 40 alidai kuwa alitembelewa na Malaika Gabrieli akiwa pangoni, aliyeanza kumsimulia Korani (angalia maelezo ya Mohamedi kwenye al-Bukhari: 6982). Miaka mitatu baada ya tukio hilo Mohamedi alianza kuhubiri ufunuo huo kwa watu wote, akitangaza kuwa "Mungu ni mmoja" (i.e., *"tauhid"*), kwamba "amejitoa kwake kabisa" (i.e., *"uislamu"*) kwake ndiyo njia pekee inayokubaliwa na Mungu, na kwamba yeye mwenyewe ndiye Nabii na Mjumbe wa Mungu. Madai ya Mohamedi yalileta matokeo ya watu kuongoka, lakini pia yalileta mtafaruku miongoni mwa washirikina na makabila tofauti. Kati ya mwaka 620 mkewe na mjomba wake walikufa. Mwaka 622 Mohamedi alialikwa na waumini wa Kiislamu huko Madina iliyojulikana kama Yathrib) kukaa huko na kuwa kiongozi wao. Aliwahimiza wafuasi wake waliokuwa Maka kuhamia Yathrib na wakati wa usiku, Mohamedi na mshiriki wake wa karibu sana Abu Bakr waliondoka toka Maka kwenda Yathrib (*hejira*).

3. Maisha yake akiwa Madina hadi kifo (AD 622-632). Kwenye miaka yake 10 ya mwisho, Maisha ya Mohamedi yalibadilishwa: Aliondoka kwa Muumini mwadilifu kwenye wito wake aliyekubali dhihaka na kukataliwa na kuwa shujaa mpambanaji, mshindi, na kuwa kiongozi aliyekubalika siyo na dini tu bali na nchi pia; alibadilisha ndoa yake toka kuwa ya mke mmoja na kuwa na wake wengi na masuria . Baada ya kupigana vita vingi na watu wa Maka, Nafasi ya Mohamedi ilikuwa kwa kuwa na waumini wengi. Mwaka 630 aliongoza jeshi la watu 10,000 kwenda Maka ambako wenyeji walijisalimisha kabla ya kupigana vita. Mwezi juni mwaka 632 Mohamedi alikufa baada ya kuugua kwa muda mfupi, baadhi ya watu wanasema kifo chake kilitokana na kulishwa sumu. "Kabla ya kufa kwake, Mohamedi alitokea kuwa kiongozi wa dini na siasa asiye na mfano wake kwenye pwani yote ya Arabuni. Alianzisha jamii, kwa hakika taifa, dini inayoamini katika Mungu mmoja na unabii. Aliwafundisha na kuwataka wafuasi wake kuwa na maisha ya maombi, kufunga na kwenda kuhiji." (Braswell 2000: 15)

**B. *Historia ya Uislamu*** (angalia Braswell 2000: 47-58; Davis 2014; Emerick 2004: 313-36, 373-91; Nehs na Eric 2009a: 50-60)

1. 632-750: Wanne "walioongoza baada ya Mohamedi" "Khalifa" na Nasaba ya Umayyad. Mohamedi hakumtaja mrithi wake. Rafiki yake wa karibu, Abu Bakr, Alichaguliwa kumrithi. Alifuatiwa na, Umar (634-644), Uthman (644-656), na Ali (656-661) walichaguliwa kama Ma Khalifa. Walijulikana kama "walioongoza baada yake" Khalifa walichaguliwa kutokana na jinsi walivyoifuata Sunna na namna walivyotumia mamlaka yao. Umar, Uthman, na Ali wote waliuawa na Waislamu wenzao. Baada ya kifo cha Ali, watu wa Nasaba iitwayo Umayyads waliuongoza Ulimwengu wa Waislamu kutokea Damascus, Syria. Kwa kipindi hicho jeshi la Waislamu liliitawala Mashariki ya kati yote, Wa Byzantine na ufalme wa Persia, Kaskazini mwa Africa, Uhispania, kufikia India na China, na kuvamia Ufaransa, mahali walipozuiliwa na Charles Martel kwenye vita vya wasafiri mwaka 732.

2. 750-1258: Ukoo wa Abbasid. Kundi lililojulikana kama Abbasid liliwashinda Umayyad na kuutawala Ulimwengu wa Uislamu kutokea Baghdad, nchini Iraq. Ukoo wa Abbasid ulionekana kuwa ni "zama za dhahabu" kwa maendeleo ya Uislamu na kufanana na kile kilichoitwa "zama za giza" kwa Wakristo wa Magharibi. Utawala wa Abbasid uliangamizwa baada ya Wa Mongolia kuifagia nchi ya Uislamu kutokea Asia ya Kati. Hatimaye, WaMongolia wenyewe walijiunga na Uislamu. Ni kwenye kipindi hicho cha utawala wa Abbasids nguvu ya wakatholiki wa Roma walijaribu kurejesha Nchi Takatifu ambayo kwanza ilikuwa ya Kikristo lakini ikashindwa na Uislamu. Mfululizo wa vita ulidumu kuanzia

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwaka 1095-1291 ulipelekea kwa sehemu Wakristo kufikisha miguu yao kwenye Nchi Takatifu, lakini hatimaye walishindwa. Mfululizo huo wa vita ulipelekea Uadui kati ya Uislamu na Wakristo uliodumu hata leo.

3. 1258-1945: hali ya Uadui kwa Uislamu, Ufalme wa Ottoman, na Ukoloni. Baada ya kushindwa kwa ukoo wa Abbasid, Ulimwengu wa Uislamu ulijawa na falme nyingi kubwa ambazo zilipigana zenyewe. Hizo ni pamoja na Ufalme wa Kiajemi, Falme tofauti tofauti za Uturuki, Ufalme wa Mamluke wa Misri na Syria, Ufalme wa Mughals, na falme nyingine kote Afrika na Asia. Ufalme wa Ottoman wa Uturuki uliiteka Constantinople (kwa sasa Istanbul, Uturuki) mwaka 1453 na kufikia 1517 waliiteka Cairo, Misri na kuuhitimisha utawala wa Ukoo wa Mamluke . Utawala/falme wa Ottoman ulidumu hadi mwaka 1922. Kwa kipindi hicho Wakatholiki wa Roma waliweza kuwatoa Uislamu nje ya Uhispania mwaka1492. Nguvu ya ukoloni wa Ulaya pia ilifanikiwa kisiasa, lakini siyo kidini, kwa kuchukua sehemu kubwa ya Ulimwengu wa Uislamu na kuunda mataifa na kuyawekea mipaka. Utamaduni wa kimagharibi ulizigusa hasa Uturuki na Iran mwanzoni mwa vita kuu ya kwanza ya Dunia. Vita kuu vya pili vya Dunia vilihitimisha kipindi hicho.

4. 1945-Hali inayofananana ya sasa. Baada ya vita kuu vya pili vya Dunia wakoloni wa kimagharibi bila vita waliamua kuwapatia makoloni yao uhuru. Wakati Uingereza ilipoipatia India Uhuru mwaka 1947, Pakistan iligawanywa kama taifa huru kwa Waislamu kwa mikoa ile iliyokuwa na Waislamu wengi. Ukweli mwingine ni kwamba Mataifa ya Kiislamu yalianza kuanzishwa tangu baada ya vita kuu vya pili, hayo ni pamoja na Sudan, Afghanistan, Iran, na Somalia. Kuvunjika kwa iliyokua Urusi (USSR) kulipelekea uhuru kwa mataifa yaliyokuwa yanamilikiwa na Uislamu huko Asia ya kati. Vuguvugu la Uislamu kwenye nchi nyingine linang'ang'ania kuyafanya mataifa hayo kuwa ya Kiislamu. Majimbo 15 kaskazini mwa Nigeria yametangaza sheria za Kiislamu kuwa ndizo zitakazoongoza Mamlaka hizo. Kuanzishwa kwa taifa jipya la Israeli mwaka 1948 kulileta mabadiliko ambayo limepelekea matokeo chanya huko Mashariki ya Kati. Kulishtua umoja wa Waislamu jambo lililofanya vita baina ya Israeli na majirani zake wanne wa Kiislamu na ndicho chanzo cha uhalifu wa Uislamu unaoendelea kwa sasa. Utajiri wa mafuta uliopo kwenye mataifa ya mashariki ya kati umesababisha kupanuka kwa kasi kwa wamisionari wa Kiislamu na kuwa na ushawishi duniani kote, na Uislamu kuonekana kuwa dini inayokua kwa kasi Zaidi duniani. Dhana nyingine ya Uislamu wa kileo ni kuinuka kwa Uislamu wenye itikadi kali wanaosisitiza *jihad* ("kung'ang'ana").

## 2. YESU NA MOHAMEDI

### I. Utangulizi

Yesu na Mohamedi ni kiini cha Ukristo na Uislamu, Kwa mtiririko huo. Kama iliyo hapo juu, Mohamedi aliishi yapata miaka 600 baada ya Yesu. Kwa kuwa Uislamu wanadai kuwa wao ndio udhihirisho wa mwisho wa Mungu (Allah) ulimwenguni na kudai kuwa Yesu alikuwa sehemu ya huo mwendelezo wa mafunuo ya Mungu, siyo jambo la kushangaza kwamba Korani na Hadithi zimemzungumzia Yesu. Waandishi Waislamu wenye mtazamo wa Kikristo wa kimagharibi mara nyingi wameyasema mambo kama haya "Yesu ameshikilia nafasi kubwa ya juu kwa Uislamu, na ameheshimiwa na Aya nyingi kwenye Korani" (Emerick 2004: 222). Hata Mohamedi alisema, "Ninamfanania sana Yesu Kristo miongoni mwa wanadamu wote, na manabii wote wamezaliwa na wamama tofauti lakini wote ni wa dini moja na hakuna nabii aliyeinuka kati yangu mimi na Yesu" (Muslim: 2365b; angalia pia 2365a, c; al-Bukhari: 3442, 3443).

### II. Mtazamo wa Uislamu juu ya Yesu

Ingawa inasemekana kwamba Yesu anaheshimiwa na Uislamu, Yesu anayeheshimiwaUislamu siyo yule anayeonekana kwenye Biblia na anayeabudiwa na Wakristo. Michael na McAlister wanaonyesha, "Isa wa Korani [i.e., Yesu] siyo yule wa Historia. Utambulisho wake na tabia yake kama nabii msingi wake ni kwenye kile kinachoonekana kuwa ufunuo kwa Mohamedi Zaidi ya miaka 600 baada ya Yesu wa historia kuishi na kufa." (Michael na McAlister 2010: 79)[7]

#### A. *Yesu au Isa*

Kwenye Korani, jina Yesu ni "Isa," Ingawa tafsiri nyingi za kiingereza zina mwita jina "Yesu." "Yesu' lugha ya mama yake ilikuwa Ki Aramaiki. Wakati wa maisha yake aliitwa *Yeshua* Ki Aramaiki, na *Iesous*

[7] Christine Schirrmacher anatuonyesha jambo muhimu kwamba "wakati muislamu anaposhiriki kwenye mdahalo baina yao na Wakristo wanasisitiza kwamba 'wanakubali' watu wa biblia kama AIbrahimu au Yesu Kristo, kweli na hata kuwapa heshima, hii inamaanisha kwamba ni kwa mtazamo wa Korani juu ya Ibrahimu au Yesu ndio wenye thamani, wakati huo huo Ibrahimu na Yesu, kwa jinsi walivyoelezwa kwenye agano la kale, hawakubaliki kabisa" (Schirrmacher 2011: 26).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Kigiriki. . . . *Yeshua* kwa Kiebrania ni *Yehoshua*, likimaanisha 'BWANA ni mwokozi.' . . . Yeshua wa Nazarethi hakuwahi kuitwa *Isa*, jina ambalo Korani ilimpa. Halina maana yeyote kwa Wakristo wanaozungumza Kiarabu kumtaja Yesu kama *Yasou* (kutokana na *Yeshua*), na kamwe hawakuwahi kumwita *Isa*." (Michael na McAlister 2010: 79) Jina *Isa* "bila shaka limetokana na jina la WaNestoria *Isho.* Hakuna kumbukumbu yeyote mahali popote kwenye historia yaKikristo ambayo labda inayoonyesha jina ngeni la Yesu kwenye Korani. Kwakuwa Waarabu wanaongea lugha sawa na ambayo inafanana na Kiebrania tungetarajia jina lake liwe Yasu' kama Wakristo wanavyolitumia." (Gilchrist 1994: 8)

**B.** ***Ukoo na kuzaliwa kwa Yesu***

Maelezo ya Uislamu kuhusu kuzaliwa kwa Yesu ni kama ifuatavyo. Mtetezi wa Uislamu Ahmed Deedat, "Anaeleza kwamba Bibi yake na Yesu ambaye ni, Hannah, hapo awali alikuwa mgumba. Aliumimina moyo wake kwa Mungu: Kama kweli Mungu angempa mtoto, angemtoa mtoto huyo hekaluni kwa ajili ya kumtumikia Mungu huko. Mungu aliyatakabali maombi yake na Maria akazaliwa." (Deedat 2002: 9) Kwa maelezo ya Uislamu, 'Imram [Kiebrania = Amram] alikuwa baba yake na Mariamu (**Q. 3:35-36; 66:12**).[8] Mariamu alikabidhiwa kwa Zechariah, baba yake na Yohana (Yohan mbatizaji) ili amlee (**Q. 3:36-37, 39-41; 19:7**). Ingawa Biblia inasema Mariamu alichumbiwa na baadaye kuolewa na Yusufu (**Math 1:18-24**), "Yusufu hayupo kwenye toleo la Kiislamu la maisha ya Yesu" (Emerick 2004: 223). Kwenye Biblia (**Math 1:18-25**) na kwenye Korani (**Q. 19:20-22**) zinakubali kwamba Mariamu alikuwa bikira wakati anapata mimba kwa nguvu zisizo za kawaida, lakini kwa mujibu wa Korani Mariamu alijifungua mwenyewe maeneo ya nje ya mji chini ya mti wa mtende, siyo Bethlehem akiwa na mume wake Yusufu ili kuutimiza unabii (**Q. 19:22-26;** linganisha na **Math 2:1-6; Luka 2:1-7**).

Deedat anachanganya kuzaliwa kwa Maria na historia ya Biblia kuhusiana na Hannah kumlingana Bwana kwa ajili ya mtoto wa kiume na baadaye kuzaliwa kwa Samueli (**1 Sam 1:1-28**). Kulingana na **Hes 26:59**, mke wa Amramu ['Imram's] alikuwa Yokebedi, siyo Hannah. Yokebedi *"alimzalia Amramu Aaron na Musa na dada yao Miriam"* (angalia pia **Kut 6:20; 15:20**). Kwa kweli, **Q. 20:30** inamnukuu Musa akimwita *"Aaron, kaka yangu."* **Q. 19:28** na kumwita Mariamu*"dada yake na Aaron."* Gilchrist anaeleza, "Mahali pengine kwenye Korani neno *ukhtun* (dada) wakati wote lilitumika kwa dada wa karibu kwenye Sura al-Nisa 4:12, 23, 176) na kwa matumizi ya neno hili kwa Mariamu linaweza kumaanisha tu 'dada wa damu wa Haruni'." (Gilchrist 2010: 5; angalia pia "kamusi ya Korani" 2009-2017: **Q. 19:28**, *yāukh'ta*) Yote haya yanaonyesha kwamba Mohamedi (yaani Korani) inamchanganya Maria wa agano jipya ma Miriamu wa agano la kale, aliyeishi miaka 1000 iliyopita.[9]

---

[8] 'Imram ni matamshi ya kiarabu ya Amram kiebrania ("Amram" 2019: Kwenye Korani).

[9] Ali anajaribu kushughulikia tatizo lililo wazi kwamba Maria aliishi Zaidi ya miaka 1000 baada ya anayedhaniwa kuwa baba yake 'amramu na kaka Musa na Haruni kwa kusema, "Haruni, kaka yake na Musa, walikuwa wa kwanza kwenye orodha ya makuhani wa Israeli. Maria na binamu yake Elisabeth (mama yake na Yohana) walikuwa wa familia ya kikuhani, na kwa hiyo walikuwa 'dada zake na Haruni na mabinti wa Amramu (ambaye alikuwa baba yake na Haruni)." (Ali 2006: Q. 19:28n.2481) Hata hivyo, "Tatizo ni kwamba Maria hakutokana na ukoo wa Haruni hata kidogo! Haruni alikuwa kuhani Mlawi, akitokea huko na kaka yake Musa wote wa Lawi, mmoja wa watoto wa Yakobo. Kwa maana nyingine Maria alitokea Yuda, mmoja wa vijana wengine wa Yakobo, Akitokea kwenye ukoo wa Daudi (Luka 1:32). Hata hakutokana na ukoo wa Haruni." (Gilchrist 2010: 5, angalia **Math 1:2; Luka 3:33; Waeb 7:14** yanayoonyesha kwamba Maria ni wa Ukoo wa Yuda; angalia pia Katz, "Ni maria" n.d.; Gilchrist 2015: 56-57). Halali na Khan wanajaribu kuliondoa tatizo kwa kusema, "Huyu Haruni (Aaron) siyo kaka wa Musa (Moses), lakini alikuwa mmoja wa watu maarufu wa kipindi cha Mariamu (Mary)" (Hilali na Khan 1998: 405 n.1; angalia pia Haleem 2005: Q. 19:28n.b).

Maelezo binafsi ya Mohamedi alipoulizwa juu ya hili yalikuwa hivi, "Watu (watu wa kale) huwapa majina (watu wao) kulingana na majina ya manabii na watu maarufu wa wakati wao" (Muslim: 2135). Jaribio la Mohamedi kutolea maelezo tatizo hili unadhihirisha uongo kwenye Korani yenyewe, kwa kuwa "Korani inamwita Mariamu 'dada yake na Haruni' siyo kutokana na desturi ya 'watu wa kale' lakini kwa sababu, kulingana na Korani, Maria alikuwa binti yake na Amramu kwa kuzaliwa, uzazi ambao umeelezwa kwa kina kwenye Korani. Kwa mtiririko huo, kwa kuwa Korani inahusika, Mariamu aliitwa'Dda wa Haruni' na 'binti wa Amramu' kwa sababu ni uzao moja kwa moja wa wazazi wa Haruni." (Sundiata 2006: 130;angalia pia Spencer 2009: 138) Gilchrist anaongeza, "Majibu ya Mohamedi hayana ushawishi. Hakuna mwingine kwenye Korani aliyetajwa kama dada wa mababu." (Gilchrist 2015: 57) Zaidi, "pia ni zaidi ya uwezekano kwamba Haruni angeweza kuitwa kaka (*akha*) wa Musa kwenye Korani, mara nyingi iwezekanavyo, kwa mtazamo wa moja kwa moja kama Mariamu aliitwa dada yake (*ukhta*) kwa maana ya mfano." (Gilchrist 2010: 5; na kama, ilivyo kwenye Makala kuu, neno lililotumiwa linamaanisha "dada wa karibu wa kuzaliwa naye," siyo "babu/baba"; kwenye ukurasa wa 3-7 Gilchrist anazungumzia makosa mengine ya Uislamu kuhusiana na kizazi cha Yesu)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

### C. *Kulingana na Uislamu, Yesu hakusulubiwa wala kufufuka*

Tofauti ya msingi na ya muhimu kati ya Yesu wa Uislamu na yule wa Biblia, ni kwamba, Yesu wa historia huingia kwa kina moyoni na kwamba, *Yesu ni nani* na *Yesu alifanya nini.* Kusulubiwa ni muhimu kwa sababu ya ulazima wake kwa Kristo kama msamaha na upatanisho kwa dhambi za wanadamu na kwa kufufuka. Yusuf Ali alilitambua hili: "Waamini wa makanisa ya Kikristo wanalichukulia hili kuwa ni fundisho la msingi kwamba maisha yake yalipelekwa msalabani, kwamba alikufa na alizikwa, na kwamba kwa siku ya tatu alifufuka akiwa na mwili wake wenye majeraha, na alitembea na kuwasiliana (kuzungumza),na alikula na wanafunzi wake, na baadaye alichukuliwa mwili wake kwenda mbinguni. Hili ni muhimu kwa fundisho la Kitheolojia la sadaka ya damu, upatanisho na msamaha wa dhambi, jambo linalokataliwa na Uislamu." (Ali 2006: Q. 4:157n.663) Islam wanyakataa mafundisho hayo yote ya msingi.

Uislamu kukataa kusulubiwa kwa Yesu, hawaonyeshi unabii wowote wa Agano la kale unaothibitisha hayo na kutimia kwa Kusulubiwa; [10] wala hawaonyeshi kifungu chochote cha Agano Jipya wala ushahidi wa Kihistoria wa kusulubiwa na kufufuka kwake. Zaidi ya hayo, kwa kukataa kusulubiwa na"fundisho la Kitheolojia la sadaka ya damu, upatanisho na msamaha wa dhambi," Kwa kutokujua Waislamu wanayakataa mambo muhimu matano kwenye Uislamu na kwenye Korani:

- Kwanza, kukataa upatanisho na msamaha, wanakataa kwa kile ambacho kwa mioyo ya dhati ya Uyahudi na Ukristo walikifanya kwa zaidi ya miaka 2000 na kilichomtangulia Mohamedi. Hata hivyo wanakataa madai yao kuwa Uislamu ni mageuzi ya mwisho ya Uyahudi na Ukristo. Sababu ni kwamba "wazo la msingi la sadaka kwenye Agano la kale ni mbadala, ambao tena unaonekana kuyagusa mambo mengine yote—fidia na ukombozi, adhabu na msamaha" (Edersheim 1881: 81; angalia pia n.97, hapo chini, na maandiko yanayofanana). Kwa mbadala wa maisha yasiyo na hatia na yale ya upande wenye hatia, ambayo ni moyo wa mbadala wa fidia, ambayo kwanza ilionekana kwenye sadaka ya Yesu pale msalabani.
- Pili, Kwa kukataa mbadala wa fidia wanakataa maandiko mengi yanayoeleza kuwa Korani inathibitisha ufunuo wa awali wa Biblia (angalia **Q. 2:41, 89, 97; 3:3; 4:47; 5:15, 48; 6:90, 92; 10:37; 12:111; 35:31; 46:9, 12, 30**).
- Tatu, kwenye **Q. 11:70, 74-76** malaika alimtokea Ibrahimu, alimwambia walikuwa wametumwa kuiangamiza Sodoma (alikokuwa anaishi Lutu), na baadaye Ibrahimu *"alianza kuhojiana nasi kwa habari ya watu wa Lutu"* (Sahih). Haya ni maelezo ya Korani yanayozungumzia **Mwanzo 18:16-33** pale Ibrahimu alipodai kwamba Mungu *"hatawaangamiza wenye haki pamoja na waovu,"* na Mungu alikubali kwamba atausamehe mji wote ikiwa tu atawaona watu kumi tu wenye haki ndani yake. Wakati ambapo Korani haitoi maelezo ya kina juu ya mazungumzo ya Ibrahimu, Mchambuzi na mwanahistoria Muislamu anakubali

[10]

| Unabii | Chanzo Agano la Kale | Kutimia Agano Jipya |
|---|---|---|
| 1. kusalitiwa na marafiki | **Zab 41:9; 55:12-14** | **Math 10:4; 26:47-50; 13:21-27; Luka 22:19-23** |
| 2. kusalitiwa kwa vipande 30 | **Zek 11:12** | **Math 26:15; 27:3** |
| 3. Fedha kutupwa | **Zek 11:13** | **Math 27:5** |
| 4. Fedha kulipwa kwa mfinyanzi | **Zek 11:13** | **Math 27:6-10** |
| 5. Kusahauliwa na wanafunzi | **Zek 13:7** | **Math 26:31, 69-74; Marko 14:27, 50** |
| 6. Kimya mbele ya washtaki | **Isa 53:7** | **Math 27:12; Matendo 8:32-35** |
| 7. Kupigwa na kutemewa mate | **Isa 50:6; 53:5** | **Math 26:67; 27:26; Marko 10:33-34** |
| 8. Kudhihakiwa | **Zab 22:7-8** | **Math 27:31; Luka 22:63-65** |
| 9. Kutobolew miguu na mikono | **Zab 22:16; Zek 12:10** | **Luka 23:33; Yohana 20:25-27** |
| 10. Kuteswa kwa dhambi za wengine | **Isa 53:5-6, 8, 10-12** | **Warumi 4:25; 1 Cor 15:3** |
| 11. Kufa pamoja na wakosaji | **Isa 53:12** | **Math 27:38; Marko 15:27-28; Luka 22:37** |
| 12. Kuwaombea watesi | **Isa 53:12** | **Luka 23:34** |
| 13. Mavazi kupigiwa kura | **Zab 22:18** | **Yohana 19:23-24** |
| 14. Marafiki kusimama mbali | **Zab 38:11** | **Math 27:55-56; Marko 15:40; Luka 23:49** |
| 15. Watu kutikisa vichwa vyao | **Zab 22:7** | **Math 27:39** |
| 16. Watu kumtazama | **Zab 22:17** | **Luka 23:35** |
| 17. Kuona kiu | **Zab 22:15; 69:21** | **Yohana 19:28** |
| 18. Kupewa siki na sifongo | **Zab 69:21** | **Yohana 19:28-29; Math 27:34** |
| 19. Kulia aliposahauliwa na Mungu | **Zab 22:1** | **Math 27:46** |
| 20. Kuisalimisha Roho yake kwa Mungu | **Zab 31:5** | **Luka 23:46** |
| 21. Mifupa yake haikuvunjika | **Zab 34:20** | **Yohana 19:33** |
| 22. Alichomwa ubavuni | **Zek 12:10** | **Yohana 19:34-37** |
| 23. Alikata Roho | **Zab 22:14; 69:20** | **Yohana 19:34** |
| 24. Giza juu ya nchi | **Amos 8:9** | **Math 27:45** |
| 25. Kuzikwa kwenye kaburi la tajiri | **Isa 53:9** | **Math 27:57-60** |

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kwamba Ibrahimu alidai kwamba mji mzima ungesamehewa ikiwa tu wangeonekana wenye haki wachache ndani yake. *Tafsir Ibn Kathir* anasema, "Walipomweleza [malaika] kuhusu jambo hilo [mpango wa kuiangamiza Sodoma], alisema nao kama Sa'id bin Jubayr anavyoelezea kuhusiana na Aya hiyo. Sa'id alisema: Wakati Gabrieli na malaika wengine waliokuwa pamoja naye walipomwendea Ibrahimu, walimwambia, (Amini, tunaenda kuwaangamiza watu wa mji huu.) Ibrahimu aliwaambia, 'Mtauangamiza mji ambao una waamini miatatu ndani yake' Wakasema 'Hapana', Akawaambia tena, 'Mtauangamiza mji ambao ndani yake wapo waamini miambili' Wakasema, 'Hapana.' Akasema, 'Mtauangamiza mji ambao una waamini arobaini ndani yake' Wakasema, 'Hapana.' Akasema tena, 'Thelathini' Walizidi kujibu, 'Hapana.' Haya yaliendelea hata alipowaambia, 'Watano' Wakasema, 'Hapana.' Tena akasema, 'Mnawaza nini ikiwa atakuwepo mtu mmoja Muislamu mjini, mtauangamiza' Wakasema, 'Hapana.'" (Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 11:74, maoni). Mwanazuoni Muislamu na mwanahistoria maarufu Abu Ja'far Mohamedi ibn Jarir al-Tabari (839-923) kwenye *Historia* anataarifu kwamba wachambuzi wengine wa Kiislamu wanasema kwamba mji utasamehewa kama wapo kumi na wanne, kumi, au waamini watano (al-Tabari 1987a: 116). Hii ni kanuni ya fidia mbadala ambayo ilikuwa ikiimarishwa, i.e., watu hawapaswi kuhukumiwa kupata maumivu kwa sababu ya dhambi zao au tabia zao; badala yake, *haki ya mtu mmoja yaweza kuwaokoa* wenye dhambi.

- Nne, **Q. 37:102-107** kwa wazi inathibitisha andiko la **Mwanzo 22:1-14** ambalo Mungu alimwambia Ibrahimu kumtoa mwanaye lakini alitoa mbadala wa kondoo kama sadaka mbadala kwa dakika za mwisho.[11] **Q. 37:107** (Hilali-Khan) inasema, *"Tunamfidia kwa sadaka iliyo kuu."* Huko ni *kukuzwa kwa kanuni ya fidia mbadala*. Mchambuzi Muislamu anatolea maelezo kwenye Biblia kuhusiana na fidia mbadala ya kondoo (angalia Ali 2006: Q. 37:107n.4108; A'la Mawdudi n.d.: Q. 37:107n.66; Jalal 2017: Q. 37:107, maoni). Zaidi ya hayo, kila mwaka Waislamu wanasherehekea tukio hili kwa kumchinja mnyama kwenye sherehe yao kubwa ya *Eidu'l-Adha* ("Sherehe ya kutoa sadaka"). Mawdudi anasema kwamba "Allah amelifanya hili kuwa desturi mpaka siku ya ufufuo kwamba waamini wote watapaswa kutoa sadaka ya mnyama kwa siku na kwa tarehe hiyo moja kwa dunia nzima ili kuihuisha kumbukumbu kubwa na ya tukio la kipekee linalodhihirisha uaminifu na Ibada" (A'la Mawdudi n.d.: Q. 37:107n.66; angalia pia Asad 1980: Q. 37:107n.43).
- Tano, Waislamu wanayo desturi iitwayo *aqiqah* siyo ya kisheria sana lakini "inahimizwa sana" ("Aqiqah" 2013: "Kusudi la Aqiqah ninini?"; angalia pia Malik: book 26, no. 7). *Aqiqah* ni sadaka ya mnyama inayotolewa badala ya mtoto mchanga aliyezaliwa, Siku saba kamili baada ya kuzaliwa. *Aqiqah* ina kusudi la mbadala au ukombozi. Mtheolojia, mchambuzi, na mwanasheria maarufu wa Kiislamu Imam Ibn Al-Qayyim (1292-1350) amekiri kuwa fidia na ukombozi ndilo kusudi la aqiqah. Amesema kwamba miongoni mwa faida zipatikanazo kutokana na aqiqah ni: "1) Ni sadaka ambayo inamaanisha kumleta mtoto kwa Allah mara anapokuja duniani. 2) Ni fidia ili kwamba mchanga huyo aweze kuwakomboa wazazi wake. 3) Ni sadaka ambayo mchanga huyo anakombolewa kama Allah alivyomkomboa Ishmaeli kwa kondoo" ("Sunnah za nabii" 2019: Faida za Aqiqah?)

Kwa wengi, Korani na Uislamu wanakubaliana na kanuni ya mbadala wa fidia wakati huo huo kimsingi wanaikataa.

Kusulubiwa kunakataliwa na Uislamu kwa sababu ya msitari mmoja tu kwenye Korani ulioandikwa miaka, ulioandikwa Zaidi ya miaka 600 baada ya maisha ya Yesu, **Q. 4:157-58**: *"Walisema (kwa majivuno), "Tulimwua Kristo Yesu mwana wa Mariamu,Mjumbe wa Allah";-lakini hawakumwua, wala hawakumsulubisha,lakini hivyo ndivyo ilivyowatokea, na wengi waliokuwa na mtazamo tofauti walikuwa na shaka kuu, bila kuwa na (uhakika) ufahamu, lakini kuwa na dhana tu ya kuifuata, kwa kuwa kwa kweli hawakumwua. Kwakweli, Allah alimwinua kwa ajili yake mwenyewe; na Allah aliinuliwa kwa nguvu, busara."*[12] Ingawa Korani inakataa kwamba Yesu hakusulubiwa, Dirks analiweka hili wazi kwamba "Korani haisemi kwamba hakukuwa na kusulubiwa. Badala yake, *Korani* inaeleza kwamba siyo Yesu Kristo aliyesulubiwa, ingawa ilifanyika kuonekana kwamba alikuwa yeye. Kwa kifupi, ufa, unaowatenganisha Uislamu na Ukristo na kuhusiana na Kusulubiwa, siyo kwamba kulikuwa au hakukuwa na kusulubiwa kwa wakati na mahali ambapo *Agano jipya* inalizungumzia, lakini tu kwamba mtu aliyesulubiwa alikuwa ni Yesu." (Dirks 2008: 78)

Kwa kukubali kwamba kulikuwa na kusulubiwa kwa wakati na mahali ambapo Agano jipya linasema,

[11] Ingawa Waislamu wengi wanaamini kuwa mtoto aliyehusika alikuwa Ishmaeli, Korani haithibitishi kwamba alikuwa Ishmaeli au Isaka. Kwa mengi zaidi, angalia namba 13, hapo juu.

[12] Kevin Greeson anaonyesha kwamba **Q. 4:157** "haisemi kwamba Isa hakufa. Inachokisema tu ni kwamba Wayahudi hawakumwua. *Injili* anakubali! Wayahudi hawakumsulubisha Yesu. Hawakuwa na mamlaka ya kumsulubisha. Walikuwa wanamilikiwa na Warumi chini ya utawala Warumi. . . . Walipaswa wamrudishe Yesu kwa Warumi na kutumaini kwamba Warumi wangemsulubisha Yesu badala yao. Na Warumi, siyo Wayahudi, walimsulubisha Yeye." (Greeson 2007: 141; angalia pia Reynolds 2018: 181)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Waislamu hawana uhakika na kile kilichotokea kwa ile siku ambayo Kristo (inaaminika) alisulubiwa. "Desturi za WaSunni zinaonyesha baadhi ya mitazamo tofauti ambayo ilipata kukubalika. Hapakuwahi kuwa na mtazamo mmoja pekee." (Larson 2008: 7) Mitazamo ya wengi ni kwamba mtu mwingine alikuwa mbadala wa Yesu na alisulubiwa mahali pake. Mchambuzi maarufu kwenye Korani *Tafsir al-Jalalayn* anaendeleza, "Mtu aliyechinjwa na kusulubiwa, ambaye alikuwa msaidizi wao [Wayahudi], alipewa mfanano wa Yesu. Kwa maneno mengine, Mungu alimvalisha mtu mwingine sura yake [Yesu] na kwa hiyo Wayahudi walifikiri kuwa alikuwa ni yeye [Yesu]." (Jalal 2017: Q. 4:157, maoni) Emerick anasema, "Ni nani aliyesulubiwa siku hii ya kupendeza? Ikiwa mtu yeyote aliuawa, itakuwa ni yule mtu aliyemsaliti Yesu [i.e., Yuda Iskariote]. Kama alionekana mwanana kama Yesu, kwenye hali ya mkanganyiko Warumi wa Kaukasia wangemkamata na kumwua, wakidhani ya kuwa Wasemiti wote wanafanana." (Emerick 2004: 224) Mufti Mohamedi Madani anasema kwamba "Allah aliubadilisha mwonekano wa mlinzi [wa nyumba ambayo Yesu alikuwa amefungwa]. . . . Kwa sababu hiyo, mlinzi alipelekwa kuuawa." (Madani 2005: 1:388) Dirks anaendeleza kwamba "Barnaba" aliyewekwa huru na Pontio Pilato (**Math 27:15-26; Marko 15:6-15; Luka 23:17-25; Yohana 18:39-40**) hakika alikuwa ni Yesu Kristo. "Yesu" aliyesulubiwa alikuwa "mwanamageuzi muasi aliyejulikana kama Yesu, Mgalilaya, aliyedai kuwa yeye ni mfalme wa Wayahudi" (Dirks 2008: 93-108, 111). Hata hivyo, Dirks pia anaelezea kwamba mtu aliyesulubiwa yawezekana alikuwa "Yuda Iskariote; Simon Mkirene; Anayefanana naye [i.e.,mtu mwenye sura ya kufanana na mtu mwingine] Yesu Kristo; [au] mmoja ambaye hakutambulishwa" (Ibid.: 111; angalia pia Ayoub 1980: 94-103 kwa aina nyingine ya "nadharia ya mbadala).

Yusuf Ali kwenye maoni yake **Q. 4:158** anasema, "mwingine [mtazamo] unasema kwamba alikufa (5:117) lakini siyo kwa wakati ule aliopaswa kusulubiwa, na kwamba 'aliinuliwa juu' kwenda kwa Allah inamaanisha kwamba badala ya kuaibishwa kama mtenda maovu, kama walivyokusudia Wayahudi,alikuwa kinyume na hayo kwa kuheshimiwa na Allah kama Mjumbe wake: (angalia 4:159)" (Ali 2006: Q. 4:158n.664). Fazlul Karim, baada ya nukuu **Q. 4:157** na **3:55**, anasema, "Aya hii haikatai kwamba Yesu alipigiliwa misumari msalabani, lakini wanakuwa kinyume na kwamba alifia pale msalabani. Hakuna aliyeshuhudia kifo chake lakini ilifikirika kwamba alikufa kwa sababu ya kupigiliwa misumari." (Karim 1939: 4:79n.1) Adil Salahi, mhariri wa "Mtazamo wa Uislamu" aliandika kwenye gazeti la *Habari za Kiarabu* la Saudi Arabia, aliongeza, "Wanazuoni wengi, wengine wakiwa mashuhuri sana, wameuelezea mtazamo huu na kusema kwamba neno hili [*mutawaffīka*] ambalo limetokea mara tatu kwenye Aya tofauti kwenye Korani [**Q. 3:55; 5:117; 19:33**], linamaanisha kwamba Yesu Kristo alikufa kifo cha kawaida" (Salahi 1992: 9; angalia pia Mohamedi 2003: 3-82 kwa ushahidi utokanao na vyanzo vya Waislamu kwanini Uislamu wa Kundi la Ahmadiyya wanahitimisha kwamba Yesu alikufa kifo cha kawaida).

Pamoja na kwamba mitazamo ya awali ilisema kwambaYesu hakusulubiwa wala hakufa msalabani, baadhi ya Uislamu wanakubali kwamba Yesu *alikufa msalabani*. Tabari (1987b: 120-25), Ayoub (1980: 91-121), Cumming (2001: 1-14), Larson (2008: 5-7), na Shamoun ("Al-Tabari" n.d.) wanajadili mitazamo mingi ya Uislamu kwenye historia ya kwamba ninini kilichotokea wakati Kristo (inadaiwa) aliposulubiwa, pamoja na mtazamo kwamba Yesu alikufa msalabani. Professor Ayoub anaendelea kusema kwamba Korani "haikatai kifo cha Kristo. . . . Kifo cha Yesu kimesimuliwa mara nyingi na kwenye maandiko tofauti tofauti." (Ayoub 1980: 106, nukuu **Q. 3:55; 5:117; 19:33**) Kwa mfano, **Q. 3:55** inasema, *"Tazama! Allah anasema: "Ee Yesu! <u>Nitakuchukua wewe na kukuinua</u> kwa ajili yangu mwenyewe na kukusafisha wewe (na uongo) wa wale wenye kukufuru"*]; Neno lililotafsiriwa *"nitakuchukua wewe"* (*mutawaffīka*) ni kihusishi tendaji cha neno *tawaffā.* Ambalo linamaanisha "kufa, kusababisha kifo, kupeleka *kifoni* " ("Kamusi ya Korani" 2009-2017:Q. 3:55, *mutawaffīka*; Shamoun, "Al-Tabari" [Nyongeza Maana ya Tawaffa kwenye Korani] n.d.). Gabriel Said Reynolds anadhihirisha, "Neno la Kiarabu (*tawaffā*) nyuma ya tafsiri [ya **Q. 3:55**] hutumika wakati wote kwenye Korani kuonyesha ile maana ya kwamba Mungu anatenganisha nafsi na mwili kwenye kifo, kwamba, Huchukua uhai wa mtu (kumbuka, kwa mfano, maombi kwenye 7:26: 'Bwana! Tujalie uvumilivu, na *tupe kufa* [*tawaffanā*] kama *Waislamu.*')" Reynolds 2018: 124.Kwa kweli, tafsiri ya Asad ya **Q. 3:55** inasomeka, *"Lo! Mungu alisema: "Ee Yesu! Hakika, <u>Nitakusababisha ufe</u>, na nitakuinua kwangu,na kukutakasa wewe [mbele ya] wale walioamua kuukataa ukweli"* (angalia pia Shakir: *"Allah alisema: Ee Isa, nitakwenda <u>kuhitimisha kipindi chako cha kukaa (hapa duniani)</u> na kukufanya uje kwangu na kukutakasa wewe na wale wasioamini"*).

Ya kufanana, **Q. 5:117** inasema, *"Mimi [akimaanisha Yesu] nalikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nakaa katikati yao; wakati <u>utakaponiinua juu</u> nitakuwa mlinzi juu yao, na shahidi juu yao mambo yote."* Neno lililotafsiriwa *"kuniinua juu"* (*tawaffaytanī*) ni muundo wa kitenzi wa neno hilo hilo, *tawaffā* na likimaanisha "kufa, kusababisha kifo, kupeleka *kifoni*" ("Kamusi ya Korani" 2009-2017: Q. 5:117, *tawaffaytanī*; Shamoun, "Al-Tabari" [Nyongeza: Maana ya Tawaffa kwenye Korani] n.d.). Shakir tafsiri hiyo **Q. 5:117** kama *"Nalikuwa shahidi wao wakati nikiwa pamoja nao, lakini wakati <u>utakaponisababishia kufa</u>, Nitakuwa mlinzi wao."* Tafsiri ya Asad inayofanana na Aya hii kama *"Nalikuwa shahidi wa yale waliyoyafanya wakati nikiwa katikati yao;*

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

*lakini wakati utakaponisababishia kufa, Wewe peke yako utakuwa mlinzi wao."* Asad anaonyesha kwamba swali la Allah kwa Yesu kwenye **Q. 5:116** (*"Ee Yesu mwana wa Mariamu! Wewe uliwaambia watu, mniabudu Mimi na mama yangu kama miungu na wamdharau Allah'?"*) Lazima lichukue nafasi "'baada ya kifo cha Yesu': huu ni ushahidi tosha toka kwa Yesu kitakachofuata baadaye, kwa wakati uliopita, kwa kifo chake mwenyewe ('utakaponisababishia kifo') kwenye Aya ya 117" (Asad 1980: Q. 5:116n.139; angalia pia Reynolds 2018: 181).

Hatimaye, **Q. 19:33** kama mtoto mchanga Yesu alisema, *"Amani ilikuwa nami siku nilipozaliwa, siku ile nitakapokufa, na siku ile nitakapoinuliwa juu kwenye uzima (tena)!"* Hili linafanana na lile alilolisema nabii Yohana (Yohana mbatizaji) kwenye **Q. 19:15**, *"Amani ilikuwa juu yake siku alipozaliwa, siku atakapokufa, na siku ile atakapoinuliwa kwenye uzima (tena)!"* Wislamu wanatambua kuwa Yohana alikufa "kifo kisichokuwa cha haki kwenye mikono ya watesi wake" (Ali 2006: Q. 19:15n. 2469; angalia pia A'la Mawdudi n.d.: Q. 19:15n.12). Kwa kuwa jambo lilelile lilisemwa kwa Yohana na Yesu na kwa mtiririko uleule na Yohana kwa hakika aliuawa, andiko linashauri kwamba Yesu hali kadhalika aliuawa. Kwa hakika, maelezo mwishoni mwa **Q. 19:33** *"kwamba nitainuliwa juu kwenye uzima (tena)"* haimaanishi chochote kama siyo kwamba angekufa kwanza. *Tafsir Ibn Abbas* anatafsiri neno hili kama ifuatavyo, "(Amani ilikuwa juu yangu siku nilipozaliwa) Nilikuwa salama kutokana na mashambulizi ya Shetani siku nilipozaliwa, (na siku nitakapokufa) na salama kutokana na mkandamizo wa kaburi siku nitakapokufa, (na siku nitakapoinuliwa kwenye uzima) *Nitakapofufuliwa hai kutoka kaburini*!" (Ibn Abbas 2016: Q. 19:33, maoni, fafanuzi imeongezwa; angalia pia Madani 2005: 3:379) tafsiri yaIbn Abbas na Madani **Q. 19:33** kama inavyozungumzia *kufufuka* kwa Yesu (siyo kwa kudhania kuwa yu hai mbinguni) inakubaliana na Biblia kuhusu Yesu kufa, kuzikwa, na kufufuka. Vivyo hivyo, Uislamu wengi wanaamini Yesu alichukuliwa mbinguni bila kufa; na Uislamu wote (pamoja na wachache wale wanaoamini Yesu alikufa) wanakataa kufufuliwa kwa mwili wa Kristo kama inenavyo Biblia.

**D. *Kulingana na Uislamu, Yesu ni nabii lakini siyo mwana wa Mungu***

Msingi wa awali wa Uislamu kuhusu Yesu ni kwamba, Yesu alikuwa nabii wa Allah, lakini siyo mwana wa Mungu (Dirks 2008: 35). Uislamu wanakataa kwamba Yesu, kama manabii wengine wote (pamoja na Mohamedi), walikuwa viumbe, wanadamu wa kufa tu. **Q. 5:75** inasema, *"Kristo mwana wa Mariamu hakuwa chochote Zaidi ya mjumbe; walikuwepo wajumbe wengine ambao walimtangulia na kufa kabla yake. Mama yake alikuwa mwanamke mkweli. Wote walikuwa wanakula chakula chao cha kila siku."* Kwenye maoni yake kuhusu Aya hii, Mawdudi anasema, "Kwa maneno haya machache Fundisho la Wakristo la Utatu ni la uongo. Asili ya Masihi iko wazi kutokana na ukweli tuliopewa hapa; alikuwa mwanadamu wa kawaida. Alizaliwa kutoka kwenye tumbo la mwanamke, alikuwa na ukoo unaojulikana, waliokuwa na mwili wa kawaida, ambao unahusika na ukomo wote wa mwanadamu na wenye tabia zote za kibinadamu. Alilala, kula, aliyejisikia vibaya kwenye joto na baridi na alikuwa mwanadamu ambaye hata alijaribiwa na shetani. Ni kwa jinsi gani mtu mwenye ufahamu anaweza kuamini kwamba hiki kiumbe kilikuwa Mungu au mshiriki au mmoja wa anayehusika na ukuu wa Mungu. Lakini Wakristo wanazidi kusisitiza juu ya Utatu wa Masihi, ambaye mwili wake kwenye maandiko yao matakatifu unaonyeshwa kama wa mwanadamu." (A'la Mawdudi n.d.: Q. 5:75n.100)

Korani pia inasema, *"Enyi watu wa Kitabu! Msijiongezee kwenye dini yenu: Wala msiseme ya kwamba Allah anawiwa chochote Zaidi ya Ukweli. Kristo Yesu Mwana wa Mariamu alikuwa (siyo Zaidi ya) mjumbe wa Allah, na neno lake, lililosemwa na Mariamu, na Roho aliyokuwa nayo: hivyo mwamini Allah na Wajumbe wake. Jiepushe kuuzungumzia 'Utatu': itakuwa heri kwako: kuwa Allah ni mmoja: Utukufu una yeye: (wa kuinuliwa sana ni yeye) Zaidi ya kuwa na mwana. Yeye ndiye mmiliki wa vyote mbinguni na duniani. Na anajitosheleza yeye Allah na mwenye mpangilio wa mambo yote."* (**Q. 4:171**; angalia pia **Q. 2:116; 5:17, 72-73, 116-17; 6:101; 9:30; 10:68; 17:111; 18:4-5; 19:35, 88-92; 21:26; 23:91; 39:4; 43:81-82; 72:3; 112:3**). Kwa somo hilo **Q. 4:171**, Mohamedi Asad anasema, "Mjadala kwenye Aya hii, ambayo inaelezea kwa wazi ubinadamu na asili ya Yesu na kukataa kuamini kwenye Uungu wake, Korani inasema kwa Yesu, kama viumbe vingine vyote, ni nafsi iliyoumbwa Naye'" (Asad 1980: Q. 4:171n.181; angalia pia Ali 2006: Q. 4:171n.675-676; A'la Mawdudi n.d.: Q. 4:171n.212-218).

Mtetezi wa Uislamu pia anaonyesha kutoka kwenye Biblia mahali ambapo Yesu aliwaambia watu wamwabudu Mungu (**Math 4:10; 19:16-17; 23:8-9; Marko 12:28-34; Yohana 17:3; 20:17**), alimwita Mungu"Baba" (jina ambalo halikutajwa kwa Yesu) (**Math 5:48; 6:1; 7:21; 11:25; 26:39**), ombeni kwa Baba (**Math 14:23**), anasema kwamba ni Baba pekee ajuaye siku na saa ya kuja kwake mara ya pili (**Math 24:36**), alijiita mwenyewe "nabii" (**Luka 4:24**), na alijulikana kama nabii (**Math 21:45-46**) (angaliaAl-Hilali 1998: 904-09; Ali 2006: Q. 5:72n.782). Walihitimisha kwamba "Yesu alikuwa mtiifu kwa Allah na kwamba hakuwa na sehemu kwenye Uungu" (Al-Hilali 1998: 909; angalia pia Ali 2006: Q. 5:117n.831; A'la Mawdudi n.d.: Q. 43:64n.57).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Wakristo hawakatai *kweli za* Biblia zilizosemwa na watetezi wa Uislamu kuhusiana na ubinadamu wa Yesu; kwa hakika , Wakristo *wanakubali* kabisa kwamba Kristo alikuwa mwanadamu kamili, lakini siyo Biblia wala *Yesu mwenyewe* aliyesema kwamba Yesu alikuwa mwanadamu *pekee*. Vifungu vya Biblia vilivyonukuliwa na Uislamu *vimechaguliwa sana.* Wameondoa vifungu vingi vya kwenye Biblia ambavyo vinawafanya Wakristo waamini hivyo- kwamba Yesu ni Zaidi *ya kuwa* mtu wa kufa lakini alikuwa Mungu aliyekuja duniani *kama mwanadamu.* Abbas Sundiata alieleza, "Korani nyakati zote imewapotosha Uislamu kudhani kwamba Wakristo wanamuinua mwanadamu wa kawaida (kama Mariamu) kwenye nafasi ya Uungu, nguvu zao zimeelekezwa kuwaonyesha kwamba haiwezekani mwanadamu kuwa Mungu! Wakristo pia wanaamini haiwezekani kwa mwanadamu kuwa Mungu. Hata hivyo, Wakristo wanaamini kuwa Mungu alikuwa mwanadamu. . . . Uislamu wanashindwa kuona kwamba Ukristo haumwinui mtu na kumlinganisha na Mungu, lakini wamwabudu Mungu aliyekuwa mwanadamu." (Sundiata 2006: 199)[13] Kwa hiyo Wakristo wanakataa *hitimisho* la Kiislamu kwamba Kristo alikuwa mwanadamu *wa kawaida* tu "hakuwa na sehemu kwenye Uungu."

Kukataliwa huku kwa Uungu wa Kristo kunaleta mgawanyiko wa msingi baina ya Ukristo na Uislamu jambo linalofikia kujiuliza moyoni kwamba Yesu ni nani: kwamba alikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili (mtazamo wa Wakristo) au alikuwa mwanadamu wa kawaida (mtazamo wa Uislamu). Jambo hili ni la muhimu kwa Ukristo kwa sababu Uungu wa Kristo (kama ulivyo ubinadamu wake) ni muhimu kwa uweza wa Kristo kukamilisha utume wa msingi kulingana na Ukristo, hii ni kusema kwamba, Upatanisho wake kwa dhambi za wanadamu. Ni kiini pia kwa Uislamu kwa sababu Uislamu (Kwa makosa) wanafikiri kwamba mtazamo wa Wakristo na mtazamo wa Uislamu kwa dhambi zisizosameheka, hii ni kusema kwamba, iliyo kuu *ya kuepukwa*, i.e., Kuabudu au kutangaza Uungu kwa chochote au kwa yeyote yule Zaidi ya Allah. Hili huleta mgawanyiko wakati wote baina ya Ukristo na Uislamu ambao hautapatiwa ufumbuzi kwa kuwa wote wawili wana misimamo tofauti juu wazo la ninini maana ya Mungu "mmoja".

Vivyo hivyo, ingawaje Uislamu unaukataa uungu wa Kristo, kuna sehemu za Korani zinazofundisha na kuonyesha kwamba wazo la Wakristo juu ya uzazi wa Kristo angalau linakubali:

- Kwanza, kwenye Korani, roho au malaika wanaweza kuchukua umbo la mwanadamu: *"Tulimtuma kwake [Mariamu] malaika wetu [malaika Gabrieli)],na alitokea mbele yake akiwa na umbo au mwonekano wa mwanadamu katika kila hali"* (**Q. 19:17**, Hilali-Khan). Kwa kuwa roho au malaika wanaweza kuwa na umbo la binadamu, Mungu yeye, anaweza kufanya kila kitu, kwa hakika pia anaweza kuchukua umbo la binadamu.
- Pili, **Q. 39:4** inasema, *"Allah angetaka kumchukua mwanae, Angemchagua yule aliyempendeza miongoni mwa hao aliowaumba."* Hili linathibitisha kwamba Allah angekuwa na mwana kama angechagua hivyo. Hili linatupelekea kufikiri kwamba alikuwa na mwana au la na kama ndivyo, ninini asili ya mwanae.
- Tatu, Uzazi wa Yesu na Korani yenyewe vinafanana sana: "Kama neno la umilele 'logos' [Neno] liliuvaa mwili kwa utu wa Mungu mwanadamu, hivyo neno la milele la Mungu (Korani) 'lilishuka' [angalia **Q. 2:97; 17:105; 24:34; 26:192-93**] kwa Mohamedi kwa umbo la kitabu" (Larson 2008: 12n.35).
- Nne, **Q. 20:9-14; 27:7-9** inaelezea simulizi ya Musa na Moto, *"Lakini alipoukaribia moto, sauti ilisikika: 'Ee Musa! . . . Hakika, Mimi ni Allah'"* (**Q. 20:11, 14**). Ali anatoa maoni yake kwamba "haukuwa moto wa kawaida. Ni kichaka kilikuwa kikiungua; alama ya Utukufu wa Allah." (Ali 2006: Q. 20:10n.2541) Daniel Shayesteh analitazama, "Mungu mwenye nguvu alikuwa moto (Kitu) na haikuonekana kuwa ni

[13] Kulingana na Biblia, Yesu ni *wa Milele.* McDowell na Larson wanasema kuwa, "Hakuna Andiko lolote linalosema kwamba Mungu'alimwuumba Yesu" (McDowell na Larson 1983: 93). Hakika, Kristo *"ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu"* (**Wafil 2:6-7**; angalia pia **2 Wakor 8:9**). Kwa maneno mengine, ingawa alikuwa Mungu, Kwa hiari yake Yesu aliacha mbingu, akawa mwanadamu, na akajinyenyekesha kwa Baba—yote hayo kwa ajili yetu. Hivyo, popote unapoona Yesu anajinyenyekesha kwa Baba na kutumia maneno kama haya *"Baba ni mkuu kuliko Mimi"* (**Yohana 14:28**), ni lazima tukumbuke yale aliyoyafanya kwa kujivua mwenyewe na kuyaacha manono ya mbinguni kwa ajili yetu. kama A. W. Pink anavyotukumbusha, "Tofauti anayoionyesha Mwokozi kati yake mwenyewe na Baba [Kwenye **Yohana 14:28**] haihusiki na asili, lakini ni tabia rasmi na nafasi. Kristo hakujizungumzia mwenyewe kwenye umuhimu wake. Aliyefundisha kwamba tusinyang'anye 'kuwa sawa na Mungu' alichukua hali ya utumwa, na siyo hivyo tu, alifanya kwa mfano wa mwanadamu. Kwa mitazamo hii, ni kusema kwamba, Kwa ile hali yake (kama Mpatanishi) na ile hali ya kudhaniwa kuwa mwanadamu wa asili, Alikuwa mdogo kwa Baba. . . . Kwa mtazamo wa hili, Kristo aliitofautisha hali yake ya sasa na ile ya Baba mbinguni patakatifu. . . . Kristo aliishikilia nafasi yake kama mtumwa, na kumtukuza yeye aliyempeleka." (Pink n.d.: 2:408) Uthibitisho wa Uungu wa Kristo tutauzungumzia Zaidi kwe fungu la **VI. Majibu kwa ya mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Yesu ni "Mwana wa Mungu,"** hapo chini.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kufuru kwenye Korani. . . . Kitu ambacho Mungu amechagua kujidhihirisha kwacho chaweza kuleta tofauti kwenye Korani? Kama hakiwezi, kwanini basi wanawalaumu Wakristo kudai kuwa Mungu alikuwa mwanadamu?" (Shayesteh 2004: 140)

Kwa kuwa *kimsingi* Korani inakubaliana na wazo la uzazi kwenye mazingira mengine, kikwazo cha msingi cha Uislamu kukubaliana na uzazi wa Kristo kimeondoka. Kama Sundiata alivyosema, "Ni mpaka pale itakapoonyeshwa kwamba Mungu *hawezi* kuwa mwanadamu na kwamba Wakristo kudai kuwa Yesu alikuwa Mungu katikati yetu hakutaaminika tena" (Sundiata 2006: 218).Kulijua hili kutasaidia kuvunja kizuizi kinachowatenganisha Uislamu na Injili.

## III. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Utangulizi

Kusulubiwa na kufufuka kwa Yesu Kristo kunaugusa moyo wa Ukristo. Umuhimu wa kiini chake umesisitizwa kwa kurudiwa mara nyingi kwenye Agano Jipya (e.g., **Math 20:28; Yohana 10:17-18; Warumi 5:8-11; 1 Wakor 15:1-4; Wagal 3:13; Waef 2:14-16; Wafil 2:5-11; Wako l 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; Waeb 2:14-15; 1 Pet 3:18; 1 Yohana 4:10; Ufu 5:1-6**). Kusulubiwa na kufufuka kimwili kwa Yesu kulitabiriwa (**Math 16:21; 17:22-23; Marko 8:31-32; 9:31; 10:32-34; Luka 9:22; 18:31-33; Yohana 2:18-22**). Yesu alidai kuwa yeye ni Mungu aliyekuja duniani kama mwanadamu. Maadui wa Yesu walitaka ishara, na akawaambia atawapa moja —kufufuka kwake. Yesu aliwaambia kuwa angethibitisha kile anachokisema juu yake kwa kufanya jambo (kufufuka kimwili kutoka kwa wafu) jambo ambalo kwa mwanadamu wa kawaida haliwezekani (hata nabii au mjumbe). Ni jaribio ambalo kwalo twatambua kuwa alikuwa akiwaambia ukweli (**Math 12:38-40; 16:1-4; Yohana 2:18-21;** angalia pia **Marko 14:58; Luka 11:29-30; Warumi 1:4**).[14] Jaribio hili la kweli ni la kipekee kwenye Historia ya Ukristo. "Kama Yesu *asingefufuka* kutoka kwa wafu, angekuwa nabii wa uongo na bandia ambaye hakuna mtu mwenye akili timamu ambaye angemfuata. Kwa maneno mengine, kama *alifufuka* kutoka kwa wafu, tukio hili linathibitisha umuhimu wa madai yake." (Habermas na Licona 2004: 27)

Kwenye Biblia, kufufuliwa kwa mwili wa Kristo ni suala la karibu sana linaloshabihiana na kusulubiwa kwake (angalia, e.g., **Math 17:22-23; Marko 10:32-34; Yohana 2:18-22; Warumi 4:24-25; 5:8-11; 1 Wakor 15:1-4; Wafil 2:5-11; Waeb 10:9-13**). Kwa kuwa kusudi la Kristo kuja ulimwenguni ilikuwa ni kuja kuzichukua dhambi na hukumu ya mwanadamu kwa kujitoa sadaka mwenyewe msalabani, kufufuka kwake (na baadaye kupaa): (1) kunadhihirisha kwamba Mungu aliikubali sadaka ya Kristo; na (2) kuthibitisha kwamba Kristo alikuwa nani na kile Kristo alichokisema

Suala la kusulubiwa na kufufuka kwa Kristo ni la kihistoria: kwamba alisulubiwa na baadaye kufufuliwa mwili wake kutoka kaburini au haikufanyika hivyo. Kwenye jambo hili muhimu hakuna uthibitisho wa Biblia kwamba tukio hili lililotokea ni la kweli au Korani kukataa kwamba halikutokea ni sahihi. Vyote haviwezi kuwa sahihi. Kwa sababu hili ni tukio la kihistoria, "Kwamba lilitokea au hilo tukio halikutokea miaka elfu mbili iliyopita halithibitishwi kwa Imani lakini kwa utafiti wa kihistoria, kwa kiasi kwamba kweli zaweza kufikiwa kwa kuuliza maswali ya namna hii" (Pannenberg 1968: 98).

Kwa sababu jambo hili linakwenda kwenye moyo na kujiuliza Yesu ni nani, na kwa sababu mambo ni mengi (kama Yesu ni kile alichosema yeye, hivyo kuungana naye ni suala la uzima wa milele au kifo), Watu wote—Wakristo, Uislamu, Wasioamini kwa kila aina—wanahitajika kufanya uchunguzi wa uthibitisho na kuamua wenyewe kwamba ni kipi cha kweli kati ya Biblia na Korani. Korani yenyewe inaonekana kusisitiza hili. Kwenye **Q. 2:111** Mohamedi aliambiwa awaambie hasa Wakristo na Wayahudi, *"Thibitisheni kama ninyi ni wakweli."* Kwenye matukio mengine ya Korani watu kutumia akili na kutafakari uthibitisho (**Q. 6:151; 7:169; 8:22; 10:16; 16:12, 67; 21:10; 23:80; 26:28; 30:28; 36:62**). Hivyo na tuugeukie ushahidi.

---

[14] **Q. 46:35** inazungumza kuhusu *"wajumbe wa kusudi lisilobadilika"*(au, kama Hilali-Khan alivyolitafsiri, *"mapenzi ya ngvu"*). Kwa manabii na wajumbe wote, ni watano tu waliotambuliwa kama "wajumbe wa mapenzi ya nguvu": Nuhu, Ibrahimu, Musa, Yesu, na Mohamedi (Hilali na Khan 1998: 686 n.2; Haleem 2005: Q. 46:35n.a). Mtetezi wa Waislamu Dr. Abdullah Hadi Al-Kahtani anasema, "Waislamu wanaamini kwamba nabii wa Mungu hawezi kusema uongo, kwakuwa manabii wote wa Mungu hawakosei" (Al-Kahtani 1996: 16). Waislamu hawataki kuuona ukweli huu kwamba—Kwakuwa Yesu alikuwa "mjumbe wa kusudi lisilobadilika" aliyetabiriwa kufa na kufufuka kwake na kusemekana kwamba kifo chake kitakuwa ishara—kwa kudai kwamba hakuuawa wala kufufuka, kimsingi wanasema kwamba Yesu alikuwa Mwongo. Zaidi ya hayo, kwa kutokumwamini Yesu wanakataa kutii maamrisho ya Korani **Q. 4:150-52** yanayosema, *"Wale wanaomkataa Allah na wajumbe wake, na wale (wanaotaka) kumtenganisha Allah na wajumbe wake, wakisema: 'Tunawaamini baadhi yao lakini wengine tunawakataa':Na (wanaotaka)wanaotaka kujitafutia njia yao,-Hakika (wanafanana)na wasioamini; na tumeandaa hukumu kali ya wasioamini. Kwa wale wanaomuamini Allah na wajumbe wake na kutokuweka tofauti kati wajumbe, tutawapa kwa haraka thawabu zao (kwa wakati): kwa kuwa Allah ni mwenye kusamehe, Mwingi wa huruma."* Kulingana na **Q. 4:150-52**, kukataa kile Yesu alichokisema inamkufanya mtu kuwa sawa na asiyeamini atakayepata *"adhabu ya aibu."* Vivyo hivyo, kwakuwa Yesu alizungumzia hasa na hata kutabiri kusulubiwa na kufufuka kwake, ni muhimu kuangalia ushahidi.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

## IV. <u>Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Kusulubiwa</u>

Mashahidi wengi wanathibitisha kwamba Yesu alifanya, ni kweli, alikufa msalabani. Ushahidi huo ni pamoja na huu ufuatao:

### A. *Mashahidi wengi*

Kusulubiwa kwa Yesu halikuwa tukio la siri au la kificho. Badala yake, lilikuwa tukio la wazi lililohusisha maafisa wa serikali ya Kirumi, Viongozi wa Wayahudi (Baraza la Wazee), na watu wa kawaida, marafiki na maadui wa Yesu. Ryan Turner anafupisha, "Ingawa wanafunzi walimsahau Yesu, wengi wao walikuwa wakishuhudia kwa mbali (Marko 14:54). Pia, alikuwepo mwanafunzi ambaye hakutajwa jina [pengine ni Yohana] ambaye Yesu, akingali msalabani, alimwamuru kumtunza Mariamu (Yohana 19:26-27). Injili ya Luka inatueleza kwamba wakati Yesu alipokuwa ameubeba msalaba, '. . . Walimfuata watu wengi, na wanawake, waliokuwa wakimlilia na kumuombolezea' [Luka 23:27]. Kwa nyongeza ya hayo watu tayari wanaserma kwamba Injili imeonyesha kumbukumbu nyingi kuhusiana na Viongozi wa Wayahudi (Mt. 27:41; Mk. 15:31), Akida wa Kirumi (Mt. 27:54; Mk. 15:39; Lk. 23:47) na maaskari (Mt. 27:35; Mk. 15:24; Lk. 23:35; na Yohana 19:18, 23) Wote hawa walishuhudia kusulubiwa kwa Yesu. Kwa Waislamu kubisha kwamba kusulubiwa siyo jambo la Kihistoria kifupi hailingani na takwimu za historia kwa sababu kulikuwa na kundi kubwa la mashahidi kusuhudia kwamba Warumi walimsulubisha Yesu." (Turner 2014: chanzo ni mashahidi)

Kwa nyongeza, wakati Yesu anapelekwa nje ya mji kusulubiwa, *"Walimshurutisha mtu aliyekuwa akipita njiani, Simon Mkirene (Baba yake na Isikanda na Rufo), Kuubeba msalaba wa Yesu"* (**Marko 15:21**). Timothy Keller anatuonyesha, "Haikuwepo sababu ya mwandishi kuyaandika majina haya vinginevyo msomaji anajua au anaweza kuwasiliana nao. Marko anasema, 'Isikanda na Rufo wanathibitisha ukweli wa kile ninachokieleza, kama ungetaka kuwauliza.'" (Keller 2008: 101) **Luka 23:49** anaongeza kwamba *"marafiki wa Yesu na wanawake waliofuatana naye toka Galilaya walisimama mbali, wakilishuhudia tukio hilo,"* Na Mama yake na Yesu mwenyewe, Dada yake na Mama yake na Yesu, na wanawake wengine aliowafahamu walikuwa mashuhuda wa tukio la kusulubiwa (**Yohana 19:25-27**). Mama alimjua mwanae. Mariamu, wanafunzi wa Yesu (pamoja na Yohana, ambaye kwa hakika alisema, *"Naye aliyeona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli; naye anajua ya kuwa anasema kweli ili ninyi nanyi mpate kusadiki,"* **Yohana 19:35**). Ndugu zake na Yesu, marafiki zake, na wale waliofuatana naye walimjua Yesu ni nani na hivyo walijua aliyesulubiwa ni Yesu, siyo mtu mwingine. Kudai kwamba mtu mwingine alikuwa msalabani, au kwamba Yesu hakufa msalabani, ni kutokukubaliana na ukweli.[15]

---

[15] Wazo la Emerick kwamba Warumi walimkamata mtu ambaye hakustahili, "wakifikiria kwamba Wasimiti wote wanafanana" ni upumbavu (Emerick 2004: 224). Ni upumbavu kwa sababu Wasimiti wote hawafanani *na Wasimiti wengine*, Kwenye jambo hili lilimhusisha Mama yake na Yesu, wanafunzi wake, marafiki zake, waliomfuata, na maadui zake (Waliotaka kuhakikisha kwamba ni Yesu aliyeuawa, siyo mmoja "anayemfanania"). Wazo kwamba mtu mwingine alikuwa mbadala pia ni upumbavu kwa sababu, kama Mawdudi anakiri kuwa, "Kwa kuwa kulikuwa na kesi kwenye mahakama ya Pilato, Upo uwezekano kwamba aliyehukumiwa ni Yesu. Pilato alimhukumu kifo." (A'la Mawdudi n.d.: Q. 4:157n.193) Yesu alikuwa katikati ya askari wa Kirumi alipohukumiwa na alipokabidhiwa kwao ili kupelekwa kuuawa; na aliendelea kuwa mikononi mwao hadi aliposulubiwa na kufa (kama alivyoendelea kuwa mbele ya wengine tangu wakati wa kesi na hadi kuhukumiwa kusulubiwa). Hapakuwa na "kukosea" ambako kungempelekea mtu mwingine asiye na hatia kuchukulia kuwa mbadala wa Yesu.

Uislamu kwa ujumla hawafikirii kweli nyingine za wazo kwamba Allah alimtoa mwingine mbadala wa Yesu pale msalabani: (1) Allah kwa njia hiyo angamfanya asiye na hatia kuwa mhanga wa tukio; (2) Allah kwa njia hiyo angewadanganya siyo tu maadui wa Yesu lakini pia angemdanganya Mama yake na Yesu, ndugu zake, marafiki, na wanafunzi; (3) Allah kwa njia hiyo angeonyesha kwamba kiasili hapaswi kuaminiwa kwa sababu uongo huo haukuwa wa lazima kabisa. Muislamu wa awali Daniel Shayesteh anauliza swali la wazi, "Kulikuwa na kusudi gani la kumfanya Yesu kuonekana kana kwamba amekufa na kipekee kumchukua Yesu kwenda mbinguni? Isingekuwa bora kwa Mungu kutokuwadanganya watu badala yake angewaua maadui mbele yao na kumchukuwa Yesu kumpeleka mbinguni mbele ya macho ya watu?" (Shayesteh 2004: 183) zaidi, kama Abbas Sundiata alivyoonyesha, "Kama Allah angewadanganya watu kufikiri kuwa tukio walilolishuhudia lilikuwa ni mazingaombwe, ni jinsi gani basi Uislamu wangeeleza kuwa Uislamu [wenyewe] ni waongo na wakatili wakubwa? . . . Siyo jambo la wazi basi kwamba njia pekee ambayo Korani inaweza kuukana ukweli wa Kihistoria kwamba Yesu alisulubiwa ni kumfanya Allah kuwa mdanganyifu kwa wanadamu?" (Sundiata 2006:248, 249) Mwanazuoni wa Kiislamu Mahmoud Ayoub alitambua tatizo. Alieleza, "Ni lazima ichukuliwe na waenezaji wa Hadithi na watoa maoni kwamba, Mungu alimchukua asiye na hatia kufa kwa ajili ya kumwokoa mwenye hatia na litakuwa ni kosa la Kiungu (*zulm*), ambalo halitabiriki kwa Mungu. Hivyo nadharia ambayo imejipatia umaarufu ni kwamba mmoja wa wanafunzi alijitolea kukubali kufa kama fidia kwa Bwana wake." (Ayoub 1980: 97) Nadharia ya mbadala wa hiari kwa mtu kujitolea kwa ajili ya Yesu, hata hivyo, haiondoi ukweli kwamba Allah alifanya uongo ili kuyaokoa maisha ya nabii wake.

Inasemekana kuwa uongo huo uliotendwa na Allah ni madai dhaifu yaliyofanyika miaka 600 baada ya ushahidi

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Kitabu cha Matendo ya Mitume, Waraka kwa Warumi, 1 na 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, 1 Wathesalonike, 1 na 2 Timotheo, Waebrania, 1 Petro, 2 Petro (siyo kwa uwazi), 1Waraka wa Yohana, na Ufu wa Yohana wote wameandika juu ya kifo cha Yesu; kwa jinsi ambavyo tukio hili la kifo lilivyoelezewa, wanaeleza ni kwa njia ya kusulubiwa. Vitabu hivyo vyote vimeandikwa na angalau waandishi saba tofauti na wote waliandika ndani ya miaka 20 na kiwango cha juu sana miaka 65 baada ya kifo cha Yesu.[16] Hili linamaanisha kwamba tukio la kusulubiwa liliandikwa wakati ambao mashahidi wengi walikuwa bado wako hai. Keller anaonyesha, "Agano jipya lisingesema kwamba Yesu alisulubiwa wakati maelfu ya watu mashahidi bado walikuwa hai waliojua kwamba alikuwa ni Yeye au la" (Keller 2008: 102).

Kwamba ni tofauti kabisa na Korani ambayo, kuhusiana na kusulubiwa, ina mstari mmoja tu ambao uliandikwa Zaidi ya miaka 600 baada ya tukio. Vivyo hivyo, Kwa kusudi la ushahidi wa Kihistoria, uchambuzi, na kuaminika, *Kwa mujibu wa maisha, kufa, na kufufuka kwa Yesu,* Biblia ipo kwenye kundi tofauti kabisa na Korani. Kama Eddy na Boyd wanavyoeleza, kwa vigezo vya uthamani wa historia "Korani ni ya karne ya saba , mbali na kwa kuchelewa sana kuchukuliwa kama chanzo huru cha kuaminika kwa habari zinazomhusu Yesu" (Eddy na Boyd 2007: 172).

**B.** ***Mwanzo wa imani ya Kikristo***

Kama ilivyo hapo juu, vitabu vya Biblia viliandikwa mapema, mwanzoni chini ya miaka 20 baada ya kifo cha Yesu. Hata hivyo, waandishi wa Agano Jipya waliungana kwenye uandishi wao mapema kuandika Imani ya Kikristo *ambayo ni ya zamani kuliko vitabu ambavyo imeandikwa ndani yake* (angalia Habermas 1984: 119; Cullmann 1949: 10, 22-23). "Desturi hizi za zamani zilionekana mara nyingi kwenye Agano Jipya na kwa kweli limebeba mafundisho ya kukariri na kutangaza ambayo yalirudiwa kwa maneno ya kinywa mpaka hapo yalipohifadhiwa kwenye vitabu vyenyewe. Kwa hiyo Imani hii kwakweli ilitangulia kuandikwa kwa Agano Jipya ambako kulitokea baadaye. . . . Mambo mawili ya msingi kwenye Imani hii ni kuhusu kufa na kufufuka kwa Yesu na uthibitisho wa Uungu wake." (Habermas 1984: 33, 120) Imani hii ni pamoja na **1 Wakor 15:3-7**

---

usio na chembe ya mashaka. Hauwezi kuelezea au kupinga ushahidi huu mkubwa wa Kihistoria wa ukweli juu ya kusulubiwa kwa Yesu (angalia mada kuu ya sehemu hii) au kuelezea au kupinga ushahidi huu wa Kihistoria wa kufufuka kwa Yesu (angalia mada kuu ya sehemu ya **2.V. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Kufufuka**). Hakika, kwa sababu ushahidi wa Kihistoria wa kufufuka kwake ni mkuu sana, wazo kwamba "mtu mwingine alikuwa mbadala kwa Yesu" inahitaji kuhitimishwa kwamba *"Yesu aliyefananishwa"* alifufuliwa toka kaburini! Kwa maneno mengine, Uongo wa Allah unaleta matokeo yale yale—mtu mwingine alisulubiwa na hatimaye kufufuliwa—isipokuwa kwamba mtu aliyehusika ni (udanganyifu) upumbavu wa Allah, siyo Yesu halisi. Zaidi ya hayo, *baada ya kufufuka kwake* muigizaji isingewezekana kuendelea kucheza kwa kuwashawishi watu wote kwamba alikuwa Yesu "halisi" kwa kuwajua wanafunzi wake kwa majina (**Yohana 20:11-21:24**), inaelezea ni jinsi gani WAgano la kale lote linavyomzungumzia Yesu halisi (**Luka 24:13-49**), anawatuma wanafunzi wake kwenda ulimwenguni mwote kuieneza Injili ya Yesu wa kweli (**Math 28:18-20; Marko 16:15-18**), na kisha akapaa mbinguni (**Marko 16:19; Luka 24:50-53; Matendo 1:9-11**)! Kwa hiyo"nadharia ya Mbadala" haina maana yeyote na siyo sahihi hata kidogo.

[16] John A. T. Robinson ametolea maelezo ya msingi kwamba Agano Jipya lote lilikamilika kabla ya kuangamizwa kwa Hekalu mwaka AD 70, jambo linalomaanisha kwamba Agano Jipya lilikamilika miaka 40 tu au pungufu ya hapo baada ya kifo cha Yesu. Angalia John A. T. Robinson, *Redating the New Testament* (Philadelphia: Westminster: 1976). Richard Bauckham, Kwenye utafiti makini, unahitimisha kwamba, kinyume cha madhanio ya karne ya kumi na tisa na mapema karne ya ishirini wasomi huru na wakosoaji kwamba Biblia iliandikwa miaka mia moja au Zaidi baada ya matukiokwa tamaduni za mazungumzo ya wale ambao hawakutajwa, Injli ina tabia ya ushuhuda na "imebeba ushuhuda wa mashahidi walioshuhudia kwa macho yao wenyewe tukio lote, siyo kwa kutokuwa na uhariri na utafsiri, lakini kwa njia ambayo ni uaminifu mkubwa wa jinsi ambavyo mashuhuda wenyewe wlivyoelezea, kwakuwa Wainjilisti walikuwa wakiwasiliana moja kwa moja na mashuhuda wa tukio, hayakuchukuliwa kutoka kwao kwa mchakato mrefu wa kuhamisha yasiyojulikana au kwa kitamaduni" (Bauckham 2006: 6; angalia pia Lewis 1967b: 155 [p.36 online], maelezo ya Injili ni "taarifa," siyo "ushairi, riwaya, fasihi za ndoto, hadithi, [au] simulizi"). Hata majina ya watu waliotajwa kwenye Injili yanathibitisha hilo. Mfuatano na matumizi ya majina halisi "yanafanana vema na kuhusiana moja kwa moja na kumbukumbu kamilifu za mfano wa majina tofauti elfu tatu ya vyanzo vya Wayahudi Wapalestina wa wakati ule. Ni kwa nadra sana mfanano huu kuwa umetokana na kuongezwa kwa majina ya kitamaduni, hata miongoni mwa Ukristo wa Kiyahudi wa Wapalestina, na hakuna uwezekano wa kuwa na matoteo ya kuongezewa majina kutoka nje ya Wayahudi wa Palestina, kwa kuwa sehemu ya matumizi ya majina ya Ughaibuni [i.e.,kutawanyika kwa Wayahudi baada ya mwaka AD 70] yalikuwa tofauti sana." (Bauckham 2006: 84) Kwa maana nyingine, "Haisadikiki kabisa kwamba simulizi ya Injili asili yake ni Wakristo wa baadaye waliotokana na jamii ya nje ya Palestina [i.e., baada ya mwaka AD 70]" (Keller 2008: 265n.8). Ukweli huu haukubaliani na tangazo la Mohamedi Asad kwamba simulizi ya kusulubiwa kwa Yesu ni hadithi ambayo kwa sehemu iliibuka miaka mingi baada ya wakati wa Yesu (Asad 1980: Q. 4:157n.171). Nadharia ya"hadithi" imejadiliwa kwa kina, hasa hasa kwenye mazingira ya kufufuka kwa Kristo, kwenye kipengele **V.H. *Kushindwa kwa maelezo mengine***.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

na **Wafil 2:6-11** (Cullmann 1949: 22-23). Kanuni za Imani zote zinalenga kifo cha Kristo. **1 Wakor 15:3-4** inatutaarifu kwamba *"Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko, na yakuwa alizikwa"* Imani iliyoandikwa kwa Wafilipi inafafanua jinsi alivyokufa: *"naam mauti ya msalaba"* (**Wafil 2:8**).

Gary Habermas anatuonyesha, "Kwamba ukiri huu [**1 Wakor 15:3-7**] ni wa Wakristo wa kwanza, Kabla ya Paulo ilitambulikana kwa umuhimu wote na wanatheolojia makini ulimwenguni kote. Vipo viashiria vingi vinavyofunua uamuzi huo. Kwanza maneno ya Paulo 'umefika' na 'umepokelewa' masharti ya kiufundi ya kupitia kwenye desturi. Kama vile, tunao ujumbe wa Paulo kwamba nyenzo hii haikuwa yake mwenyewe, lakini ilipokelewa kutoka kwenye chanzo kingine. Pili, idadi ya maneno kwenye Imani hii siyo ya Paulo, anaonyesha tena chanzo chake cha asili. . . . Tatu, inapendeza kwamba Imani imeundwa kiasili, kwa mfuatano, kwa njia hiyo kutupatia viashiria Zaidi vya kutamka na ukiri wa asili wa chanzo hiki. Nne, vipo viashiria kwamba yaweza kuwa ya asili ya Kisimiti, kama vile matumizi ya Kiaramaiki ya neno 'Cephas' badala ya Petro (mst. 5), baadaye, kutuonyesha chanzo cha awali kabla ya tafsiri ya Kigiriki ya Paulo." (Habermas 1984: 124-25, nukuu imeondolewa; angalia pia Jeremias 1966: 101-03) Habermas anaendelea kusema, "Kulingana na wasomi wengi, Paulo alipokea Imani hii toka kwa mitume, kinachoifanya kuwa ya mbele zaidi, na Imani yapaswa kurudiwa kabla ya kufanyiwa marekebisho. Hivyo kwa sasa tupo kwenye kilele cha Kusulubiwa, na kumbuka, ni mashahidi walioona ndio walioeneza habari hizi; siyo za shuhuda za kusikia tu." (Habermas 1987: 43; angalia pia Habermas 1984: 125 na nukuu zilizopo; Wright 2003: 319)

**C.** ***Ushahidi wa kitabibu wa kifo***

Makala iliyoandikwa kwa kina kwenye gazeti la *Journal of the American Medical Association* ilichunguza kwa kina kwa mtazamo wa Kitabibu tukio zima lililopelekea kusulubiwa kwa Yesu (i.e., jasho lake na matone makuu ya damu kwenye bustani ya Gethsemane, kupigwa kwake na Wayahudi na pia kuteswa na Warumi, kushindwa kwake kuubeba msalaba wake), asili ya kusulubiwa kwenyewe, na kuchomwa kwake mkuki na askari wa Kirumi damu na maji vikatoka ndani yake, kama ilivyoandikwa kwenye maandiko tofauti kwenye Biblia. Mwandishi anahitimisha, "Kilichosababisha kifo cha Yesu, kama wahanga wengine wa kusulubiwa, yawezekana ni kutokana na maumivu ambayo yalipelekea uchovu mshtuko na kukosa hewa na pengine kushindwa kwa moyo kwa papo hapo. . . . Hata hivyo jambo la msingi siyo kwamba *ni jinsi gani* alivyokufa lakini ni *kama* alikufa. Ni wazi kwamba, uzito wa kihistoria na uthibitisho wa kitabibu vinaonyesha kwamba Yesu alikufa kabla ya kujeruhiwa ubavuni na kusaidia mtazamo wa kidesturi kwamba mkuki ulipenya kwenyeti ya mbavu zake za kulia, bila shaka ulitoboa siyo tu mapafu ya kulia lakini pia moyo na kwa njia hiyo kuthibitisha kifo chake. Vivyo hivyo, tafsiri inayojielekeza kwenye kudhaniwa kwamba Yesu hakufa msalabani imeonekana kupata nafasi kwenye ujuzi wa kitabibu wa sasa." (Edwards, et al. 1986: 1463)

Askari wa kirumi aliyemchoma mkuki ubavuni alihakikisha kwamba kwa hakika Yesu amekufa (**Yohana 19:31-34**). Ikiwa askari hakuwa na uhakika kwamba Yesu amekufa, pengine askari wangeweza kuuvunja mguu wa Yesu kama walivyofanya kwa wanaume wengine wawili waliosulubiwa pamoja na Yesu au wangefanya jambo jingine kuhakikisha kifo chake. Kama Yesu kweli hakufa, lakini askari wa Kirumi alitoa taarifa kwa Pilato kwamba alikuwa amekufa, angekuwa ameihalifu amri yake na angekuwa amemdanganya kamanda wake na kwa hiyo bila shaka angelipia kwa uhai wake. Kwa sababu hiyo, haikubaliki kuendelea kung'ang'ania kwamba Yesu hakufa msalabani.

**D.** ***Yesu kuzikwa kaburini***

Pontio Pilato, kiranja wa Rumi (gavana) wa Yudea, aliagiza Yesu asulubiwe (**Math 27:26; Marko 15:15; Luka 23:24-25; Yohana 19:16**). Baada ya kusulubiwa, Yusufu wa Arimataya, mjumbe wa baraza la wazee la Kiyahudi, aliomba kupewa mwili wa Yesu kwa ajili ya maziko; Pilato aliruhusu mwili ukazikwe lakini baada ya kuthibitishiwa na askari aliyekuwepo kwamba kwa hakika Yesu alikuwa amekufa (**Math 27:57-58; Marko 15:42-45; Luka 23:50-52; Yohana 19:38**).[17] Imani ya mitume awali, kabla ya Paulo na kurudi nyuma hadi kwenye umuhimu wa wakati wa kusulubiwa kwenyewe, ina maneno haya *"kwamba alizikwa"* (**1 Wakor 15:4**). N. T. Wright anaonyesha kwamba, "Kutajwa kwa kuzikwa kwa Yesu [**1 Wakor 15:4a**] yaweza kuufikia ukweli huu kwa kifupi na simulizi za kiasili kwa ufupisho kama yangechukuliwa kwa umuhimu wake wenyewe. [Itasaidia] kuthibitisha kwamba kweli na kwa uhakika Yesu alikufa." (Wright 2003: 321) Muhuri maalum wa serikali, na askari wa Kirumi waliondoa uwezekano wa mtu yeyote kuvunja au kuutoa mwili kaburini (Ibid.: 53-

[17] "Hata wasomi mahiri wanatambua kwamba Yusufu yawezekana ni halisi, mwanahistoria binafsi aliyemzika Yesu, Kwa kuwa haikuwa rahisi kwamba waumini wa mwanzo wa Kikristo kutengeneza kaburi binafsi, kumpa jina na mji ulioko karibu, na kuweka wahusika wa uongo kwenye baraza la historia la wazee, ambalo wajumbe wake ni watu wanaojulikana sana" (Craig 1981: 53).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

61).[18]

**E.** ***Mwitikio wa wanafunzi***

Mara baada ya tukio la kusulubiwa walitegemea kwamba Yesu *pekee* hakika angekufa kwa kusulibiwa. Kwa mfano, **Yohana 20:19** inatueleza kwamba wanafunzi walikuwa chumbani ambapo*"milango ilikuwa imefungwa kwa hofu ya Wayahudi."* Hili pekee lingeeleweka kama viongozi wao wangelielezea, kwa kweli, kwa kuuliwa kwa amri ya viongozi wa Wayahudi na wanafunzi walikuwa na hofu kwamba viongozi wa Wayahudi wangewafuatillia. Siku ya jumapili mara baada ya kusulubiwa, **Marko 16:10** anaongeza kwamba wanafunzi wa Yesu walikuwa *wakilia na kuomboleza."* **Luka 24** inatuarifu kwamba wanafunzi wengine wawili, mmoja akiitwa Kleopa, walikuwa wakitembea barabarani kuelekea Emmaus. **Luka 24:17** anasema kwamba walionekana*"wakiwa na huzuni."* Wanafunzi wawili wanaeleza sababu kwenye **Luka 24:20-21** walipokuwa wakisema *"jinsi kuhani mkuu na watawala walivyomtoa [Yesu]na kumhukumu kifo, na kumsulubisha. Lakini tuliamini kwamba ni yeye ambaye angewakomboa WaIsraeli"* Tena, huzuni na kutoweka kwa tumaini la hao wanafunzi linaleta mwanga wa *pekee* juu ya kusulubiwa kwa Yesu. Ukweli kwamba mmoja wa wanafunzi alikuwa njiani kwenda Emmaus ametajwa kwa jina ni ushahidi mwingine kwamba maelezo ni ya uhakika na ya kuaminika, Kwakuwa Kleopa angeweza kuulizwa juu ya tukio la siku hiyo.

**F.** ***Uvumi ya kwamba alijidhuru mwenyewe***

Kwa mazingira ya Kiyahudi Ukristo ulizaliwa karne ya kwanza, hata hivyo injili zote nne na waandishi wengine wa Agano Jipya wamesisitiza ukweli kwamba Yesu alisulubiwa na Warumi. Kama simulizi ya maisha yake ingetengenezwa muda mrefu baada ya ukweli na wafuasi wake, maelezo ya kusulubiwa kwa Yesu kamwe yasingekuwepo. "Ni vigumu kufikiria Zaidi njia sahihi ya kuwashawishi watu wa karne ya kwanza kwenye mazingira ya Kiyahudi kwamba ni mtu mwingine na *siyo* Masihi kuliko kuwaambia kwamba aliyetazamiwa kuwa mwokozi aliuawa na watesi wa jeshi la Israeli! Kwa kwenda mbali Zaidi na kuwaambia kwamba aliyetazamiwa kuwa mwokozi alikufa kifo cha laana kwenye mti ingeendelea kufanya mambo yote kuwa mabaya zaidi (cf. Kumb. 21:22-23). . . . Kwa hiyo, Ukweli kwamba desturi ya injili zote nne zimeendelea kuandika juu ya Kusulubiwa lakini pia kuifanya kuwa kiini cha ujumbe wao ni lazima kuchukulia kama ushahidi kwamba Wakristo wa kwanza, ikiwa ni pamoja na waandishi wa injili zote nne, wamekuwa tayari kulitambua, kukumbuka, na kwa ujasiri kulitangaza tukio moja la kweli na la kutisha la kihistoria likiambatana na mwanzo wa harakati zao mpya. Hii ni aina ya uvumi wa kujidhuru mwenyewe ambayo kwa asili wanahistoria hutafuta ili kuweza kuzihakiki kazi za zamani." (Eddy na Boyd 2007: 411)

**G.** ***Kuthibitishwa na maadui na vyanzo vingine visivyo vya Kikristo***

1. <u>Madhababu ya Talimudi ya Wababeli.</u> *Madhababu ya Talimudi ya Wababeli* ni ujumbe muhimu kwa Ualimu wa Kiyahudi. Jitihada za Baraza la Wazee, kifungu cha 43a kinasema, "Jioni kabla ya pasaka Yesu aliangikwa. Kwa siku arobaini kabla ya kuuawa kwake, mjumbe alimtangulia na kulia, 'Anaenda kupigwa kwa mawe kwa sababu anafanya uchawi na kuwadanganya Waisraeli waasi. Yeyote anayeweza kusema chochote cha kumsaidia, na aje mbele aweze kuomba kwa niaba yake.' Lakini kwakuwa hakuna kilicholetwa kwa ajili ya kumsadia aliangikwa jioni kabla ya pasaka!" (Bab. Talmud: Sanhedrin 43a) Andiko linathibitisha kwamba Yesu, likimaanisha Yesu Kristo kwa kuongeza "Mnazareti" baada ya jina lake (Bab. Talmud: Sanhedrin 43a, n.34). Mahali pa "kuangikwa" limenukuliwa kutoka **Kumb 21:22-23** na "kabla ya wakati wa Wakristo palikwisha kutumiwa kwa ajili ya wahanga wengine kusulubiwa" (Carroll na Green 1995: 172). Agano jipya linatumia neno "kuangika" kwa maana iyo hiyo (**Luka 39; Matendo 5:30; 10:39; Wagal 3:13**). Wasomi wengi wanasema kwamba njia hii ya *Talmud* ilikuwepo tokea kipindi cha kukusanya maandiko, AD 70-200 (Habermas 1984: 97-98). Hii inathibitisha kwamba *Babylonian Talmud* ni "kazi maalum" ya waalimu wa Kiyahudi ya kutekeleza wajibu wa kumtoa Yesu ili auawe na kwamba alikufa kwa hasira
2. <u>Toledot Yeshu.</u> *Toledot Yeshu* ni toleo la mashambulizi ya maisha ya Yesu, aliyekulia kwenye majibu ya jamii ya Kiyahudi kwa Ukristo" (*Toledot Yeshu* n.d.: Utangulizi). Ingawa haikuandikwa hadi karne ya tano au ya sita, *Toledot Yeshu* tena inathibitisha kifo cha Yesu "Yesu aliuawa mnamo saa sita kabla ya siku ya Pasaka na ya sabato" (Ibid.: text).
3. <u>Josephus.</u> Josephus alizaliwa mwaka AD 37. Alikuwa Kuhani wa Kiyahudi na baadaye kupigana na

[18] Josh McDowell anaonyesha, "Muhuri hiyo juu ya kaburi la Yesu ulikuwa ushuhuda wa jamii yote kwamba Mwili wa Yesu kwa hakika ulikuwa pale. Kwa nyongeza, Kwa sababu muhuri ulikuwa wa Kirumi, ilithibitisha ukweli kwamba Mwili wake ulikuwa ukilindwa na Wavandali na hakuna upungufu kwamba ni dola na mamlaka ya Rumi." (McDowell 1981: 59)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Warumi wakati wa vita vya mwaka AD 66-70.Baada ya Wayahudi kushindwa, alijiunga na Warumi kama mwanahistoria wa mahakama kwa mfalme Vespasian. Kwenye kitabu chake *Zamani za Wayahudi,* kilichoandikwa mwak AD 93, Josephus aliandika kile kilichoitwa *Ushuhuda wa Flavia*: "Wakati huo aliishi Yesu, mtu mwenye hekima, *Kama kweli mtu anataka kumwita mtu.* Ni mmoja aliyetenda mambo ya ajabu na alikuwa mwalimu wa wale watu walioukubali ukweli kwa furaha. Aliwashinda Wayahudi na Wagiriki wengi. *Alikuwa Masihi.* Wakati Pilato, alipomsikiliza akishtakiwa na watu wakuu waliosimama miongoni mwetu, alimhukumu kusulubiwa, wale ambao kwanza walimpenda hawakukata tamaa kwa mguso wake kwao. *Siku ya tatu aliwatokea akiwa amerudishiwa uhai, kwa kuwa manabii wa Mungu waliyatabiri hayo na mengi mengine yaliyomhusu yeye.* Na kabila la Wakristo, lililoitwa hivyo baada yake, hata sasa hawajatoweka." (Josephus 93:18.63-64, italiki imeongezwa) Watu wengi wanaamini kwamba hatimaye mhariri Mkristo aliongeza sehemu ya *italiki.* Wasomi wengi wanakubali kwamba Josephus kwa kiasi aliandika bila kuongeza sehemu ya italiki ya *Ushuhuda* (angalia Habermas na Licona 2004: 266-70n.42).

4. <u>Tacitus.</u> Tacitus, Aliyeishi kati ya mwaka AD 55-120, anajulikana kama "mwanahistoria mkuu" wa Rumi ya zamani (Habermas 1984: 87). *Historia yake,* iliandikwa yapata AD 115, inathibitisha kifo cha Yesu. Kwa kurejea moto mkubwa wa Rumi chini ya utawala wa Nero, Tacitus anasema, "Nero aliwafunga waliokutwa na makosa na kuwasababishia maumivu makali na mateso kwa wale aliowachukia, wale walioitwa Wakristo hadharani. Christus, kutoka kwenye jina lao la asili, walipata mateso makali wakati wa utawala wa Tiberius kwa mkono wa mmoja wa mpangaji wetu, Pontio Pilato." (Tacitus c.115: 15.44)

5. <u>Lucian wa Samosata.</u> Lucian wa Samosata alikuwa Mgirikia muigizaji mpinga Kristo. Kati ya mwaka AD 165-75 aliandika *Kufa kwa Peregrinus.* Ndani yake, alizungumzia Wakristo wanaomwabudu "Mtu aliyesulubiwa huko Palestina kwa sababu alianzisha kitu kisicho cha kawaida ulimwenguni" (Lucian wa Samosata c.165-75: 11).

6. <u>Mara Bar-Serapion.</u> Mara Bar-Serapion alikuwa mwanafalsafa mvumilivu kutoka Syria. Aliandika kati ya mwaka AD 73-200. Alimwandikia mwanae wa kiume kumshawishi kuwaiga waalimu wenye hekima wa nyakati zilizopita. Kwenye barua yake alisema, "Ni faida gali aliyopata Athenians kwa kumwua Socrates, angalia walipokea kama malipizi yake kwa njaa na maradhi? Au kwa watu wa Samos kwa kumchoma Pythagoras, angalia kwa saa moja nchi yao yote ilifunikwa kwa mchanga? Au kwa Wayahudi *kwa kumwua* Mfalme wao mwenye Hekima, angalia kwamba kwa kila wakati ufalme wao ulitwaliwa kwao na kupelekwa mbali *kutoka kwao?* Kwa haki aliyoifanya Mungu aliwalipa kwa hekima *wote* watatu wao. Kwa Athenians alikufa kwa njaa; na watu wa Samos walifunikwa na bahari pasipo kuokolewa; na kwa Wayahudi, walikuwa ukiwa na kufukuzwa kutoka kwenye ufalme wao, walitawanywa kwenye nchi zote." (Mara Bar-Serapion n.d.: n.p., fafanuzi ya asili)

Kwa kazi iliyoanzishwa ni kwamba hakuna hata mtu mmoja wa zamani aliyekuwa na mashaka kwamba Yesu alikufa kwa kusulubiwa; ilikua, kwa hakika, ilijulikana hivyo kwa watu wote. Madai ya Korani kwamba Yesu hakufa kwa kusulubiwa hayana msingi wowote wa Kihistoria wala kweli yoyote ni madai matupu yaliyotengenezwa na wanatheolojia na hakuna sababu ya Kihistoria.

## H. *Kushindwa kwa maelezo mengine*

Hakuna maelezo mengine yanayokubalika ambayo yalishakuwepo kuelezea kutokuwepo kusulubiwa. Kwa kifupi Korani kukataa kufa kwa Yesu au kwamba alisulubiwa hakuna kweli zozote za msingi za kihistoria zinazoweza kupelekea kushindwa kwa sababu hizo hapo juu. Hilo linahusika pia na wazo kwamba mtu mwingine alikuwa *mbadala* kwa Yesu au kwamba hakufa msalabani lakini alihuishwa kaburini.

1. <u>Nadharia ya "mbadala".</u> Kwa nyongeza ya sababu hizo hapo juu (angalia namba 32, hapo juu), nadharia ya mbadala inashindwa kwa sababu nyingine, kama vile baadhi ya Waislamu mashuhuri wanavyokiri. Kwa mfano, Muislamu Professor Mahmoud Ayoub anahitimisha kwamba nadharia ya mbadala inakubalika kwa sababu za lugha na kwa sababu ya haki na unyofu wa Mungu. Kwanza aliuliza, "Itakuwa kwenye kurudiarudia kwa agano la Mungu, haki na huruma zake, kuwadanganya wanadamu kwa karne zote hizi?" (Ayoub 1980: 104) Kwa Allah kuendelea kutumia uongo huu "itapelekea kushakiwa kwa shuhuda za kihistoria, hata zile taarifa za kihistoria zinazoendelea kuenezwa (*tawātur*). Kuendelea kuenezwa kwa taarifa za kihistoria kunatupa uhakika wa chanzo cha ufahamu, ambazo kwamba tawātur ina msingi imara wa kumbukumbu. Kama hata hivyo tukiruhusu uwezekano wa matukio ya kukanganya utambulisho, hatimaye itatulazimisha kushakia sheria zote takatifu." (Ibid.: 101) Hatimaye, "itaifanya historia ya Ukristo kuwa na msingi wa uongo wa kimbingu ambao haukudhihirishwa hadi Korani ilipofunuliwa baada ya karne nyingi" (Ibid.: 97).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

2. <u>"Nadharia ya Kuzimia".</u> Pengine maelezo mengine muhimu kuhusiana na kusulubiwa ambayo angalau yanajaribu kuzungumzia hizo kweli ni yale yanayojulikana kama "nadharia ya kuzimia," inayosema kwamba Yesu hakufia msalabani lakini alishushwa chini akiwa hajitambui (i.e., alizimia") na akahuishwa akiwa kaburini.

Nadharia ya kuzimia ni kinyume na shuhuda zinazofanana za mashahidi wa kwanza—labda marafiki au maadui wa Ukristo (Moule na Cupitt 1972: 508; Maier 1973: 112). Nyongeza, nadharia ya kuzimia inaenda kinyume na ushahidi wa kimwili. Kwanza, "Kusulubiwa ni kifo ambacho kimsingi ni cha kukosa pumzi, kama misuli ya kawaida inayozunguka mapafu ili kuwa na kupumua kwa kawaida wakati mwili umening'inizwa upande chini. Kwa hiyo, kifo cha kulazimishwa msalabani hakimruhusu mtu kupumua; mtu hawezi kuuingilia mfumo na uwezo wa kupumua akaendelea kuishi kwa muda mrefu." (Habermas 1984: 57) Pili, nadhari ya kuzimia pia inapuuza suala la Yesu kuchomwa mkuki ubavuni. "Daktari aliyefuatilia jambo hili alisema na wakati wote alikubali kwamba uchunguzi wa Kidaktari upo sahihi. Upo uwezekano kwamba maji yalitoka kwenye kifuko kilichouzunguka moyo, wakati ambao damu ilitoka upande wa kulia wa moyo. Ingawaje Yesu alikuwa hai kabla ya kuchomwa mkuki, kwa hakika mkuki ndio uliomwua. Kwa hiyo, kovu la kifuani pia linaikataa nadharia ya kuzimia." (Ibid.: 58) Tatu, kama angeliweza kwa sehemu kuvumilia kusulubiwa, ni jinsi gani angeweza kuliondoa jiwe kubwa lililokuwa limeufunga mlango wa kaburi? Akiwa kwenye hali yake mbaya na dhaifu kimwili, angeweza kuondoa kitu ambacho hata mtu mwenye nguvu na afya njema angepata shida kuliondoa (kulingana na desturi)? Hili lingekuwa jambo gumu Zaidi hasa ikikumbukwa kwamba jiwe lilitakiwa kusukumwa kwenda mlimani ili kutoka kwenye mlango wa kaburi." (Habermas 1984: 56-57)

Mwisho, nadharia ya kuzimia kwa mapana inahusisha mshtuko mkubwa ambao unaweza kuua chochote kilicho hai. David Strauss (ambaye ni adui wa Wongofu wa Ukristo) mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Strauss alionyesha kuwa, "Ni vigumu kwamba kiumbe aliyeibiwa akiwa nusu mfu kutoka kaburini, ambaye ni mdhaifu na mgonjwa, anayehitaji matibabu, aliyetakiwa kufungwa bandeji, kuimarishwa na kuhurumiwa, ambaye mwishowe aliyabeba mateso yake, ambaye wanafunzi wake wangepata mtazamo kwamba alikuwa mshindi juu ya kifo na kaburi, mfalme wa maisha, mtazamo ambao ungejengea msingi wa huduma yake baadaye. Uvuvio huo ungedhoofisha mtazamo ambao ulifanywa kwenye maisha na kufa, kwamba ingewapa wao sauti ya maombolezo, lakini haukuwepo uwezekano wa kubadili huzuni yao kwa furaha na, kuinua heshima yao kuwa ibada." (Strauss 1865: 412)

**I.** ***Hitimisho***

Ukweli kwamba Yesu alikufa kwa kusulubiwa ni tukio "lenye nguvu lililo wazi kihistoria" ambalo kwamba "limekubaliwa na kila msomi aliyejifunza juu ya somo hilo, hata yule ambaye amejawa na mashaka" (Habermas na Licona 2004: 44; angalia ibid.: 48-49). Hata Muislamu Alhaj A. D. Ajijola, mjumbe wa baraza kuu la mambo ya Kiislamu la Nigeria, anasema "ni ukweli wa kihistoria kwamba Yesu, mwana wa Mariamu, aliwekwa msalabani" (Ajijola 1972: 72). Pia anakiri kwamba "Wakristo na Wayahudi, pamoja na tofauti zao, wanakubaliana kwamba Yesu alikufa msalabani. Historia ya utawala wa Rumi inaungana na ukweli huu." (Ibid.: 39) Vivyo hivyo, Ajijola anakubaliana na fundisho la Uislamu na kumfanya kutokuheshimu kile alichokikiri kuwa ukweli wa kihistoria na kuutangaza, "Miaka mia sita baada ya Yesu, mtu kutoka jangwa la Arabia alijitokeza na kutangaza kinyume ulimwenguni kote: 'Hawakumchinja wala kumsulubisha.' [**Q. 4:157**] Madai haya yanasimama kama muujiza wa Mohamedi nabii asiyesoma wa Rasi ya Arabuni (Baraka za Mungu ziwe juu yake)." (Ibid.: 39-40)

Kweli za hapo juu pamoja na hitimisho vina umuhimu mkubwa kuhusiana na msingi wa kukubaliwa kwa Korani. Kama Eddy na Boyd wanavyoonyesha, "Kama kuna kweli yoyote ya maisha ya Yesu ambayo imepata kutambuliwa kwa kukubalika kwake kote, ni ukweli wa Yesu kusulubiwa. Kwa Korani kuukosea msingi huu muhimu kunasababisha maswali kuhusiana na kweli za kihistoria kwa *kila* madai itakayoyafanya juu ya Yesu." (Eddy na Boyd 2007: 172)

**V. <u>Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Kufufuka</u>**

Takwimu za kihistoria zinafanana na zile zilizoanza kwamba Yesu alikufa kwa kusulubiwa pia kusema kwamba mwili wake ulifufuka toka kwa wafu. Uislamu wanafundisha kwamba Yesu alihamishwa akiwa na mwili kwenda mbinguni, ilivyokuwa kwa Henoko na Elia na vivyo hivyo kwa kupaa kwa Yesu siku arobaini baada ya kufufuka kwake kama ilivyoandikwa kwenye Biblia (**Q. 4:157-58**; angalia pia **Q. 3:55**; linganisha na **Mwanzo 5:24; 2 Wafal 2:1-11; Matendo 1:9-11**). Hata hivyo, kufufuka ni tofauti na kuchukuliwa mbinguni:

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

"Kufufuka ni kuinuliwa mwili mtu aliyekufa kutoka kaburini kuwa na uhai tena" (Craig 1981: 133; angalia pia Wright 2003: 109 ["Ufufuo ni kile ambacho *hakikufanyika* kwa Henoko na Elia"]). Yesu alitabiri kufufuka kwake na alitoa kama jaribio ambalo kwalo tungejua kwamba alikuwa akiwaambia ukweli (**Math 12:38-40; 16:1-4; Yohana 2:18-21;** *angalia pia* **Marko 14:58; Luka 11:29-30; Warumi 1:4**). Kwamba alifufuliwa ni ukweli, swali la kihistoria: kama alifanya au hakufanya. Takwimu za kihistoria zifuatazo zinaonyesha kwambaYesu kwa hakika mwili wake ulifufuliwa toka kaburini:

**A.** ***Kaburi lilikuwa tupu***

Kaburi alilozikwa Yesu lilikuwa la Yusufu wa Arimataya (**Math 27:57-60; Marko 15:45-46; Luka 23:50-53; Yohana 19:38-42**); hivyo ni kaburi ambalo lilijulikana. Zaidi, wanawake waliokwenda kaburini siku ya jumapili baada ya maziko waliona mahali alipokuwa amelazwa Yesu, hivyo walijua eneo lilikokuwa kaburi (**Math 27:61; Marko 15:47; Luka 13:55; Yohana 20:1**).

1. <u>Umuhimu wa Wanawake.</u> Siku ya jumapili iliyofuata baada ya maziko, Mariamu Magdalene na wanawake wengine walikwenda kaburini, wakakuta jiwe limeviringishwa mbali na kaburi lilikuwa tupu, na walikutana na Kristo mfufuka (**Math 28:1-7; Marko 16:1-9; Luka 24:1-8; Yohana 20:1**). Waliwataarifu wanafunzi kwamba kaburi lilikuwa tupu na kwamba Yesu alikuwa amefufuka kutoka kaburini na yuko hai (**Math 28:8; Marko 16:10-11; Luka 24:9-12; Yohana 20: 2-18**). Kwa kifungu hiki ni wazi kwamba mwanzo wa kuonekana kwa Yesu kulifuatiwa na kufufuka kwake na mwanzo wa taarifa ya kufufuka iliyotolewa na wanawake. Kweli hizi zinaonyesha kwamba maelezo ya Biblia ni ya kuaminika. Sababu ni kwamba kwa Wayahudi wa zamani wanawake hawakuonekana kwamba ni mashahidi wa kuaminiwa; hawakuwa mahiri kusimama kama mashahidi mahakamani au kuwa na ukomo wa wazi kwenye ushuhuda ambao wangetoa ("Mashahidi" 2008: n.p.; Meacham 2009: sheria nyingine). Paul Maier anavyoeleza, kwakuwa ushuhuda wa wanawake ulionekana kutokuaminiwa, "kama maelezo ya kufufuka yalikuwa ya kutengenezwa . . . wanawake *kamwe* wasingehusishwa kwenye mkanda huo, hata hivyo, wasingewekwa kama mashahidi wa kwanza" (Maier 1973: 98).
2. <u>Umuhimu wa Wayahudi.</u> Viongozi wa Wayahudi hawakupinga kamwe kwamba kaburi lilikuwa tupu. Badala yake, wakati askari wa Kirumi alipotoa taarifa kwa kuhani mkuu kile kilichotokea, viongozi wa Wayahudi walimpa rushwa askari na kutengeneza uongo kwamba *"wanafunzi wake walikuja usiku na kumuiba"* (**Math 28:11-15**). "Kwenye karne ya pili A.D. na mbeleni baada ya Mathayo kuandika tukio la kwanza, Mamlaka ya Yerusalemu iliendelea kukiri kaburi tupu kwa kuelezea kwamba wanafunzi waliuiba mwili. Kwa kuwa, kwenye *Mjadala wake na Trypho [ukurasa wa. 108],* Justin Martyr, aliyetokea jirani ya Samaria, alitaarifu c. 150 A.D. kwamba mamlaka ya Wayahudi walituma watu maalum waliowapatia fedha kuzunguka Mediterranean kuyasimamisha madai ya Wakristo kwa maelezo yao ya kufufulia."(Ibid.: 116-17)

   Kwa nyongeza, Edward Bode anaonyesha madai kwamba mwili uliibiwa yalitolewa na kuendelezwa mapema, kwa sababu baada ya kitambo kirefu mambo mengine mengi yametukia kuelezea kuwa kwake tupu. . . . Zaidi ya hayo, ujasiri [madai ya viongozi wa Kiyahudi] yasingeshindana na uwepo wa kaburi tupu; badala yake ingekubaliana na ukweli wa kaburi tupu kwa kujaribu kuelezea utupu kwa namna nyingine tofauti na kufufuka kwa Yesu." (Bode 1970: 163; angalia pia Wright 2003: 638) Kama William Lane Craig alivyoeleza, "Propaganda za Wayahudi wa awali kinyume na yale aliyoyaandika Mathayo yanakubaliana na kubeba ushahidi wa ukweli kwamba Kaburi la Yesu lilikuwa tupu. Ushahidi huu una nguvu Zaidi kwa sababu ulitokanan na maadui wa Wakristo 'Wazushi wenyewe." (Craig 1981: 83-84)
3. <u>Ukosefu wa ibada ya kaburi.</u> Upo ukweli mwingine muhimu ambao ni lazima kuuangalia. Dunn anautazama, "Moja ya mambo ambayo siyo ya kawaida kuyaangalia ni kwamba hapana kumbukumbu yoyote ya tangu miaka ya awali ya Ukristo ya kaburi lililokuwa linapewa heshima kama mahali alipolazwa Yesu. . . . Kwa kweli hili ni jambao lisilo la kawaida, kwa sababu kwa ndani ya muda mfupi Wayahudi, kama dini nyingine, tamanio la kumbukumbu ya kujengea kaburi la yule waliyemheshimu na (kwa maana) kwa kuheshimiwa kwa eneo hilo kumethibitishwa wazi. . . . Kwanini Wakristo wa kwanza hawakuachilia jambo hili muhimu la asili la kiibada? Jibu pekee la wazi kwenye mwanga wa ushahidi huu limefunuliwa ni kwamba hawakuliamini kaburi lililoubeba mwili wake. Hawakuyaabudu mabaki kwa sababu hawakufikiri kwamba kulibaki kitu chochote cha kuabudiwa." (Dunn 2003: 837-38; angalia pia Craig 1981: 63) Kutokuabudiwa kwa kaburi la Yesu ni tofauti na kuabudiwa kwa makaburi na mifupa ya wakristo wafia dini wa kwanza (angalia *The Martyrdom of Polycarp* c.160: 18). Ni tofauti pia na kaburi la Mohamedi huko Madina ambalo hadi leo lilibaki kuwa eneo la kutembelewa na kuabudiwa na Waislamu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Mwanahistoria Michael Grant anahitimisha, "Kama tukitumia vigezo vile vile ambavyo vingetumiwa na watu wa kale kama vyanzo, basi ushahidi ni sahihi na wa kukubalika vyakutosha kutulazimu kuhitimisha kwamba kaburi kwakweli lilikuwa tupu" (Grant 1977: 176).

**B.** ***Wakristo wa kwanza walianza kutangaza kufufuka kwa Yesu hata Yerusalemu***

Ukweli kwamba kaburi la Yesu lilikuwa tupu na uhakika wa Imani ya Wakristo kwenye ufufuo umethibitishwa na ukweli kwamba Wakristo wa kwanza hawakusubiri kwa miongo ili kutangaza kufufuka kwa Yesu (ili kwamba ushuhuda usiwe umekufa) lakini walifanya hivyo tokea awali.[19] Hawakwenda kutangaza kufufuka kwa Yesu kwenye mikoa ya mbali (mahali ambapo wasingepata upinzani), lakini walianzia kutangaza pale pale Yerusalemu, Mji ambao ndiko alikouliwa Yesu na kuzikwa na maadui zake wa kwanza, viongozi wa Wayahudi na Warumi, walikuwa maarufu zaidi (**Matendo 2-7**).

Edward Bode anakumbusha, "Kuwapa Wayahudi wazo la kufufuka kwa mwili na wakati huo huo wakilijua eneo liliko kaburi, ni jambo ambalo lisingewezekana kumhubiri Yesu mfufuka ndani ya Yerusalemu kama hilo kaburi lingekuwa limeushikilia mwili bado. Kwa ufahamu wa Wayahudi juu ya kufufuka na uwepo wa kaburi, mara iyo hiyo au baadaye wangemtuma mtu wao wenyewe kuona kama kaburi lilikuwa tupu." (Bode 1970: 174; angalia pia Craig 1981: 82-83) "Kaburi tupu lisingethibitisha kufufuka kwa Yesu au kuumbia imani. *Lakini kinyume chake siyo kweli.* Kama mamlaka ya Wayahudi wangeweza kuutengeneza mwili wa Yesu, hatimaye wangeweza *kutokukubaliana* na kufufuka kwa Yesu, kama wanafunzi walivyoamini na kutangaza" (Neill 1964: 288, fafanuzi ya asili). Viongozi wa Wayahudi walikuwa na maana, sababu, na fursa ya kuzuilia vuguvugu la awali la Wakristo, na kirahisi sana wangeweza na kwa bidii wangeenda kaburini, kuutoa mwili uliokufa wa Yesu, na kuutembeza ili kila mmoja auone; lakini hawakufanya hivyo kwa sababu wasingeweza.

Hayo pia ni ya kweli kwa mamlaka ya Rumi ambayo zaidi ya mambo mengine yote, walitaka kudumisha Amani na kuepuka migongano miongoni mwa wale waliowaongoza. Terry Miethe anaeleza kwamba "iwe miaka saba, miaka nane, au miaka kumi, madai ni kwamba mwili haukuwepo pale, kwamba mashahidi wote walioona kwa macho yao walikuwa bado wapo hai, na kwamba Kanisa lilisababisha mtafaruku mkubwa kwa kudai kwamba serikali ya Kirumi ilipaswa kuyaweka hayo vizuri kwa kutengeneza ushahidi utakaopingana" (Miethe 1987: 70). Hivyo, "Kama mamlaka ya [Wayahudi au Warumi] wangeweza kutengeneza mzoga wa Yesu, wangeilipua Imani ya kufufuka milele; Ukweli kwamba walishindwa kuilipua unadhihirisha kwamba hawakuweza kutengeneza mzoga wa Yesu, na kushindwa kwao kufanya hivyo . . . kunaonyesha kwamba wasingeweza kuutengeneza." (Packer 1987: 149) Kushindwa kwa maadui wa kwanza wa Ukristo kuutengeneza Mwili wa Yesu ni ushuhuda wa kweli kwamba kaburi lilikuwa tupu—na maelezo pekee ya kweli na ya kuaminika kwa yote ni kwamba kaburi lilikuwa tupu kwa sababu alifufuka kutoka kaburi kama alivyotabiri na kama wanafunzi wake walivyokuwa wakitangaza.[20]

**C.** ***Mashahidi wengi***

Mwanzoni, tuliitafakari Imani ya wakristo wa kwanza, pamoja na **1 Wakor 15:3-7**. Imani hiyo ni ya muhimu sana kwa kuwa inarudi nyuma hadi mwanzoni mwa mwaka AD 30, kimsingi kwenye kusulubiwa na kufufuka kwenyewe, na kujengewa msingi wa ushuhuda na wale walioyaona wenyewe (Habermas 1987: 43; angalia pia Habermas 1984: 125 na nukuu zilizopo). Aya ya 4-7 ya Imani inasema: *"[4] Na kwamba alizikwa,na kwamba alifufuka siku ya tatu kama yanenavyo maandiko,[5] na kwamba alimtokea Kefa, baadaye wale Thenashara.[6] Baadaye aliwatokea ndugu wengine Zaidi ya mia tano kwa wakati mmoja, wengi wao wakiwepo hadi sasa na wengine,lakini wengine wamekwisha kulala;[7] baadaye alimtokea Yakobo, baadaye aliwatokea mitume wote."* A. M. Hunter anaonyesha kwamba**1 Wakor 15:3-7** "ni ushuhuda wa asili wa ukweli wa kufufuka unaoturudisha nyuma ndani ya miaka makumi ya kusulubiwa, na kwa sasa inaitwa 'makala ya zamani ya Kanisa la Kikristo tulilo nalo.' Zaidi ya hayo, Ni'asili' ambaye *ukweli ulikuwa wazi kwa kushuhudiwa.* Wakati Paulo anaandika, Petro na Yakobo walikuwa bado wapo hai na miongoni mwa wale'ndugu mia tanao' walikuwa hai bado na wangeweza kuulizwa." (Hunter 1976: 100, fafanuzi ya asili.) Habermas anaandika ufupisho wa umuhimu wa Imani ya kwanza: "Isingekuwezekana kusema kwamba hapakuwa na uthibitisho wa

---

[19] Ukweli kwamba wanafunzi wa Yesu walianza kutangaza *kufufuka kwake* na ni uthibitisho wa *kusulubiwa kwake.* Kutangaza kwamba mtu amefufuka toka kwa wafu hakuna maana hadi pale ambapo mtu *amekufa* kwanza.

[20] "Mbegu kwa chipukizi la kwanza na kukua kwa Kanisa kulianzia kwenye mji wa Yerusalemu wenyewe, mahali ambapo, sehemu nyingine zote, ingelikuwa ni dhihaka kumhubiri Yesu mfufuka mpaka pale ambapo mitume na wasikilizaji wao wanajua kuwa Kaburi la Yusufu lilikuwa tupu. Miezi michache baadaye, mamlaka walikata tamaa kuzimisha vuguvugu ambalo hatimaye waliwaanzishia mateso. Kitu kingine ambacho kingekuwa na ufanisi kidogo labda ingekuwa ni kuelezea kinyume cha habari kwamba kulikuwa na mwili kwenye kaburi la Yusufu, lakini jaribio hilo halikufanywa kwa sababu walikuwepo wa Yerusalemu wengi walioona wenyewe kwamba kaburi lilikuwa tupu kwa wakati ule." (Maier 1973: 120)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

awali, ushuhuda wa waliokuwepo kwenye ufufuo au kwa mafundisho mengine ya muhimu kwa Ukristo, kwa kuwa Imani hii inatupa ushahidi wa kimaandiko kuhusiana na kweli ya injili, ambayo ni msingi wa Imani ya Ukristo. Inatuunganisha na tukio lenyewe na wale wlioshiriki kwa wakati na mahali penyewe. . . . Ukweli kwamba walikuwa mashuhuda halisi waliotoa yale ambayo tukio hilo linadhihirisha kwamba wasimuliaji waliofuata baadaye wasingeweza kusimulia ushuhuda huu wa msingi." (Habermas 1984: 126-27)

Kwa heshima ya mashahidi 500, C. H. Dodd anaangalia, "Ingekuwa vigumu kwa kusudi lolote kuutaja ukweli kwamba wengi wa wale 500 walikuwa bado hai, mpaka pale Paulo aliposema, kwa hakika, 'mashahidi walikuwepo ili kuhojiwa'" (Dodd 1968: 128). Ni muhimu kukumbuka kwamba "Waraka wa Paulo ulikuwa kwa ajili ya Kanisa na kwa hiyo ulikuwa ni Makala ya wazi kwa watu wote, ulioandikwa ili kusomwa kwa sauti. Paulo alikuwa akiwaalika kila mmoja mwenye mashaka kwamba Yesu aliwatokea watu baada ya kifo chake kwenda kuzungumza na mashahidi waliokuwepo wakati wa tukio kama alitaka. Ilikuwa ni changamoto yenye ujasiri na ambayo kwa urahisi ingeweza kuchukuliwa, kwa kuwa ulikuwa ni wakati wa Amani kwa dola ya Rumi kutembelea eneo lote la Mediterranean kirahisi na salama. Paulo asingeleta changamoto hiyo Kama kweli hao mashuhuda wasingelikuwapo." (Keller 2008: 204)

**D.** ***Maisha ya Wakristo wa kwanza yalibadilishwa kwa kile walichikiona***

Kama ilivyoelezwa mwanzoni, wanafunzi hawakuamini taarifa iliyoletwa na wanawake kwamba Yesu alifufuka toka kaburini. Kisha Yesu akawatokea wanafunzi ili kuwadhihirishia kuwa hayakuwa maono, au mang'amung'amu, au roho, au miungu; aliwataka wauguse mwili wake, na alikula pamoja nao (**Luka 24:36-43; Yohana 20:19-29; 21:9-14**). Kutokea kwa Yesu mwenyewe baada ya kufufuka kwa mwili wake kuliwabadilisha wanafunzi. Habermas na Licona wanajadili hili: "Baada ya kifo cha Yesu, maisha ya wanafunzi yalibadilishwa kiasi kwamba waliyastahimili mateso na hata kifo. . . . Linganisha hili na kutiwa kwao moyo na tabia yao wakati Yesu anakamatwa na kuuawa. Walimkana na kumwacha, na walijificha kwa hofu. Baadaye, kwa hiari yao walijihatarisha kwa kutangaza hadharani kufufuka kwa Kristo. Kweli hizi zinathibitishwa na maelezo mengi, toka kwenye vyanzo vya agano jipya kama vilivyo vya walio nje yake." (Habermas na Licona 2004: 56) Clement wa Rumi, anayeaminiwa kwamba aliona mitume (Irenaeus c.185: 3.3.3; Tertullian c.200: 32), aliandika hata mwishoni mwa karne ya kwanza kwamba ujasiri wao wa kuhubiri ni kwa sababu "walikuwa na uhakika kupitia kwa kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo" (Clement c.95: ch. 42). Habermas na Licona wanahitimisha, "Kama Paulo, Yakobo na wanafunzi halisi hawakuamini kwamba walimwona Bwana mfufuka, maisha yao yasingelibadilishwa. Wasingeuhubiria ulimwengu habari za Yesu na kufufuka kwake, hivyo wasingeteseka hata kuuawa kwa matendo yao ya uinjilisti na Ukristo usingelikuwepo leo." (Habermas na Licona 2004: 270n.44)

Wakati mwingi Agano Jipya limezungumzia mateso waliyoyapata wanafunzi wa kwanza wale waliomwona Yesu mfufuka na ujasiri ambao kwao walitangaza kuwa Yesu alifufuka na kwamba ni Bwana (mfano, **Matendo 4:1-31; 5:17-42; 6:7-7:60; 8:1-3; 9:1-31; 12:1-5; 14:1-28; 16:16-40; 18:12-16; 20:17-24; 21:10-13, 27-26:29; 28:16-31; 2 Wakor 11:23-33**). Polycarp, ambaye aliuawa mwenyewe yapata mwaka AD 160 (*Martyrdom* c.160: 9), kwenye *Waraka wake kwa Wafilipi* (c.110) hakuthibitishi tu kuteswa kufa kwa Paulo na mitume wengine lakini pia chanzo cha Imani yao—kufufuka kwa Kristo: "Kwa kuwa hawakuupenda Ulimwengu huu, lakini kwake yeye aliyetufia, na kwa ajili yetu alifufuliwa tena na Mungu kutoka kwa wafu" (Polycarp c.110: 9). Kama mtu anatafuta ushahidi wa Kihistoria, maelezo pekee yanayokubalika kwa mabadiliko haya ya kushangaza ya tabia na maisha ya wanafunzi ambayo pia yanadhihirishwa na ushahidi unaotambulikana (mfano, Kifo cha Yesu, maziko yake, kaburi tupu) ni kufufuka kwa mwili kwa Yesu. Origen anaelezea hili kwenye mwaka AD 248: "Lakini kwa kweli na uthibitisho usio na shaka [wa kufufuka kwa Kristo] Ninaushikilia wajibu wa wanafunzi wake, waliojitoa wenyewe kufundisha mafundisho ambayo yalikuwa ya kuhatarisha maisha ya mwanadamu,—fundisho ambalo wasingelifundisha kwa ujasiri waliokuwa nao juu ya kufufuka kwa Yesu kutoka kwa wafu; ambaye pia, wakati huo huo, siyo tu kwamba linawaandaa wengine kukidharau kifo, lakini wao wenyewe walikuwa wa kwanza kudhihirisha kuyadharau matishio." (Origen 248: 2:56) Ujasiri wa kuhubiri kufufuka kwa Yesu mbele ya mateso na kifo kunaikana nadharia ya kuzimia, nadharia ya mwili kuibiwa, au hata "uakilishi mwingine" ambao unajaribu kuondoa ukweli wa kufufuka, kwa sababu hakuna atakayekuwa tayari kuteswa na kufa kwa ajili ya kile anachokijua kuwa ni uongo.[21]

[21] Charles Colson alisema, "Lakini vipi kwa habari ya Mitume? Watu kumi na wawili wasio na nguvu, wakulima kweli, walikabiliana siyo tu na usumbufu au vurugu za kisiasa, lakini walipigwa, kupigwa mawe, kuuawa. Kila mmoja wa wanafunzi alisisitiza, hadi kwenye pumzi ya mwisho ya uhai wao, kwamba kwa macho yao walimwona Yesu akifufuka kwenye mwili kutoka kwa wafu.Unafikiri kwamba miongoni mwa hao wanafunzi angejitoa kabla ya kukatwa kichwa au kupigwa mawe? Kwamba mmoja wao angeweza kufanya mpango na wenye mamlaka? Hakuna aliyefanya hivyo. Unaona, watu wanaweza kuyatoa maisha yao kwa kile wanachokiamini kuwa ni cha kweli—hawawezi kuyatoa maisha yao kwa kitu

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Ni kweli, kwamba watu wengi wapo tayari kufa kunakosababishwa na unyofu wa kile wanachokiamini hata kama wale wanaosababisha kuthibitisha ni waongo au wabaya. Hata hivyo, Habermas na Licona wanaonyesha kuwa, kwa kuwaheshimu Wakristo wa kwanza waliokabiliana na mateso na kuuawa kwa ajili ya Imani yao, "Ipo tofauti muhimu kati ya kifo cha mitume na wale wanaoifia Imani yao siku za leo. Wanaojitolea kufa nyakati hizi wanafanya hivyo siyo kwa ajili ya kile wanachokiamini ila kwamba wengine wamewa fundisha. Mitume walikufa kwa kushikilia ushuhuda wao wenyewe kwamba wao *wenyewe* walimwona Yesu mfufuka. Wanaojitolea kufa kwa sasa wanakufa kwa kile *wanachokiamini* kuwa ni kweli. Wanafunzi wa Yesu walikufa kwa kile *walichokijua* kwamba ni cha kweli au cha uongo." (Habermas na Licona 2004: 59)

**E.** ***Kuongoka ghafla kwa Paulo, adui wa Kristo***

Mtume Paulo, mwanzoni akijulikana kama Sauli wa Tarso, alikuwa Farisayo msomi (**Matendo 22:3; 26:4-5; Wafil 3:4-5**). Aliyejituma sana kwa Imani yake ya Kiyahudi, aliamini kwenye Mungu mmoja, alikulia, kufundishwa na kuwa na juhudi nyingi kwenye kuwatesa Wakristo (**Matendo 7:54-8:3; 9:1-2; 22:4-5; 26:9-11; Wafil 3:6**). Hata hivyo, alipokuwa akiendelea na kuwatesa Wakristo, Ghafla Paulo aliongoka na kuwa Mkristo (**Matendo 9:1-22**). Ninini kilichotokea kwa kuongoka huku kwa ghafla—Mmoja aliyembadilisha Paulo kutoka kuwa mtesi na kuwa mteswa? Paulo mwenyewe anaeleza sababu ya kubadilika kwake ni pale alipokutana na Kristo mfufuka. Aliongeza kwenye ile Imani ya awali ya mitume kwenye **1 Wakorintho 15**, *"na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake"* (**1 Wakor 15:8**; angalia pia **Matendo 22:1-16; 26:1-23; 1 Wakor 15:9-10; Wagal 1:11-24; Wafil 3:6-10**). Maelezo ya Paulo ni ya kuaminika kwa sababu yeye binafsi alikuwa tayari kuendelea kuteseka na hata kufa kwa Imani yake kwa Kristo aliyefufuka. Zaidi, viongozi wa Kanisa la kwanza waliomlea walimhesabu na kumpa mamlaka ya kiutendaji kama Mitume wengine (angalia **2 Pet 3:16**; Polycarp, c.110: 3:2; 9:1; Ignatius, c.110a: 12:2; c.110b: 4:3).

Wakati watu wengi wakihama kutoka kundi moja la imani kwenda jingine, Habermas na Licona wanatukumbusha kwamba "Wakati mwingi watu huongoka kwenye dini hushika kwa kusikia ujumbe kutoka kwenye chanzo cha pili na kuuamini ujumbe. Kuongoka kwa Paulo ni kile walichokiona kuwa ni kutokewa binafsi na Yesu aliyefufuka. Leo tunaweza kuamini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ni ujumbe wa kutoka chanzo cha pili cha uthibitisho, Kumuamini Paulo na wanafunzi waliomwona Yesu aliyefufuka. Lakini kwa Paulo, uzoefu wake ulitokana na uthibitisho wa msingi: Yesu aliyefufuka alimtokea moja kwa moja. Hakuamini kwa maneno yaliyotokana na ushuhuda wa mtu fulani. Kwa hiyo, tofauti ni vyanzo vya msingi na kile cha pili." (Habermas na Licona 2004: 66)

**F.** ***Kuongoka ghafla kwa Yakobo, aliyekuwa na mashaka juu ya Kristo***

Biblia inaonyesha kwamba Yesu alikuwa na ndugu wengi, mmojawapo alikuwa ni Yakobo (**Math 13:55-56; Marko 6:3;** angalia pia **Math 12:46-47; Marko 3:31-32; Luka 8:19-20; Yohana 2:12; Matendo 1:14; 1 Cor 9:5; Wagal 1:19**). Wakati wa maisha ya Yesu, Yakobo na ndugu zake hawakuamini kuwa Yesu alikuwa kile alichodai na kwa hakika walimwona kama aliyechanganyikiwa (**Marko 3:21, 31; Yohana 7:1-5**). Wakati akiwa msalabani, Yesu alimkabidhi mama yake kwa kutunzwa na mwanafunzi wake Yohana badala ya ndugu yake mwenyewe kuthibitisha kwamba Yakobo hakuwa anaamini (**Yohana 19:25-27**).

Baada ya Yesu kufa na kufufuka, kama Paulo alivyosimulia kwenye Imani ya kale,*"tena alimtokea Yakobo"* (**1 Wakor 15:7**). Ingawa tu maelezo machache ya kuongoka kwa Yakobo zaidi ya yale ya kuongoka kwa Paulo, kweli za kihistoria zinaonyesha kwamba kuongoka kwa Yakobo kulikuwa kwa ghafla na kwa nguvu kubwa kama ilivyokuwa kwa Paulo. Kutokewa kwa Yakobo na Yesu aliyefufuka kimsingi ilikuwa ni mapema, kwa sababu Yakobo ni miongoni mwa wale waliokuwa wakisubiri orofani kule Yerusalemu kujazwa na Roho mtakatifu kulikotokea siku ya Pentekoste; hili linaweka kutokewa kwa Yakobo ndani ya siku 50 baada ya kufufuka (**Matendo 1:14**). Yakobo baadaye alikuwa kiongozi wa Kanisa huko Yerusalemu (**Matendo 15:13-21; Wagal 1:19**). Aliandika moja ya waraka uliopo kwenye Agano Jipya. Alikuwa mwongofu kamili kiasi kwamba, yeye kama wanafunzi wengine wa zamani, alikufa kifo cha kuuawa, kilichoshuhudiwa na vyanzo vya Wasio wakristo na Wakristo (Josephus 93: 20.9.1; Eusebius 325: 2.23).

Kama ilivyo kwa Paulo, Swali ni lazima liulizwe: Ni maelezo gani mazuri yanayoweza kutolewa kwa kuongoka huku na kwa kubadilishwa maisha ya Yakobo, aliyekuwa na mashaka hapo awali? Maelezo rahisi yanayokubalika na kwamba yaweza kuubeba ukweli wote ni kile kilichowekwa *tokea mwanzo* (**1 Wakor 15:7**) ni Yakobo kutokewa na Kristo aliyefufuka. Kama Wright alivyoliweka, "Ni vigumu kutolea maelezo kwa

---

wanachojua kuwa ni cha uongo." (Colson 2002: n.p.) Kama Habermas na Licona walivyoonyesha, "Kama mashahidi waliokuwepo kwenye tukio *kweli waliamini* kuwa alifufuka kutoka kwa wafu, tunaweza kuhitimisha ubishi kwamba waliuiba mwili na kuunda hadithi. Kwa kweli, karibia wasomi wote wamekubaliana kwenye hili, kwa nafasi zao za kitheolojia." (Habermas na Licona 2004: 62)

kiongozi huyu muhimu na asiyelinganishwa hadi hapo yeye mwenyewe kujulikana kwamba alimwona Yesu aliyefufuka" (Wright 2003: 325).

**G. *Muundo na uwepo wa kanisa la Kikristo***

Wakati Yesu akiwapo ulimwenguni wanafunzi wake hawakuwa na uelewa juu ya kufa na kufufuka kwa Masihi; bado "hata wengi wa wasomi waliokuwa na wasiwasi walipokiri kwamba angalau *Imani* kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu lilikuwa kwenye moyo wa Imani ya Wakristo wa kwanza" (Craig 1981: 127). Imani hiyo ilitoka wapi? Imani hiyo haikutokana na wapagani. Kwa kuunganishwa na utafiti wa kina wa Imani ya Kipagani kuhusiana na kufufuka na maisha baada ya kifo, N. T. Wright anafupisha, "Ukristo ulizaliwa kwenye ulimwengu ambao msingi wa madai yao ulionekana kuwa ni wa uongo. Wengi waliamini kwamba wafu hawaishi tena; nje ya Wayahudi, hakuna aliyeamini kufufuka." (Wright 2003: 35; kwa uchunguzi wa Wright angalia kumbukumbu ibid.: 32-84)[22] kuhusiana na suala hili muhimu, Craig anaangalia, "Kama mtu akikataa kwamba Yesu kweli hakufufuka kutoka kwa wafu, basi ni lazima aelezee Imani ya wanafunzi kwamba alifufuka kwa mujibu wa ushawishi wa Wayahudi au kwa mujibu wa ushawishi wa Wakristo" (Craig 1981: 129). Ni wazi kuwa, kuamini kwenye kusulubiwa na kufufuka kwa Masihi hakutokani na ushawishi wa Kikristo, kwa sababu Ukristo haukuwepo. Wazo hili pia halikuja kutoka kwa Wayahudi kupitia Wayahudi wengine kuamini kwenye kufufuka: "Msingi wa Wayahudi wa kufufuka umetofautiana kwenye mambo muhimu mawili, Msingi wa kuheshimu kufufuka kwa Yesu. *Wakati wote* Wayahudi hufikiri kuwa kufufuka (1) kutatokea baada ya mwisho wa Dunia, siyo kwenye historia, na (2) kutawahusu watu wote na siyo mtu mmoja mmoja. Kwa kudhibitisha hili, kufufuka kwa Yesu kulikuwa kwa pande zote mbili ndani ya historia na kwa mtu binafsi." (Ibid.) Hivyo, Professor C. F. D. Moule anahitimisha, "Kwa wakati Fulani sikufikiri chochote juu ya Agano la kale kwamba lingeonyesha jambo hili [imani ya kufufuka Masihi]. . . . Sikuweza kugundua chochote [Kwenye mstari wowote wa Agano la kale au Biblia ya ziada ya Imani ya Kiyahudi] kinachozungumzia kuingia kwenye *uzima* wa milele kwa mtu *binafsi, kabla ya* kuhitimisha historia: na *ni kwenye* hili mtu anapaswa kulielezea." (Moule 1972: 508, fafanuzi la asili)

Hata hivyo, "*jambo fulani* ni lazima lilitokea asubuhi ya Pasaka lililochochea mlipuko huo wa Kiroho unaoitwa Ukristo" (Maier 1973: 105, fafanuzi limeongezwa). Ni "jambo gani hilo Fulani"? Ndilo pekee linalokubalika kuelezea *asili* ya Ukristo—inayohitaji elimu ya Kiungu (theolojia) kwa kina kubadilisha Imani ya mwanzo ya Kiyahudi—ndivyo Yesu alivyokuwa, kwa kweli, alifufuka kutoka kwa wafu. Hakuna maelezo

[22] Baadhi ya Imani za Kipagani, bila shaka, zina simulizi za kufa na kuinuka miungu na mizuka kama vile Adonis, Attis, Demeter, Dionysus, Persephone, Isis na Osiris, Tammuz, na Balder, mwana wa mungu Norse Odin. Simulizi hizo haziwezi kuchukuliwa kama *ushahidi* wa kihistoria kama wa kusulubiwa na kufufuka kwa Yesu. Zaidi, C. S. Lewis anakumbusha udanganyifu wa kimantiki wa kutolea mfano simulizi hizo kama sababu ya kufifisha historia ya ukweli wa kufufuka kwa Kristo: "Hoja ya Agnostic kutokana na ile inayofanana kati ya Ukristo na Upagani zinafanya pale tu unapokuwa una majibu. Kama ulianza kwa kujua kutoka kwenye msingi mwingine kwamba Ukristo ni uongo, basi simulizi za kipagani zitakuwa msumari mwingine kwenye jeneza: kama vile ukianza kwa kujua kwamba hakuna kitu kinachofanana na mamba, basi simulizi za kwamba kuna aina nyingine ya joka inaweza kuthibitisha kutokuamini kwako. Lakini kama ukweli wa Ukristo ni wa kuhojiwa sana ambao unaujadili, basi hoja kutoka kwa Anthropolojia ni uhakika wa *petitio* [i.e., *petitio principii*—udanganyifu wa kimantiki wa "kuanza swali" ambapo kile kinachotakiwa kuthibitishwa kinachukuliwa kwa usahihi]." (Lewis 1970: 132)

Kujidhihirisha kuwa simulizi hizo za kipagani hazikuwa chanzo cha Imani ya Kikristo kwenye kufufuka kwa Yesu, kwa sababu Wakristo wa kwanza wote walikuwa Wayahudi, wakitokea Uyahudi, na siyo Wapagani. Wright anaeleza, "Yupo muumini yeyote wa kwenye Imani hii, kutoka Misri hadi Norway, wakati wowote wa zamani, alifikiri kwamba mwanadamu halisi, ambaye alikufa anaweza kuwa hai tena? Bila shaka hapana. Hizi Imani nyingi na za kisasa zinatoa kifo cha miungu na kufufuka kama *kielelezo,* ambacho msingi wake ulikuwa mzunguko wa mbegu ya wakati na mavuno, ya kukuza na kuongezeka kwa binadamu. . . . Ulimwengu wa Wayahudi ambako ndiko Ukristo ulikozaliwa ulishawishika kwa njia nyingi na ulimwengu mpana wa Wagiriki wa Roma. . . . Lakini, chakushangaza sana, hapakuwa na ishara ya kufa na kuinuka kwa miungu na mizuka kwenye ulimwengu wa Wayahudi. . . . Wakati Wakristo walipozungumzia kufufuka kwa Yesu hawakusema kuwa ni jambo linalotokea kila mwaka, kama la kupanda mbegu na kuvuna mazao. Wangeweza kutumia mfano wa kupanda na kuvuna kulizungumzia hili; wangeweza kusherehekea kifo cha Yesu kwa kuumega mkate; lakini kuchanganya hili na ulimwengu wa kufa na kuinuka miungu lingekuwa kosa kubwa." (Wright 2003: 80-81, fafanuzi imeongezwa; angalia pia McDowell na Wilson 1993: 167-88) C. S. Lewis anaongeza, "Simulizi zote za Wapagani ni kuhusu mmoja aliyekufa na kuinuka, labda kila mwaka, au vinginevyo hakuna ajuaye ni wapi na hakuna ajuaye ni lini. Simulizi za Wakristo ni kuhusu mtu wa Kihistoria, ambaye kuuawa kwake kwaweza kuandikwa kwa usahihi, chini ya iliyoitwa mahakama ya Kirumi, na ambaye jamii aliyoianzisha inaendelea na uhusiano hadi siku ya leo." (Lewis 1980: 83) Hata watawala wa kirumi waliokufa wakijiita miungu, au simulizi ambazo wanadamu kama Romulus walikuwa miungu, hawataweza kuwa chanzo cha kumwamini Yesu aliyefufuka, kwa sababu hizo simulizi na matangazo "hayakuhitaji kufufuka; yangetokea wakati wote bila hicho. Inahusisha nafsi siyo mwili." (Wright 2003: 83)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mengine yatakayoendana na ukweli huu. Kwa kuyaunganisha na haya, Timothy Keller anafanya uchunguzi mwingine muhimu kwamba "wengi wamegeuka kufikiria kama mtazamo wa ulimwengu ulivyo" (unaoamini kwenye uhakika wa kufufuliwa kwa mwili) "Kwa kawaida kulichukua miaka kujadiliwa na kuzozana kwenye majadiliano ya waandishi na wale waliotafakari . . . mpaka upande mmoja uliposhinda. Hivi ndivyo asili na mtazamo wa kidunia ulivyobadilishwa. Hata hivyo, mtazamo wa Wakristo kuhusu kufufuka, bila shaka unafanana na historia, ulichipuka na kwa ghafla ukaenea baada ya kifo cha Yesu. Hapakuwa na mpango wala mwendelezo. Wafuasi wake walisema Imani yao haiji kutokana na mazungumzo wala majadiliano. Waliwaeleza wengine kile walichokiona wenyewe. Hakuna hata mmoja aliyekuja na maelezo mbadala yaliyokubalika juu ya madai hayo." (Keller 2008: 209) Haikufanya hivyo kwa asili ya Ukristo kulihusisha mageuzi makubwa kwenye mtazamo wa kiwango cha kidunia, lakini kufufuka kulikuwa wazo kuu la mtazamo mpya wa kiulimwengu. Kama N. T. Wright anavyoeleza, "Hata pale ambapo kufufuka kulifundishwa kwa Wayahudi, ilikuwa mara kwa mara wasiwasi mkubwa, lakini kwa Ukristo wa kwanza ilikuwa ikiendelea kutoka kwenye mzunguko na kuwa kitovu." (Wright 2003: 477) Ukweli huu pia unahitaji maelezo ya kihistoria. Tena, maelezo pekee ya kukubalika ni kile alichokifanya Yesu, kwa kweli, kimwili alifufuka kutoka kwa wafu.

Mabadiliko haya ya ghafla na wazi ya Imani yanathibitishwa na upekee wa Imani, mwenendo na tabia za Wakristo, kuanzia mwanzo na kuendelea:

1. <u>Ibada ya Jumapili.</u> "Moja ya imani waliyoishikilia sana Wayahudi ni kuitimiza Sabato, na hata sasa Wakristo Wayahudi walibadili kuabudu kwao kutoka jumamosi na kuwa jumapili [**Matendo 20:7; 1 Wakor 16:2**], waliyoiita'Siku ya Bwana' [**Ufu 1:10;** *Didache* c.70-110: 14.1]. Ni kwa kuzingatia sana pekee kwaweza kuelezea mabadiliko haya: kusherehekea kwao kila juma kwa kufufuka."(Maier 1973: 122) James D. G. Dunn anaongeza, "Hakuna uthibitisho wa wazi kwa desturi kwamba Yesu kwanza alionekana*'siku ya kwanza ya juma'* (Jumapili) kufuatia kusulubiwa na kuzikwa kwake. . . . Wala hatutasahau kukamatwa kwake lakini mara chache ukweli uliodharauliwa kwamba ni kutoka mapema kama ambavyo tunaweza kufikia, Jumapili ilikuwa siku muhimu na maalumu kwa Wakristo, 'Siku ya Bwana', kifupi ni kwa sababu ndiyo siku ambayo walisherehekea kufufuka kwa Bwana." (Dunn 2003: 860) Kweli, mababa wa kwanza wa Kanisa Ignatius na Justin Martyr kwa kifupi waliitaja siku ya kufufuka kama msingi wa siku mpya ya kuabudu (Ignatius c.110d: 9.1; Justin Martyr c.155: 67).
2. <u>Ubatizo.</u> Ubatizo ulifanywa na Wayahudi wa kwanza kwa waongofu wapya kama ishara ya toba na utakaso ("Ubatizo" 1906; angalia **Math 3:1-6; Marko 1:4; Luka 3:3; Yohana 1:25-27**), maana yake kwa Ukristo ilibadilika moja kwa moja ikihusishwa na kufa na kufufuka kwa Yesu (**Warumi 6:3-5; Wakol 2:12**). Kanisa laweza kuhifadhi wazo la Wayahudi wa zamani la ubatizo, lakini halitawezakupuuza mabadiliko haya ya maana yalitokea mapema kwenye historia ya Kanisa.
3. <u>Ushirika (Meza ya Bwana).</u> **1 Wakor 11:23-26** inaleta jambo jingine kwenye mwanzo wa Imani linaloturudisha hadi mwanzoni mwa Ukristo mapema kati ya miaka ya -30, kwenye jambo hili hadi kwa Yesu mwenyewe (Jeremias 1966: 101, 104-05; Habermas 1984: 121). Kusherehekewa kwa meza ya Bwana kunatukumbusha kifo cha Yesu pale msalabani na kile alichokisema kwenye chakula cha jioni cha mwisho alichoshiriki na wanafunzi wake. Kama tulivyoona, Kwa vyovyote, ni kufufuka kunakoleta uthamani wa sadaka ya Yesu pale msalabani. Baadaye, **1 Wakor 11:26** anamalizia kwa kusema *"Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya <u>Bwana hata ajapo.</u>"* Huku ni kutambua kwamba Yesu yuko hai na atarudi.

Nadharia yoyote ya kile kilichotokea siku ya kwanza ya Pasaka asubuhi *kingine tofauti na kufufuka kwa mwili wa Kristo* "hakiwezi kutatua tatizo ambalo tunaliangalia: asili, ambayo ni Imani ya Kanisa la Kikristo kwenye muujiza wa kufufuka kwa Masihi" (Strauss 1865: 412).

### H. *Kushindwa kwa maelezo mengine*

Nadharia nyingi zilizoandaliwa kwa lengo la kuuondoa ukweli wa kufufuka (nadharia ya kuzimia; kuibiwa kwa mwili; Ubishi kwamba Yesu hakufa hivyo hakufufuka; kufufuka ni hadithi kama kufa na kuinuka miungu na mizimu ya ibada za kipagani) haya yamezungumzwa hapo juu. Mjadala mwingine sasa unaibuliwa.

1. <u>Kufufuka ni simulizi itakayoendelea baadaye.</u> Haya ni "maelezo toshelevu pekee" Mwanazuoni Kiislamu na mtafsiri wa Korani Mohamedi Asad anaweza kuja na maelezo haya **Q. 4:157** kuhusiana na kusulubiwa kwamba *"hawakumwua, wala kumsulubisha, lakini ilifanywa kuonekana nao."* Asad anaeleza, "Simulizi ya kusulubiwa kama ilivyoelezewa kwa kifupi kwenye Aya za Korani wa-lakin shubbiha lahum, inayomaanisha kama 'lakini ilifanywa kuonekana nao kama vile ilikuwa hivyo' – inaonyesha kwamba kwa muda, mrefu baada ya wakati wa Yesu, simulizi iliendelea kukua kwa kiasi (bila shaka chini ya ushawishi mkubwa wa Imani ya Mithraistic) kwa matokeo kwamba angekufa msalabani ili kuwa fidia kwa 'dhambi ya asili' ambayo kwayo mwanadamu anadaiwa kumtwisha; na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

simulizi hii kuimarishwa miongoni mwa wafuasi wa Yesu siku zilizofuata kwamba hata maadui zake, Wayahudi walianza kuiamini – ingawa kwenye hali ya upinzani (Kwa kuwa kusulubiwa wakati huo ilikuwa ni adhabu ya kifo inayowastahili wahalifu wa sheria). Kwa ufahamu wangu ndiyo maelezo toshelevu kwa aya hii wa-lakin shubbiha lahum, kwa maelezo ya kama hayo shubbiha li ni sawa na khuyyila 1i, '[kitu] ilikuwa sura ya kikaragosi kwangu', i.e., 'kwenye ufahamu wangu' – kwa maneno mengine, '[kitu] ilionekana kwangu.'" (Asad 1980: Q. 4:157n.171) Nadhari ya "simulizi" ya Asad inajielekeza moja kwa moja kwenye suala la kusulubiwa lakini kwa umuhimu yaweza vile vile kuwa ya kufufuka kwa kuwa vyote viwili vinategemeana.

Yapata miaka 200 iliyopita Julius Müller alionyesha jambo muhimu kwamba inahitaji muda wa kutosha kwa mwandishi wa simulizi kuendeleza kuhusiana na watu, historia na matukio, hasa pale ambapo vyanzo vya msingi na mashahidi walioona wakiwepo bado. Müller aliandika: "Wengi wameamua ni lazima muda wa kutosha upatikane ili kukamilisha mageuzi ya historia yote kwa desturi, wakati simulizi nyingi zinapoandaliwa kwenye utawala uleule mahali ambapo mashujaa walikulia na kuandaliwa. Hapana mtu ambaye hatafikiri ni jinsi gani simulizi hizo zitakavyoinuka kwenye mwaka wa historia, kujipatia heshima kubwa kote, na kusisitiza kumbukumbu za kihistoria, tabia ya kweli na mahusiano ya maisha ya mashujaa kwenye ufahamu wa jamii, ikiwa bado mashahidi wa tukio hilo wapo hai, ni nani atakayekuwa na shaka juu ya ukweli wa matukio yaliyowekwa kwenye kumbukumbu. Wakati huo huo, simulizi zisizo za kweli, kama hazipendi wakati wa sasa wa wazi, lakini hupenda giza la ajabu la kale la kijivu, hutaka kutafuta upotevu wa umri, pamoja na nafasi, na kuupoteza ujasiri wao na mara chache viumbe wa ajabu kwenye maeneo na nchi isiyojulikana." (Müller 1844: 26, imenukuliwa kwa Craig 1981: 101)

Kwa kuheshimu madai ya Agano Jipya kwamba Yesu alifufuka, hali iko wazi na thabiti. "Injili zote nne (i.e., Mathayo, Marko, Luka/Matendo, Yohana) ziliandikwa wakati wa karne ya kwanza. Kila Injili inaonyesha kufufuka kwa Yesu, na Matendo ya Mitume ni mwendelezo wa Injili ya tatu, Luka. Hili inamaanisha kwamba injili zote nne ziliandikwa ndani ya miaka sabini baada ya Yesu, zikitaarifu madai ya wanafunzi kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu." (Habermas na Licona 2004: 53) Nyongeza, Tunayo barua ya Paulo kwa Warumi, Wakoritho wa 1 na 2 , wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, Wathesalonike wa kwanza, 2 Timotheo, na Waraka wa kwanza wa Petro, zote kwa pamoja zinazungumzia kufufuka. Nyaraka hizo ni muhimu na kwamba wote wawili Paulo na Petro waliuawa kati ya miaka ya-60 AD, ikimaanisha kwamba nyaraka zao ziliandikwa kati ya miaka 20-30 baada ya kufufuka kwenyewe. Walikuwa pia mashahidi wa kuonekana kwa Yesu baada ya ufufuo. Zaidi, kama tulivyosema hapo juu, baadhi ya nyaraka za Paulo zimebeba Imani ya awali ambayo iliandikwa kabla ya kuandikwa kwa nyaraka za Paulo na kuturudisha hadi kwenye mambo muhimu ya Ufufuo wenyewe.

Umuhimu wa maelezo haya mengi ya awali ni kwamba hayana muda wa "simulizi" za kufufuka kuendelezwa. Msomi wa Greco-Roman A. N. Sherwin-White anaeleza, "Herodotus anatuwezesha kuonja mdundo wa wasimulizi, na kuonja mwendelezo kwamba hata vizazi viwili ni muda mfupi sana wa maisha kuruhusu tabia ya kihistoria kushinda kwenye msingi wa historia ya mila ya midomo" (Sherwin-White 1992: 189-90). Craig anahitimisha, "Müller anawapa changamoto wasomi wa wakati wake kutafuta hata mfano mmoja wa kihistoria ambao kwa miaka thelathini kulikuwa na mfululizo mkubwa wa simulizi, vipengele vya tabia nyingi ambazo ni mali ya uongo, ambavyo vilikusanywa karibu na mambo muhimu ya kihistoria na kuimarishwa kwenye Imani ya jumla. Changamoto yake haikufikiwa hata leo. Urefu wa muda ni muhimu ukusanyaji wa simulizi kuhusiana na matukio ya injili utatuweka kwenye karne ya pili A.D., wakati ambao injili ya hadithi ya Apocrypha ilipozaliwa." (Craig 1981: 101-02)

2. <u>Maelezo ya Kisaikolojia.</u> Haikubaliki kung'ang'ania kwamba madai ya wanafunzi ya kufufuka kwa Yesu kama ni majibu ya kisaikolojia kwa kifo chake. Wazo la kwamba Petro, Yakobo, na wengine "Lilisababishwa na hali ya huzuni waliyokuwa nayo . . . haina msingi wowote wa ushahidi" (Wright 2003: 20). Yayo hayo yangefanyika kwamba Paulo alianza kueneza habari za kufufuka kwasababu alihukumiwa na dhamiri juu ya mateso yake kwa Wakristo. Siyo tu kwamba hakuna ushahidi wowote juu ya hili, lakini ukweli ni kwamba Paulo alikuwa na juhudi nyingi za kuendelea kuwatesa Wakristo mpaka wakati ule alipokutana na Yesu mfufuka.

Zaidi, hakuna mwanafunzi ambaye kisaikolojia alikuwa amejiandaa kuamini kwenye kufufuka kwa Yesu, kwa sababu hakuna hata mmoja aliyetarajia au kulitazamia jambo hilo. Kweli, "'kufufuka' siyo jambo ambalo *mtu yeyote* alilitarajia kutokea kwa mtu mmoja wakati ambao ulimwengu ulikuwa ukiendelea na mambo yake kawaida. Ukweli—wazo hili mara nyingi lilipuuzwa na maadui—Wanafunzi hawakutarajia jambo kama hilo kutokea kwa Yesu." (Wright 2003: 689, fafanuzi

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

imeongezwa) Kwenye karne ya kwanza kulikuwepo na vuguvugu lingine la Masihi ambalo viongozi wake waliuawa na wenye mamlaka. "Hapakusikika hata kidogo kwamba yupo mmoja wa wafuasi aliyekuwa amevunjika moyo na kudai kwamba shujaa wao alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Walijua vizuri. 'Kufufuka' halikuwa tukio la siri. . . . Mwanamageuzi wa Kiyahudi ambaye kiongozi wake aliuawa na wenye mamlaka, na ambaye alifanikiwa kutoroka kukamatwa yeye mwenyewe, alikuwa na chaguzi mbili: kuachana na mageuzi au kumtafuta kiongozi mwingine. Tunao ushahidi wa watu waliofanya yote mawili. Kudai kwamba kiongozi wao halisi alikuwa hai tena halikuwa chaguo. Vinginevyo, bila shaka, alikuwa." (Wright 1993: 63)

3. <u>Kufufuka kwa Yesu ni kwa"kiroho tu"</u> Kwa karne ya kwanza, Mazishi ya Wayahudi yalikuwa kwenye ngazi mbili: Kwanza, mwili ulilazwa kwenye sakafu, kuzungushiwa kitambaa cha nguo na kuwekwa kwenye pango kama kaburi na kuwekewa jiwe kama mlango unaoweza kuondolewa (kama kaburi la Yusufu wa Arimataya ambalo Yesu alilazwa); pili, kwa mwaka mmoja au zaidi, baada ya mwili kuoza, ndugu au marafiki wangerudi, kukusanya mifupa na kuiweka kwenye kisanduku (kisanduku cha mifupa). "Kama wanafunzi wangeamini kwamba kile walichokiita 'kufufuka' lilikuwa tukio la 'kiroho', kuuacha mwili kwenye kaburi, mapema au baadaye mtu angeenda kuikusanya mifupa ya Yesu na kuihifadhi vizuri. . . . Lakini bila shaka, kama kwa hatua yeyote mtu angerudi kuikusanya mifupa ya Yesu na kuiweka kwenye kisanduku, hilo kwa kweli lingeuangamiza Ukristo hata kabla ya kuanza vizuri." (Wright 1998: 52)

Yesu mwenyewe alikuwa na wazo hilo kwamba ni Roho alipokutana na wanafunzi wake wakamshika na kumgusa alipokuwa akila na kunywa pamoja nao (**Matt 28:9; Luka 24:36-43; Yohana 20:15-17**, **24-29; 21:9-14**). Kwa kweli, kila mmoja aliyesikia madai hayo ya kufufuka alijua kwamba kile kilichodaiwa ni kufufuka kwa *mwili* (kwamba hili, baada ya yote, ndiyo maana ya kufufuka").[23] Hili lisingekuwa hivyo, Viongozi wa Wayahudi wasingetengeneza habari ya uongo kwamba mwili umeibiwa lakini wenyewe wangeenda kaburini na kuutoa mwili.

4. <u>Wanafunzi waliota ndoto au waliona maono.</u> "Palitakiwa kuwa na mkusanyiko wa ndoto/maono ya makundi yasiyopungua mia tano kwa ukubwa, wote kwa pamoja waone kitu kile kile—umuhimu usiowezekana kwa jambo au tukio ambalo kimsingi ni la kibinafsi. Watu wengi tofauti *wasingeweza* kuona jambo lile lile kwenye maeneo tofauti kwa ndoto ya kawaida, maono, au tukio linalowahusisha watu au makundi mengi. Maono hayo, Zaidi sana, hutukia pale tu ambapo wapokeaji huwa kwenye hali ya matarajio makubwa na matumaini ya kuona taraja lao linatimizwa, hali ambayo inapingana kabisa na ile ya wanafunzi, ambao walikuwa wamekosa tumaini na kugubikwa na huzuni na kuvunjika moyo. Kwa kweli, habari za kufufuka karibu zililazimishwa kwao kukutana na hali ya wazi ya kutokuamini kwao." (Craig 1981: 113) Kama George Eldon Ladd alivyofupisha, *"Imani haikuumba kuonekana; kuonekana kuliumba imani"* (Ladd 1975: 138, fafanuzi imeongezwa).

Watu wa zamani na wale wa ulimwengu wa sasa walikuwa na maono ya kufiwa na wapendwa wao. Hata hivyo, kama N. T. Wright anavyoonyesha, maono hayo ni hali *isiyojitosheleza* kabisa kwa Imani ya wakristo wa kwanza. Kwa jinsi yalivyo ya 'Kawaaida' haya 'maono' ndivyo yanavyoendelea kupoteza uhalisia, bila kujali ni kwa jinsi gani utambuzi umeharibika au watakavyojisikia, wangesema kile ambacho hakuna mtu angekisema kuhusiana na mtu aliyekufa kabla, kwamba wangekuwa *wamefufuliwa* kutoka kwa wafu. Kwa kweli, maono haya yalikuwa na yalimaanisha kwa uhakika, kama watu wa zamani na wa ulimwengu wa sasa walivyogundua, kwamba mtu alikuwa amekufa, siyo kwamba alikuwa hai." (Wright 2003: 690-91, fafanuzi imeongezwa)

Hatimaye, "Kuonekana kwa Yesu aliyefufuka kulikuwa na hitimisho la muda; wakati Paulo alipomwona Yesu, huo ulikuwa ni mwisho wa mfululizo huo wa kuonekana kwake [**1 Wakor 15:8**]." (Wright 2003: 318) William Lane Craig anaonyesha kwamba, tofauti na kuonekana kwake halisi kimwili baada ya Kristo mfufuka ambako kuliishia muda siyo mwingi baada ya kufufuka, "ndoto

[23] N. T. Wright anathibitisha kwamba watu wote wa karne ya kwanza (Wapagani, Wayahudi, na Wakristo) walijua kwamba "kufufuka" kulimaanisha "maisha mapya baada ya kufa kwa muda. Wapagani walikataa uwezekano huo; baadhi ya Wayahudi walithibitisha hili kama tumaini la muda mrefu ujao; Wakristo wote walidai kuwa ilitokea kwa Yesu na itawatokea wao baadaye. Wote walizungumzia . . . kuishi upya kimwili kufuatia kipindi cha kufa kama mwanzo (kipindi ambacho mtu anaweza au asiweze kuwa'hai' kwenye aina nyingine isiyokuwa na mwili). Hakuna hata mmoja (isipokuwa Wakristo, kwa kumheshimu Yesu) wanaofikiri kwamba hili lilikwishatokea, hata kwenye hali ya kutengwa." (Wright 2003: 31) Zaidi, maneno la kigiriki *egeiro* na *anastasis*, ambayo yanatafsiriwa moja kwa moja kama "kufufuka" kwenye Biblia na kwingineko, "ni maneno ambayo wakati wote hutumika kuzungumzia kitu fulani maalum kukiainisha kutoka kwenye kuishi kimwili, kikijulikana, kurudi kwenye maisha ya kimwili. Hakuna uthibitisho wa maneno hayo kutumika kwa kuwakilisha kitu kisicho na mwili kuishi baada ya kifo." (Ibid.: 330)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

zaweza kundelea kwa miongo mingi, na hata karne. Walioendelea kuona au kuota au kuwa na maono wangeendelea." (Craig 1981: 113) Wazo kwamba wanafunzi walikuwa na njozi, maono au aina Fulani ya "uzoefu wa kidini" badala ya uhalisia wa kumwona Yesu aliyefufuka, kuna ukataa ukweli wa mashahidi waliokuwepo wakati wa tukio na kushuhudia kilichotokea.

5. Mwili ulichukuliwa au kuondolewa. Kama tulivyozungumzia hapo nyuma, mwitikio wa kwanza kwa tangazo kwamba Yesu alifufuka ulidaiwa na viongozi wa Kiyahudi kwamba wanafunzi waliuiba mwili. Maier anakumbusha, "Nadharia ya mwili kuibiwa inaanzishwa na vikwazo viwili visivyowezekana: tatizo la kimalengo na tatizo la kuuawa. Kuandaa mbinu ya kuvunja kaburi lililo na ulinzi mkali kulihitaji nguvu ya ziada na uthubutu wa hali ya juu wa kundi la watu wenye ujuzi mkubwa. Lakini ni nani aliyekuwa na hizo sababu? Ni nani aliyekuwa na msukumo na ujasiri wa lazima kufanya hayo yatokee? Kwa kweli siyo wanafunzi ambao tayari walikuwa wamevunjika moyo, waliokusanyika na kujificha kwa kukosa tumaini kwa ushahidi wa kushindwa kwa Yesu na hofu ya wenye mamlaka wa hekalu—kundi la watunga hila walikuwa wakikazana kuwapofusha wakaaji wa nchi yote." (Maier 1973: 109) Maier anaendelea kuonyesha, "Lakini hata kama wanafunzi walikuwa na nguvu kubwa na msukumo wa kuweza kuuiba mwili na tena— wakiwa na mashaka tele—kutangaza kufufuka, ni jinsi gani wangekuwa na tumaini la kukamilisha jambo hilo? Eneo la kaburi lilikuwa limezungukwa na walinzi waliokuwa wamepewa maelekezo ya kuzuia jaribio la aina yoyote. . . . Walinzi wa wakati wa zamani walikuwa wakilala kwa zamu, hivyo ilikuwa ni vigumu sana kwa upande wa wavamizi kuweza kuwafikia wote wakiwa wamelala, kama ambavyo wakati mwingine ilidaiwa. Vurugu ambazo zingesababishwa na kuvunja mihuri, kuliviringisha jiwe ili kufungua kaburi, kuingia kaburini, na kuuchuka mwili kungewaamsha walinzi hata kama wote walikuwa wamelala." (Ibid.: 110-11)

Nyongeza, James Dunn anaangalia kwamba kutokuabudiwa kwa kaburi la Yesu siyo tu kwamba ni ushahidi wa kufufuka lakini pia ni ushahidi kinyume na wazo la kwamba wanafunzi waliuiba mwili: "Kwa kuwa kama kweli wanafunzi waliuondoa mwili, ni jambao la kutofikirika kwamba wasingeenda kuulaza mwili kwa heshima kupumzika mahali penginepo. Kwa jambo lipi, ni lisilofikirika kwamba kuabudu kwa siri kusingeweza kuendelea kwa kitambo kirefu kwa wale ambao tayari walielewa na kwamba baadhi ya mawazo yasingeweza kuwafikia wanafunzi wote." (Dunn 2003: 838) Wazo la kwamba mtu aliuondoa mwili halipambani siyo tu na "tatizo la nia na tatizo la kuuawa," lakini ni kinyume na muhuri wa Kirumi kwenye kaburi na walinzi. Na haipo kwenye nyaraka zilizo hifadhiwa kuhusiana na kufufuka na kuonekana kwa Yesu. Kama zilivyo nadharia nyingine, hakuna kumbukumbu ya ushahidi wa kihistoria kwamba mtu aliuondoa mwili wa Yesu. Hivyo, kama ilivyo kile kilichoitwa maelezo mengine, wazo kwamba kitu Fulani kilitokea kwa mwili wa Yesu *tofauti na kufufuka kwa mwili wake* hakitaendana na ukweli wa historia uliopo.

## I. *Hitimisho*

Kwamba Yesu alisulubiwa na kufufuliwa kwa mwili kunaweza kuthibitishwa na uchunguzi wa kihistoria sawa sawa na matukio mengine ya kihistoria. Kutangaza maelezo mbadala haimaanishi kuyajengea msingi maelezo hayo. Kama tulivyoona, kile kinachoitwa maelezo mbadala ya kusulubiwa na kufufuka yamesimamia mahali ambapo hapana ushahidi wowote wala hayana kumbukumbu zozote za kihistoria, au yanajikanganya na kumbukumbu za historia. Sababu za kwanini maelezo mbadala yamekuwa yakiendelezwa ni kwa yenyewe kutokuwa na mtiririko wa ushahidi lakini yakiwa na ushindani wa sababu za kifalsafa na kitheolojia zisizo na uthibitisho. Kusudi la hili ni kwamba ushahidi wenyewe unajitosheleza na kwamba mwenye maelezo mbadala hataki kukubali kwamba Yesu kweli ni mwana wa Mungu. Hata hivyo, kuyaaminisha maelezo yoyote ya kiufahamu au kitheolojia yaweze kukubalika, haitoshi kuumaliza ukweli wa kufufuka kwa Yesu kwa kutangaza tu kwamba "halikufanyika (au halitafanyika) wala kutokea." Hata Korani inasema kwamba ni lazima mtu aangalie ushahidi ili awe na sababu ya kuutumia. Kwa kifupi, ni lazima kukabiliana na kujibu maswali mengi ya kihistoria: "Kwanini Ukristo uliendelea kwa haraka sana, ni kwa nguvu ipi? Hapana kundi jingine la wafuasi wa Masihi kwa kipindi hicho waliokuwa wamedai kuwa kiongozi wao alifufuka kutoka kwa wafu—kwanini makundi hayo yalifanya hivyo? Hakuna kundi lolote la Wayahudi waliowahi kumwabudu mwanadamu kama Mungu. Nini kilichowaongoza kufanya hicho? Wayahudi hawaamini mwanadamu wa Kiungu au kufufuka kwa mtu biafsi. Ni nini kilichobadilisha mtazamo wao wenye misingi ya kidunia kama kwa usiku mmoja? Unayachukulia vipi maelezo ya mamia ya mashahidi waliokuwepo kwenye ufufuo ambao waliishi kwa miongo kadhaa na umma ukaukubali ushuhuda wao, hatimaye waliyatoa maisha yao kwa kile walichokiamini?" (Keller 2008: 210)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

## VI. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Yesu ni "Mwana wa Mungu"

Waislamu wanaposikia neno "Mwana wa Mungu," wengi humdhania Allah kujamiiana na Mariamu, jambo ambalo (na Wakristo) kwa kweli ni mtazamo ambao siyo wa kweli na hata ni kufuru. Kwenye maeneo mengine, Biblia inamwita Yesu *"mwana pekee"* Mwana wa Baba (angalia **Yohana 1:14, 18; 3:16, 18; 1 Yohana 4:9**). Korani inasema, *"Haikubaliki kwa utukufu wa Allah kwamba aweza kuzaa [au 'kujitwalia']mwana"* (**Q. 19:35;** angalia pia **Q. 2:116; 10:68; 18:4; 19:88, 92; 23:91; 39:4; 112:3**) Yusuf Ali anatamka mashaka ya Waislamu: "Kuzaa mtoto ni kitendo cha kimwili kinachotegemeana na uhitaji wa asili wa wanadamu au wanyama. Allah Mkuu anajitegemea kwa mahitaji yote, na ni matusi kwake kumhusisha na tendo hilo. Ni sehemu ya masalia ya upagani kiganga/kichawi." (Ali 2006: Q. 19:35n.2487; angalia pia ibid.: Q.72:3n.; Deedat 2002: 29) Wazo hili linathibitishwa na Korani kwa kusema, *"Ni kwa jinsi gani anaweza kuwa na mtoto wakati hamna mwenzi"* (**Q. 6:101**; angalia pia **Q. 72:3**).[24] Hata hivyo, wakati Biblia inapomwelezea Yesu kama "Mwana wa Mungu," haimaanishi *hata kidogo* au kuhusisha mchakato wa kimwili wa kutunga mimba na kuzaa mtoto zaidi ya wale Wamisri waliojiita wenyewe"wana wa Naili" wakimaanisha kwamba Naili aliolewa na kuwa na watoto (Michael na McAlister 2010: 145). Badala yake, "maelezo'Mwana wa Mungu' ni msemo wa fumbo"kuuelezea uhusiano wa Yesu na Mungu Baba (Ibid.; angalia pia Feinberg 2001: 492 ["Maandiko yanamzungumzia Kristo kama Mwana, lakini kila mmoja amekubali kuwa ni lazima awe Mwana kwa jinsi ya fumbo"]; Lewis 1967a: 137).

Kwa nyongeza, John Gilchrist anaangalia kwamba upinzani wa Kiislamu kwa Yesu kama "Mwana wa Mungu" haukuwasumbua waumini wa Kikristo kwenye kuuelewa msemo huo: "Hakuna mahali popote kitabu kinapoonyesha uelewa wa msingi wa Imani ya Kikristo kwa Yesu, kwamba alikuwa mfano wa Uungu, ambaye hakuumbwa wakati wowote, aliyekuwa na Baba tokea mwanzo, aliyechukua umbo la mwanadamu *na kuwa* mtu Yesu. Korani inakwepa yote haya kwa maelezo mbadala ya Arian [kuhusiana na kutokuamini kwa Arias (AD 256-336)], kwa kusema kwamba mwana aliletwa Duniani wakati fulani. Arius anafundisha kwamba 'kuna wakati ambao Mwana wa Mungu hakuwepo' na kwamba Mungu pekee baadaye *alijitwalia* Mwana ambaye *alimuumba* kama kielelezo cha Kimungu kinachojitegemea. Ni kwa kanuni hii Korani wakati wote (na bila kuruhusu) inashambulia." (Gilchrist 2015: 101)[25]

---

[24] Reynolds anaangalia, "Kirahisi njia ambazo Korani inazitumia kuhoji, maneno ya wazi (Mungu hana mwenzi; hajamiiani na hawezi kuwa na mtoto; cf 72:3) inaeleza labda ni kutokuyaelewa mafumbo ya Biblia juu ya wana wa Mungu au (yakufanana zaidi) majadiliano ya majani-mtu." (Reynolds 2018: 237)

Baadhi wa wanazuoni wa Kiislamu wanakiri kwamba matumizi ya neno "mzaliwa" kwenye tafsiri ya baadhi ya vifungu vya Korani siyo sahihi. Kwa mfano, Muislam Tiger Chan anazungumzia tafsiri ya Korani ambayo inatafsiri kwa makosa neno *ittakhadha kama* "mzaliwa" badala ya "kuchukuliwa" (e.g.,tafsiri ya Yusuf Ali ya **Q. 2:116** [*"wanasema: 'Allah amezaa mtoto'"*] na **Q. 19:88** [*"Wanasema: '(Allah) Mwenye utukufu wote amezaa mtoto!'"*]). Chan anasema kwamba kuna msingi wa lugha kwa *ittakhadha* kumaanisha "kuzaa" na kuhitimisha, "Msitari wa mwisho ni huu, Korani haifundishi kwamba Wakristo wanaamini kwamba Yesu ni mtoto wa kuzaliwa na Mungu" (Chan 2003: n.p.; angalia pia "Kamusi ya Korani" 2009-2017: Q. 19:88, *ittakhadha*) Hata hivyo, hata tafsiri sahihi ya"kuchukuliwa" haisuluhishi suala hili kwa sababu, kama Chan alivyoeleza, "Kama tukisoma vile vitabu vya Wakristo vya kitheolojia vinachosema, inasema kwamba Wakristo hawaamini kwamba Mungu alizaa mtoto halisi kimwili. . . . Fundisho la utatu lina watu 3 Utatu wa Mungu ni huu, Mungu Baba, Mungu mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Watu 3 kwenye utatu wako sawa kwenye nafsi na uwezo. Mungu Baba 'alimchukua' Yesu kama'mwana', ndiyo maana Yesu anaitwa Mwana, Mungu Baba anaitwa Baba. Huu ni uhusiano wa Kiungu unaoitwa ('kuchukuliwa') watu watatu kama Baba, Mwana na Roho mMtakatifu. Kwenye mtazamo wa Kikorani, neno '*ittakhaza*' [**Q. 19:88**], *"Na wanasema: Allah mkarimu amejitwalia (kwa ajili yake) mwana"* (Shakir)] inatuonyesha kwamba hakuna jambo kama hilo la Mungu kujichukulia chochote kama kuwa na hali ya Uana. Aya ya Korani 19:88 inakataa fundisho hilo kama fundisho la Utatu. Inakataa aina yoyote ya Uana. Biblia haisemi kwamba Wakristo wanaamini Yesu kama mwana wa kimwili wa Mungu, inakataa kila maandishi yanayozungumzia Uana wa Mungu." (Chan 2003: n.p.) Hata hapa, Chan na Korani hawako sahihi: Waumini wa Ukristo *wakati wote* wanachukulia kwamba Baba "hakumchukulia" Kristo kama Mwana, lakini Kristo wakati wote na kwenye umilele amekuwa Mwana,Mtu wa pili kwenye Utatu.

[25] Abd al-Fadi anaongeza, "Bila shaka neno 'Mwana' linawatatiza watu wengi, kwa sababu linajitokeza mara, kupitia uhusiano wake na neno 'Baba', kwamba Baba alimleta Mwana kwa wakati, kwa hiyo ni lazima iwepo tofauti ya muda na hali kati yao" (al-Fadi 2003: 20). Wazo hili siyo sahihi. Kulingana na Biblia, "Mungu, tokea mwanzo, alikuwa na cheo cha Baba, hivyo hili linaonyesha uwepo wa Mwana tokea mwanzo pia. . . .Hakuna atakayeitwa baba hadi hapo Mwana atakapokuwepo. Wakati tofauti, kwenye jambo hili, ni la kufikirika na kuaminika bila ushahidi kuhusiana na Mungu na Mwanae Yesu Kristo. . . . Tuna tumia neno Mwana wa kweli au Mwana wa Nuru kuonyesha uhusiano kati yao na Kweli au Nuru. Kwa njia hii, Yesu anaitwa Mwana wa Mungu, kwa sababu ya ukamilifu wa kufanana kati yao Baba na Mwana kwenye Mungu mmoja. Yesu amekuwa akiitwa hivyo kwa sababu ni wa pekee mkamilifu na ufunuo wa milele wa utu wa Mungu kwenye ubinadamu, au , kama tunavyosoma kwa Waebrania 1:1-2, Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu kupitia manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi kupitia Mwana, aliyemweka

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Pingamizi hili la Kiislamu pia linadumu kwenye kutokujua tafsiri ya neno *"mzaliwa pekee."* Maandiko yote kwenye Biblia yanayozungumzia kumhusu Kristo kama *"mzaliwa pekee"* Mwana (**Yohana 1:14, 18; 3:16, 18; 1 Yohana 4:9**) inamaanisha asili yake ya *umilele*, siyo wakati alipokuja kimwili kama mwanadamu. Neno la Kigiriki ni *monogenēs*. Wakati wengine (hasa wazee) tafsiri ya Biblia humaanisha kama *"mzaliwa pekee,"* maana halisi ya neno ni "mmoja pekee wa aina yake au kundi, *upekee (wa aina)*" (Danker 2000: *monogenēs*, 658, fafanuzi imeongezwa). Kuthibitisha kwamba hii ndiyo maana halisi ya *monogenēs* ni kuangalia **Waeb 11:17** Pale Isaka alipoitwa *mwana pekee* wa Ibrahimu. Isaka hakuwa "mzaliwa pekee" kwa Ibrahimu kwa sababu Ibrahimu pia alikuwa na baba wa Ishmaeli. John Feinberg anaeleza, "Neno ni hili Isaka alikuwa mtoto wa kipekee kwa Ibrahimu. . . . Ingawa Ibrahimu alikuwa na mwana mwingine, Isaka yeye alikuwa wa pekee, na yeye pekee ndiye aliyekuwa mwana wa ahadi." (Feinberg 2001: 491) Linapotumiwa na Kristo, *mzaliwa pekee* ni "maelezo ya aina ya Uana ambao Yesu alikuwa nao na siyo mchakato wa kuunda uhusiano huo" (Zodhiates 1992: *monogenēs*, 996).

Kunayo mistari mingine mitatu kwenye Biblia inayomzungumzia Yesu kama "Mzaliwa": **Matendo 13:33; Waeb 1:5; 5:5**.[26] Kila mmoja umenukuliwa kwenye **Zab 2:7** ("*Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.*") na inamzungumzia Yesu. Jochen Katz anaeleza kwamba, kwa mazingira yao, "Mistari yote hiyo inazungumzia **kufufuka na kuinuliwa** kwa Kristo. Inamzungumzia kwenye hali ya kuichukua Ofisi kama Mfalme na Kuhani. Hili lilitokea kama miaka 33 **baada** ya kuzaliwa kwa Yesu. Ni wazi, kwenye matumizi ya Biblia, neno 'mzaliwa' linapotumiwa kwa Yesu kwenye mistari hiyo **halihusishwi** na chochote kama kujamiina lakini lina maana ya fumbo. Maelezo ya 'Mwana pekee' wa Mungu halikutajwa kwa ajili ya muujiza wa jinsi alivyochukuliwa mimba kwa Roho mtakatifu au kwa kuzaliwa kwake na Bikira Maria. . . . Biblia inamaanisha nini basi? Ninafikiri **Warumi 1:4** inalisema hili wazi Zaidi kwamba 'ni kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu.' Kufufuka kulikuwa ni wakati wa tangazo kwa umma wa kile kilichokuwa kinasubiriwa kwa muda mrefu. . . . Zaburi ya 2 ni zaburi ya uzinduzi wa wafalme wa Waisraeli – tangazo kwa umma la kifalme. Na wafalme wengi walitawazwa kuwa wafalme wakiwa watu wazima. **Hakuna hata mmoja** aliyekufa mfalme wakati anatungwa mimba. Maana hiyohiyo inaendelea hadi kwenye Agano Jipya na kutumika kwa Yesu kama na wale wengine, kwamba kufufuka ni tangazo la Mungu kwa umma kuhusu utambulisho wa kweli na mamlaka ya Yesu, Masihi, mfalme wa kweli wa Israeli, mwakilishi wa Mungu katikati ya wanadamu." (Katz, "Wewe ni"n.d.: n.p., fafanuzi iliyokolezwa rangi kwenye asili; angalia pia Guthrie 2007: 927-28)[27]

---

kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu." (Ibid.: 21) McDowell na Larson wanatoa maoni ya kufanana, "Baadhi ya watu, hutumia ukweli kwamba Yesu ni Mwana, wanaweza kusema, 'Ulishawahi kumsikia mwana asiye na mwanzo?' Kwenye hili wanamaanisha wanawatofautisha Mwana 'aliyeumbwa' na Baba asiyeumbwa. Kwa sababu hiyo, swali laweza kujirudia, 'Ulishawahi kumsikia Baba asiye na mwanzo?' . . . Ni wazi kwamba . . . kama Baba ni wa Umilele, ndivyo na mwana." (McDowell na Larson 1983: 75) Kwa kweli, neno "baba" ni "neno la uhusiano na halina maana nyingine yoyote isipokuwa kwenye uhusiano wa mtu ambaye ni Baba. Hivyo kwa njia nyingine utambulisho wa kuwa Baba unamtegemea Mwana , na vinginevyo." (Pannenberg 1991: 57)

[26] Kwenye maelezo ya Luka ya ubatizo wa Yesu, **Luka 3:22** yanahitimisha na sauti kutoka mbinguni ikisema, *"Wewe ni Mwanangu Mpendwa, Ninayependezwa nawe."* Kwenye maandiko mengine juu ya mstari huu baadhi ya maandishi ya zamani yanahitimisha kwa kusema *"Mimi leo nimekuzaa."* Muislam Jerald Dirks anadai kwamba haya maandiko tofauti yanathibitisha kwamba "ulikuwa ni Uana wa kutengenezwa', ambao ilianza tu baada ya Allah kutoa uhusiano maalum baina yake na Yesu, wakati wa kubatizwa kwake" (Dirks 2008: 69). Huu siyo ukweli. Kuacha ukweli kwamba mengi ya maadiko ya zamani matumizi ya lugha ya "ninapendezwa nawe", ukweli ni kwamba Luka anatumia lugha ya "Uana" kwenye mtazamo mwingine wa maisha ya Yesu, akijumuisha na wazo la kuzaliwa (**Luka 1:30-35**), kubatizwa (**Luka 3:21-22**), na kufufuka (**Luka 24:6-7**). Kama tunadhani kwamba lugha ya "mzaliwa" ya **Luka 3:22** ni maandiko sahihi, "kitendo cha kuzaliwa kwenye mazingira haya maalum hayazungumzii/taji wakati ambao Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Badala yake, Hii ni njia ya Luka kuonyesha wakati ambao Mungu aliuchagua kwa Yesu kuanza kuitumikia ofisi yake Masihi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu." (Shamoun, "Jesus Christ" n.d.: n.p.) Zaidi, maandiko haya "hayafanyi chochote kupingana na ushuhuda wa wazi wa Luka na Matendo kwamba Kristo ni Mungu kamili – na kwa hiyo ni wa milelel – ambaye alikuja duniani kutoka mbinguni kuwa mwanadamu kupitia kwa mbarikiwa Bikira Mariamu" (Ibid.).

[27] Imani ya Nikea (AD 325) inajumuisha maneno, "Ninamwaamini . . . Bwana mmoja Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu, mzaliwa wa Baba kabla ya ulimwengu wote; Mungu wa Mungu, Nuru ya Nuru, Mungu kamili wa Mungu kamili; aliyezaliwa, siyo kufanywa, kuwa kiini kimoja na Baba." Kwenye Imani, neno "mzaliwa" kwa wazi limetumiwa kwa njia maalum, kinyume na matumizi ya kawaida ya neno, hasa *kupingana* na wazo kwamba Kristo aliumbwa ao kutengenezwa kwa wakati. Hili halikufanyika kiholela, lakini "kulikuwa [sic.] na msingi wa kuhalalisha kukinga neno *mzaliwa* kwa sifa/kustahili 'siyo kufanywa'"—hasa hasa, kwamba wakati Agano Jipya linapotumia lugha ya "mzaliwa" kumhusu Kristo pia huelezea Uungu wake, na "na kanisa linapingana na kuliweka andiko moja kupingana na jingine" (Sproul 1992: 88). Kwamba hii ni njia sahihi ya kulifikia andiko.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Neno "Mwana wa Mungu" linadhihirisha ndani kuwa Yesu ni nani.[28] "Waislamu wanaelewa vema kuwa inamaanisha nini kwa Yesu kuitwa Mwana wa Mungu: Ni Mungu katika mwili," na "Waislamu wengi hawafikirii kwamba Wakristo wanaamini kwamba Mungu alikuwa na mahusiano ya wanandoa na Mariamu" (Carlton 2011: 13, 14). Kweli zifuatazo kwenye Biblia zinaonyesha msingi wa maneno na matendo ya Yesu mwenyewe, yakionyesha jinsi Yesu alivyoielezea nafasi yake kufunua kwamba alikuwa na ni wa *kipekee*, Mwana wa Mungu wa Mbinguni (kwa muhustasari wa ushahidi wa Kibiblia kwa Uungu wa Kristo angalia Brown 2002: 20-27):

**A.** ***Yesu alikuwa Mungu kamili: mwasisi na mtenda miujiza***

Tofauti na mwanadamu yeyote aliyepata kuishi, Yesu kwa nguvu ya Roho Mtakatifu alitungwa mimba na kuzaliwa na Bikira Mariamu (**Math 1:18-25; Luka 1:26-38**). Waislamu wanalikiri hili. Waislamu wanakiri pia kwamba Yesu alikuwa na nguvu zisizo za kawaida na alitenda miujiza mingi. Hata hivyo, upo ushahidi wa nyongeza unaodhihirisha kwamba Yesu alikuwa Zaidi ya mwanadamu na hata nabii lakini alikuwa na ni "Mwana wa Mungu."

**B.** ***Yesu alijilinganisha na Mungu na kujitambulisha mwenyewe kuwa ni Mungu***

Ajijola kwa usahihi anasema, "Mungu anajitambulisha kwa tabia zake. Kama imethibitika na kukubalika kwamba Yesu ni Bwana wa tabia ya Kiungu, mtu yupo sahihi kumpeleka kwa Mungu." (Ajijola 1972: 20) Yesu kweli ni, "Bwana wa tabia ya Kiungu,"kama maneno na matendo ya Yesu yanavyodhihirisha:

1. Alidai kuwepo kabla (i.e., alikuwepo kabla ya kuwa mwanadamu) (**Yohana 8:58; 17:5, 24**). Ni kweli alikuwepo (**Yohana 1:1-2, 14-15, 30; 8:58; 1 Wakor 8:6; Wafil 2:6-7; Wakol 1:15-17; Waeb 1:2; 1 Yohana 2:13-14**).
2. Alidai kuwa alitoka kwa Baba Mbinguni (**Yohana 3:13; 5:23-24; 6:29, 32-39, 41-42, 46, 50-51, 57-58, 62; 7:33; 8:23, 42; 11:41-42; 16:5, 27-28; 17:3, 5, 8, 18, 23, 25**). Kweli alikuwa hivyo (**Yohana 3:31; 13:3; 29-30; 1 Wakor 15:47; 1 Yohana 4:9-10, 14**).
3. Alidai kuwa yeye pekee ndiye amjuaye Baba na aweza kumdhihirisha Baba (**Math 11:27; Yohana 6:46; 17:25**). Hii ni kweli (**Yohana 1:18; Waeb 1:1-2; 1 Yohana 5:20**).
4. Alidai kuwa hatafanya lolote kwa ajili yake bali lile Baba alitakalo (**Yohana 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Kweli aliishi maisha matakatifu na ni udhihirisho halisi wa Baba (**Math 1:22-23; 27:3-4; Marko 1:24; Luka 1:35; 4:34; 23:22, 40-41, 47; Yohana 5:30; 7:18; 8:29, 46; 14:6-11; 17:6; Matendo 3:14; 4:27, 30; 13:28, 35; 2 Wakor 4:4; 5:21; Wakol 1:15, 19; 2:9; 1 Tim 3:16; Waeb 1:3, 9; 3:2; 4:15; 7:26-28; 9:14; 1 Pet 1:19; 2:22; 1 Yohana 2:29; 3:5; Ufu 3:7; 5:1-8**).
5. Biblia inasema Mungu aliwatuma manabii (**2 Nyakati 36:15; Yer 26:5; Luka 11:49-51**). Kuonyesha kwamba ni Mungu aliyekuja Duniani, Yesu alisema kwamba yeye ndiye aliyewatuma manabii ulimwenguni (**Math 23:34-35**).
6. Alidai kutuma na kubatiza kwa Roho mtakatifu (**Luka 24:49; Yohana 15:26; 16:7; 20:22**). Kwa kweli alifanya hivyo (**Math 3:11; Marko 1:8; Luka 3:16; Yohana 1:33; Matendo 1:8; 2:1-21**).
7. Anajua na kutabiri yajayo (**Math 10:17-23; 12:40, 27-28; 16:21; 17: 9, 22-27; 20:17-19; 21:1-7; 23:34-36; 24:1-31; 26:1-2, 13, 20-25, 31-34, 69-75; Marko 8:31; 9:1, 9, 30-31; 10:32-34; 11:1-7; 13:1-27; 14: 9, 12-21, 27-30, 66-72; 16:6-7; Luka 8: 49-56; 9:22, 43-44; 17:22-36; 18:31-33; 19: 29-35, 41-44; 21:7-28; 22: 7-13, 20-23, 31-34, 54-62; 24:6-8; Yohana 2:18-22; 4:21; 6:70-71; 11:23, 43-44; 12:27-33; 13:18-28, 36-38; 16:4, 16-20, 32; 18:4, 25-27; 21: 4-6, 18-19; Matendo 1:5, 8**).
8. Alisema yeye ndiye Bwana wa Sabato (**Math 12:8; Marko 2:28; Luka 6:5**). Mafarisayo walidai kuwa wanafunzi wa Yesu walikosea kwa kuvunja masuke ya ngano siku ya sabato. Yesu alijibu kwamba "wanafunzi hawakuwa na hatia *kwa sababu* [Yeye] kama mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato" (Carson 1982: 67). Kwa kusema hivyo, Yesu aliuelezea ukuu wake juu ya Sabato na hivyo, kuwa na mamlaka ya kuibadili sheria ya Sabato" (Moo 1984: 17). Maelezo haya yanadai kuwa sawa na Mungu kwa sababu Sabato ni sehemu ya amri kumi (Amri kumi za Mungu), ambayo ni amri ya Mungu iliyotolewa na Mungu mwenyewe kwa Musa Mlimani Sinai (**Kut 20:1-17**). Kwa maelezo mengine, ni Mungu pekee anayeweza kuitangaza sheria ya Mungu, na kwa hiyo ni Mungu pekee ambaye yupo juu ya sheria ya Mungu na anayo mamlaka ya kuibadili au kuivunja sheria Yake.
9. Alidai kuwa na mamlaka ya kuwasamehe watu dhambi zao (**Math 9:2-8, 12-13; Marko 2:3-12;**

[28] Fundisho kwamba Yesu ni Mungu kwenye mwili mtu wa pili kwenye Utatu pia inatueleza kuwa *Mungu* ni nani. Ukiri wa msingi wa Waislamu (*tauhid*) ni kwamba yupo Mungu mmoja. Wakristo hali kadhalika wanaamini na kukiri kwamba Mungu ni mmoja. Asili ya Mungu ni "Mmoja" ni tofauti kati ya Uislamu na Ukristo. Wazo la Utatu la Wakristo litajadiliwa kwa kina hapo chini, kwenye kipengele cha **4.IV. Utatu**.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**Luka 5:17-26, 31-32; 7:47-50; 9:56; 19:10; Yohana 5:33-34; 8:1-11; 10:7-9; 12:47**). Hakika, yeye ndiye Mwokozi ambaye pekee aweza kuwaokoa watu na dhambi zao (**Math 1:21; Luka 2:11; Yohana 1:29; 3:17; 4:42; Matendo 3:26; 4:12; 5:31; 13:23, 38-39; 15:11; 16:31; Warumi 3:24-26; 4:25; 5:1, 6-11, 15-21; 8:2; 10:9; 1 Wakor 1:30; 6:11; 15:17; 2 Wakor 5:18-21; Wagal 1:3-4; Waef 2:13-16; 4:32; 5:2, 25-26; Wafil 3:20; Wakol 1:12-14; 3:13; 1 Wathes 1:10; 5:9-10; 1 Tim 1:15; 2 Tim 2:10; 3:15; Tito 1:4; 2:13-14; Waeb 2:17; 5:9; 7:25; 13:20; 1 Pet 1:18-19; 3:18; 2 Pet 1:11; 1 Yohana 3:5; 4:9-10, 14; Ufu 5:9; 14:4**).

C. S. Lewis anakumbusha maana ya Yesu kudai kusamehe dhambi—dhambi yoyote: "Tunaweza kujua jinsi ambavyo mwanadamu anaweza kumsamehe mtu aliyemkosea yeye mwenyewe. Unakanyaga kidole changu na ninakusamehe, unaiba fedha zangu na ninakusamehe. Lakini ninini anachokifanya mtu, mwenyewe hajaiba na hajakanyaga, nani atakayetangaza kwamba amekusamehe kwa kukanyaga vidole vya mtu mwingine na kuiba fedha za mtu mwingine? . . . Ndivyo alivyofanya Yesu. Aliwaambia watu kwamba dhambi zao zimesamehewa, na kamwe hakusubiri kuwauliza watu wengine ambao bila shaka dhambi zao ziliwajeruhi wengine. Hakusita kujionyesha kama yeye ndiye kwa sehemu alikuwa mhusika mkuu, mtu ambaye kimsingi alishtakiwa kwa makosa yote. Hili linaleta mguso wa pekee kama kweli yeye alikuwa Mungu ambaye sheria zake zilivunjwa na ambaye upendo wake ulijeruhiwa na kila dhambi. Kwenye midomo ya wasemaji wote ambao siyo Mungu, maneno haya yangehusisha kile ninachoweza kukiona kama ni upumbavu na kiburi ambacho hakikuwahi kudhihirishwa na tabia nyingine yoyote kwenye historia." (Lewis 1996: 55)

10. Alidai kuwa na nguvu ya kuwarithisha watu uzima wa milele (**Yohana 3:16; 4:14; 5:25-29, 40; 6:27, 32-40, 44, 47-58, 68; 10:10, 27-28; 11:25-26; 14:6, 19; 17:1-3; Ufu 1:18**). Alifanya hivyo kwa kweli (**Warumi 6:23; 2 Tim 1:10; 1 Yohana 5:11-13, 20; 21:27**).

11. Alidai kuwa muasisi wa maisha yenyewe (**Yohana 11:25**). Kweli ndivyo alivyo (**Yohana 1:4; 5:26; Ufu 1:18**).

12. Alidai kuwa na mamlaka yote (**Math 11:27; 19:28; 26:64; 28:18; Marko 14:62; Luka 10:22; 22:29-30, 69; Yohana 17:2; 18:36-37**). Kweli anayo mamlaka yote na anatawala kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana (**Luka 1:32-33; 2:11; 19:37-38; 23:42; Yohana 3:31; 13:3; Matendo 2:30-36; 5:31; 10:36; Warumi 9:5; 14:9; 1 Wakor 15:23-28; Waef 1:20-22; Wafil 2:9-11; Wakol 2:10, 15; 1 Tim 6:15-16; 2 Tim 4:8; Waeb 2:7-8; 10:12-13; 1 Pet 3:22; Ufu 1:5; 5:12; 11:15; 12:10; 14:14; 17:14; 19:11-16; 20:4-6**).

13. Alisema atauhukumu Ulimwengu (**Math 7:21-23; 13:41; 16:27; 25:31-46; Yohana 5:22, 27-29; Ufu 2:23; 22:12**). Kweli atafanya hivyo (**Math 3:12; Luka 3:17; Matendo 10:42; 17:31; Warumi 2:16; 14:10; 1 Wakor 4:4-5; 2 Wakor 5:10; 2 Tim 4:1, 8; 1 Pet 4:5**).

14. Yesu alijilinganisha na kujitambulisha na Mungu kwa ujumla (**Marko 9:37; Luka 22:69-70; Yohana 5:17-23; 8:12-58; 10:30, 34-38; 12:44-49; 14:1, 6-11; 15:23; 17:21-23**). D. A. Carson anaelezea baadhi ya kweli zilizopo kwenye Injili ya Yohana: "Yesu alisisitiza kwamba kumwamini yeye ni kumwamini yeye aliyempeleka (12.44), kumtazama yeye ni kumtazama yeye aliyempeleka (12.45; 14.9), Kumchukia yeye ni kumchukia Baba (15.23). Alisema wote wamheshimu Mwana kama wanavyomheshimu Baba (5.23), kwamba yeye na Baba ni wamoja (10.30). Hatujifunzi tu kwamba Mwana hatafanya chochote isipokuwa kile alichoonyeshwa na Baba, lakini kwamba Mwana *hutenda* chochote atendacho Baba (5.19). . . . Maneno ya Yesu ni maneno ya Mungu (3.34); hii ndiyo sababu mtu akimpokea *Yesu* mashahidi huthibitisha kwamba *Mungu* ni wa Kweli [3:33]. . . . Kwa kifupi, njia iyo hiyo, Imani itupelekayo kwenye uzima husikia neno la *Yesu* na kumwamini *yeye aliyempeleka* (5.24; 14.24). Ni Yesu pekee aliyemwona Baba (6.46); lakini kumjua Yesu ni kumjua Baba (8.19)." (Carson 1994: 147, 156)

Ufupisho wa C. S. Lewis unamaanisha madai ya Yesu hapo juu: "miongoni mwa Wayahudi hawa alitokea mtu aliyesema kana kwamba yeye alikuwa Mungu. Alidai kusamehe dhambi. Alisema alikuwepo tokea mwanzo. Alisema atakuja kuhukumu Ulimwengu nyakati za mwisho. Sasa tuyaweke haya vizuri. Miongoni mwa imani, kama Wahindi, kila mmoja aweza kusema kuwa alikuwa sehemu ya Mungu, au mmoja na Mungu: kusingekuwa na jambo lolote la kushangaza kuhusianana hilo. Lakini mtu huyu, kwa kuwa alikuwa Myahudi, kusingemaanisha aina hiyo ya Mungu. Mungu, kwa lugha yao, humaanisha kiumbe nje ya Ulimwengu ambao aliuumba na alikuwa tofauti sana na kitu kingine chochote. Na unapolijua hilo, utaona kwamba kile huyu mtu anachokisema kilikuwa, kwa maana nyingine, jambo ambalo ni la kushtusha sana ambalo halikuwahi kutamkwa na midomo ya mwanadamu. . . . Ninajaribu hapa kumzuia yeyote ayakayesema mambo ambayo watu husema kumhusu Yeye: 'Niko tayari' kumkubali Yesu kama mwalimu maarufu, lakini sikubali madai yake kuwa Yeye ni Mungu.' Hilo ni jambo moja ambalo hatupaswi kulisema. Mtu aliyekuwa mtu wa kawaida na kusema mambo

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kama hayo Yesu aliyoyasema asingelikuwa mwalimu maarufu. Angeweza kuwa ni mwenda wazimu—kwa kiwango cha mtu yule aliyesema kwamba aliiba yai—au vinginevyo angekuwa Shetani wa Kuzimu. Ni lazima ufanye uchaguzi wako. Kwamba huyu mtu alikuwa, na ni, Mwana wa Mungu; au vinginevyo ni kichaa au kitu kingine kibaya. Unaweza kumnyamazisha kwa upumbavu, ungeweza kumtemea mate usoni na kumwua kama pepo; au ungeweza kumwangukia na kumwita Bwana na Mungu. Lakini tusimshushue kwa jambo lolote la kijinga kuhusiana na kuwa kwake mwalimu maarufu. Hakuacha nafasi hiyo kwetu. Wala hakukusudia kufanya hivyo." (Lewis 1996: 55-56)

**C.** ***Yesu alidai kuwa na uhusiano wa kipekee na Mungu Baba, Alimwita "Baba Yangu"***

Kwenye **Math 7:21; 10:32-33; 11:27; 12:50; 16:17; 18:10, 19; 20:23; 25:34; 26:39, 42, 53; Luka 2:49; 10:22; 22:29; 24:49; Yohana 2:16; 5:17, 43; 6:32, 40; 8:19, 38, 49, 54; 10:18, 25, 29, 37; 14:2, 7, 20, 21, 23; 15:1, 8, 10, 15, 23, 24; 20:17; Ufu 2:27; 3:5, 21** Yesu anaonyesha uhusiano wake maalum na Mungu Baba kwa kumwita "Baba yangu." Hilali ananukuu Yesu kutumia neno "Baba" kama kuashiria kwamba Yesu hakuwa Mungu (Al-Hilali 1998: 905). Tena, Hilali hakutokea kujua maana ya Yesu kutumia neno hilo. Yesu hakumtaja Mungu kama "Baba yetu," alichowafundisha wanafunzi wake kusema wanapokuwa wakiomba kwa Mungu (**Math 6:9;** angalia pia **Luka 11:2; Warumi 1:7; 1 Wakor 1:3; 2 Wakor 1:2; Wagal 1:3; Waef 1:2; Wafil 1:2; Wakol 1:2; 2 Wathes 1:1; Filemoni 1:3**). Badala yake, alimtaja Baba moja kwa moja, akitumia neno la Kiaramaiki "Abba," neno la ukaribu, mguso binafsi (**Marko 14:62**). Ingawa ilikuwa ni mara chache sana kwa Wayahudi wengine *kumwelezea* Mungu kama Abba, "hatuna ushahidi kwamba kabla ya Yesu *hajamuelezea* Mungu kama Abba" (Bauckham 1978: 249, fafanuzi imeongezwa).

Alikuwa ni Yesu alimwita Mungu *"Baba yangu"* kilichosababisha Wayahudi wajaribu kumwua kwa kufanya kufuru. Walitambua (kama ambavyo Hilali kwa hakika hakuelewa) kwamba wakati Yesu alipomwita Mungu *"Baba yangu"* alikuwa *"akimwita Mungu Baba yake mwenyewe, kujifanya yeye mwenyewe sawa na Mungu"* (**Yohana 5:18**; angalia pia **Yohana 8:38-59; 10:22-33**). Vile vile, Yesu alisema, *"Mimi na Baba tu wamoja"* (**Yohana 10:30**).

Muunganiko wa kina kati ya Kristo na Baba ulikuwa wazi kwenye tukio jingine. Kwenye **Yohana 14:6-14** mazungumzo yafuatayo yalikuwa baina ya Yesu na Wanafunzi wake Tomaso na Philipo: [6] *Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona. Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake. Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu; la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe. Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.*

Carson anaonyesha kwamba maelezo ya Yesu yanaeleza umoja kamili kati yake mwenyewe na Baba; kwakweli, "ni kwa uhakika wa kiwango hiki cha umoja kinatuhakikishia kwamba Yesu anamfunua Baba kwetu (Carson 1991: 494). Kuna mambo muhimu ya kujifunza kwenye umoja huu baina ya Yesu na Baba:

- Kwanza, "Siyo kila barabara ituongozayo kuurithi uzima wa milele. Yesu ndiye njia iliyochaguliwa na Mungu." (Ngewa 2006: 1283)
- Pili, "Matokeo ya Yesu na Baba kuwa wamoja ni kwamba chochote atakachoulizwa Baba pia ataulizwa Yesu. Wakati wote Baba ni mwenye vyote. Yesu, kama Mwana, amemkabidhi, lakini kwa wakati huo huo, yeye na Baba wanafanya kama mmoja. Kila kiombwacho au kitolewacho na Baba pia kitaombwa na kutolewa na Yesu. Hivyo Yesu akawa mmoja wa kuombwa baraka (*niombe mimi*) na wa kufanya maombi yajibiwe mapema (*kwa jina langu*) ([**Yohana**] **14:13b-14a**)." (Ngewa 2006: 1284)

Tatu, wakati upekee ukidumu baina ya Baba na Mwana (wawili tofauti lakini bado ni wamoja), Kile Yesu anachokisema hapa ni kulikataa wazo la kwamba Yeye ni nabii tu wa *kawaida* au Mjumbe. "Uwakilishi huu' [Mjumbe] unashindwa kutenda wakati tunapoelezwa kwamba *chochote* afanyacho Yesu ni kile ambacho Baba amempa *kukifanya*, na kwamba hufanya *kila kitu* afanyacho Baba: sasa tunazungumzia upekee lugha ya 'Uana'. Hakuna mwakilishi wa kawaida [Mjumbe] atakayemtaja yeye aliyemtuma kama Baba yake, madai kwamba yeyote aliyemwona Yeye alimwona Baba, na kuthibitisha muungano baina yake yeye mwenyewe na yule aliyemtuma." (Carson 1991: 494-95; angalia pia **Yohana 5:19-23** na majadiliano kwenye namba 23 hapo juu na Sehemu ya Pili, namba 6)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**D.** ***Matumizi ya Yesu ya neno "Mwana wa Adamu" ni kumbukumbu kwa Uungu wake***

Yesu aliitwa *"Mwana wa Adamu"* yapata mara 80 kwenye Injili; ni utambulisho wake muhimu kwa kila siku. Hilali anatambua kwamba Yesu "hujiita mwenyewe 'Mwana wa Adamu' (Marko 2:10)" (Al-Hilali 1998: 905). Hata hivyo, Hilali ni wazi kwamba haelewi maana ya neno. *"Mwana wa Adamu"* ni vyote viwili Uanadamu na Uungu, kama ilivyo kwa Yesu ni mwanadamu na ni Mungu. Msemo*"Mwana wa Adamu"* umenukuliwa toka kitabu cha **Dan 7:13-14** (*"Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. 14 Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa."*). Kwenye **Ufu 1:13-14** Yohana anapokea ufunuo kutoka kwa Yesu, ambaye ameelezwa kama *"mmoja kama Mwana wa adamu . . . [ambaye] kichwa na nywele zake ni nyeupe kama sufi, kama theluji."* Picha hizo zinatoka kwenye maono ya Danieli **Dan 7:9, 13**. Hata hivyo, maono ya Danieli (**Dan 7:9**) ilikuwa *"Mzee wa siku"* ambaye *"mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi."* Kwenye mazingira hayo, "Yohana aliona 'mtu kama mwanadamu' aliyeheshimiwa na kutambuliwa kama Mzee wa Siku—muunganiko wa siri lakini wenye ukweli wa madai kwamba cheo chake ni 'wa kwanza na wa mwisho' ([Ufu] 1:17), ambaye kwa hicho Mungu alitangaza Uungu na Umilele wake (Isa. 41:4; 44:6; 48:12). Mwana wa Adamu ni Mungu, mwingi wa busara na utakatifu." (Johnson 2001: 59)

Hivyo basi, popote Yesu alipotumia neno*"Mwana wa Adamu"* alitangaza kwamba alikuwa, na kweli, Mungu alikuja Ulimwenguni *kama mwanadamu*. Kwenye **Yohana 3:13** alinena wazi kwa kusema, *"Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu."* Vivyo hivyo, kwenye **Yohana 6:62** Yesu alisema,*"Itakuwaje basi, mmwonapo Mwanawa Adamu akipaa huko alikokuwako kwanza? "* Carson anaeleza kwamba "Yesu mwana wa Adamu (nafasi iliyounganishwa maalumu na utendaji wake kama aliyefunuliwa toka mbinguni) kwanza *alishuka* [**Yohana 6:38**], na hivyo kupaa kwake ni kurudi *kule alikokuwa kabla* (*cf.* 17:5). Hili halithibitishi tu uwepo wa Yesu Kabla, lakini unamuweka kwenye daraja tofauti sana na wale mashujaa wa dini ya Kiyahudi waliomtangulia." (Carson 1991: 301)[29]

Tunamwona Yesu akidai kuwa Mungu na kwenye maelezo mengine *"Mwana wa Adamu."* Kwa mfano, Yesu anadai kwamba *"Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi"* (**Math 9:6; Marko 2:10; Luka 5:24**) ni madai ya Kuwa Mungu *kuja ulimwenguni kama mwanadamu*, kwa sababu ni Mungu pekee mwenye uwezo wa kusamehe dhambi; hapa Yesu anadai kusamehe dhambi kwa mamlaka yake mwenyewe (angalia nukuu kutoka C. S. Lewis [1996: 55] hapo juu). Kwenye **Math 12:8; Marko 2:28; Luka 6:5** Yesu alisema, *"Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato."* Kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa kusema kwamba, Yesu alidai kuwa yeye ni Mungu mwenyewe. Kwenye **Luka 19:10** Yesu alisema, *"Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea"* (angalia pia **Luke 19:9-10**). Kupata wokovu kwa mtu yeyote ni kitu ambacho ni Mungu pekee anayeweza kukifanya. Kwenye **Math 13:41-42** Yesu alisema, *"Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, 42 na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."* Hili linazungumzia hukumu ya mwisho. Vivyo hivyo, kwenye **Math 16:27** Yesu anasema kwamba *"Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake."* J. Knox Chamblin anaonyesha kwamba "kama kwenye Daniel 7:13-14, Mwana wa Adamu anafunuliwa kama Mungu (malaika ni *wake,* siyo wa Baba tu, mst. 27)" (Chamblin 1989: 743).

[29] Carson anazungumzia kuhusu neno "Mwana wa Adamu" kuwa muhimu kwa kuunganishwa na kazi za Yesu kama alivyo funuliwa kutoka mbinguni. "Kulingana na Daniel 7:9-22Mwana wa Adamu ni mtu aliyetoka mbinguni atakayeshiriki kwenye hukumu ya siku ya mwisho; hata hivyo, Yesu analeta jambo jipya kwenye nafasi yake kwa kusema kwamba Mwana wa Admu ni lazima pia apate mateso. Hivyo, Yesu anaunganisha pamoja Mwana wa Adamu na mtumishi atesekaye (Isa. 52:13-53:12 [angalia **Math 17:12; 20:25-28; Marko 10:42-45; Luka 22:25-27; Yohana 3:14**])." (Schreiner 1989: 818) "Kufa na kuinuliwa kwa mtumishi wa Bwana ni njia ambayo Mungu anaufunua Utukufu wake na kuuonyesha Uungu wake kwa Ulimwengu. . . . Mtumishi, kwenye mateso na kuinuliwa kwake, Siyo mwanadamu wa kawaida aliyetoka kwa Mungu, lakini, ni kwenye mateso na kuinuliwa kwake, ni utambulisho wake wa Mungu wa pekee" (Bauckham 1999: 49, 51). Hivyo, neno"Mwana wa Adamu" alifunua (pamoja na maneno mengine na matendo ya Yesu) asili ya kweli ya Mungu ni nani. Kama Richard Bauckham alivyoliweka hivi, "Yesu alifunua utambulisho wa Kimungu—Mungu kweli ni nani—Kwenye mateso kama ilivyo kwenye kuinuliwa, na kwa kuunganishwa vyote viwili. Utambulisho wa Mungu umefunuliwa katika Yesu mwenyewe, maisha yake na msalaba wake, kama ilivyo kwenye kweli ya kuinuliwa kwake, kwenye njia ambayo ni ya kuendelea na kwa agano la kale na Wayahudi kumjua Mungu, lakini pia ni kitabu cha kushangaza." (Ibid.: viii) Asili ya kuwa Mungu ni nani na anavyofanana ni eneo kubwa la mgongano baina ya Ukristo na Uislamu. Kwa kifupi, Allah kwa Uislamu ni, mmoja naweza kusema, "mungu wa kipimo kimoja" ., mungu wa nguvu za kuinuliwa pekee; wazo lake la kuwa mungu wa upendo pekee pia, mateso, huruma kwake ni jambo la kigeni  na kweli ni chuki kwa Uislamu. Hata hivyo, Mungu wa Biblia, Zaidi sana kama ilivyofunuliwa kwa Yesu, ni vigumu zaidi sana kuliko Allah wa Uislamu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Kutuma Malaika na kufanya hukumu ya milele ni matendo ya Mungu. Hili ni sawa na lile ambalo Yesu alijiita mwenyewe *"Mwana wa Adamu"* kwenye **Math 24:30-31**; **24:42-44; 25:31-46; Marko 8:38; 13:26; Luka 9:22-26; 12:8-9; Yohana 9:35-39**. Maelezo ya Yesu kuhusu kusamehe dhambi, kutoa wokovu, na hukumu inadhihirisha msingi wa tofauti kati yake mwenyewe na Mohamedi: Mohamedi anaweza tu kutangaza kile ambacho Allah anaweza kufanya kwenye kusamehe dhambi, kuokoa, na kuhukumu watu; Yesu alisema kwamba Yeye mwenyewe anaweza kuyafanya hayo yote.

Kwenye **Math 24:42-44** *"Mwana wa Adamu"* kimsingi liko sawa na "Bwana." Kwenye **Math 25:31-46** *"Mwana wa Adamu"* ni sawa na "Mfalme" ambaye *"atakayeketi katika kiti chake cha utukufu na enzi"* na kuhukumu watu wote wa ulimwengu wote, kuwatupa wengine Jehanamu na wengine kuwapa uzima wa milele. Hili linawezekana kwa Mungu pekee. Hili tena, wakati Yesu alipojiita mwenyewe *"Mwana wa Mungu"* alijilinganisha mwenyewe na Mungu mwenye nguvu. Kwenye **Math 19:27-28** Yesu anasema kwamba, *"katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli"* (angalia pia **Luka 22:29-30**). "Kiti cha Enzi" kitakuwa ni Kiti cha Enzi cha Mungu. Kwenye **Yohana 6:27** Yesu anasema kwamba watu wakitendee kazi *"chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa."* Tena, uzima wa milele ni kitu ambacho ni Mungu pekee anayeweza kutoa, na hapa Yesu anasema kwamba yeye anaweza kutoa (angalia pia **Yohana 6:40, 53-54**).

**E.** ***Yesu alitumia neno "Mwana wa Adamu" sambamba na neno "Mwana wa Mungu" kuonyesha kwamba maneno yote mawili yana maana sawa***

Kwenye **Math 16:13-17** Yesu analinganisha kuwa *"Mwana wa Adamu"* sawa na kuwa *"Mwana wa Mungu."* Aliwauliza wanafunzi wake, *"Watu wanasema mwana wa adamu ni na ni?"* (**Math 16:13**) Kwenye **Math 16:14** wakamjibu, *"Wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii."* Yesu *alikataa* jibu kwamba yeye ni *mmojawapo* wa nabii, kwa sababu aliwauliza tena, *"Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?"* (**Math 16:15**) Kwenye **Math 16:16** Petro alijibu, *"Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."* Na Yesu akajibu, *"Heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni"* (**Math 16:17**). Hivyo, ingawa Yesu kweli alikuwa nabii, hakuwa *sawa na* nabii mwingine. Vivyo hivyo, inagwa Yesu kweli alikuwa mwanadamu, hakuwa mwanadamu wa *kawaida.*

Kwenye **Yohana 1:49** Nathanael alisema, *"Rabi, wewe u <u>Mwana wa Mungu</u>, ndiwe Mfalme wa Israeli."* Yesu hakukataa hili lakini kwenye **Yohana 1:50-51** anaeleza, *"Utaona mambo makubwa kuliko haya. . . . Akamwambia, Amin, amin, nawaambia, Mtaziona mbingu zimefunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya <u>Mwana wa Adamu</u>."* Wakati neno *"Mwana wa Mungu"* na *"Mfalme wa Israel"* linamaanisha Masihi, majibu ya Yesu yanapanua maana bila shaka Nathanael alitarajia *"Mwana wa Mugu."* Yesu alifanya hili kwa kurejea maono ya Yakobo kwenye **Mwanzo 28:12**. Neno linasema *", tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake"* linabeba picha ambayo ina "mahusiano yasiyoingilika baina ya Yesu na Baba" (Köstenberger 2007: 430). Yesu anasema kwamba Yeye ni nafasi ya Mungu kujifunua mwenyewe hapa duniani. Kwa mtazamo huu, aya hii ya mwisho inarudia uthibitisho wa utangulizi [**Yohana 1:1-18**]: Yesu ni ufunuo kamili wa utukufu na uwepo wa Mungu." (Burge 1989: 849)

Kwenye **Yohana 5:19-29**, Kwa kurudia Yesu anajiita mwenyewe "Mwana," *"Mwana wa Mungu,"* na *"Mwana wa Adamu."* Yesu kutajwa kama *"Mwana wa Mungu"* na *"Mwana wa Adamu"* ni sawa kwenye kutoa hukumu siku ya kufufuka na hukumu. Kwa hiyo maneno haya mawili basi yana maana sawa. Kwa kweli, Maelezo ya Yesu kutoka **Yohana 5:21-29** kuhusiana na hukumu, hasa hasa maneno yake kwenye **Yohana 5:22** kwamba *"Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote,"* ni maelezo ya ajabu ya Mamlaka ya Kiungu ya Kristo, kwa kuwa Korani na Maandiko ya Waebrania (Agano la Kale) yanathibitisha kwamba hukumu ni nafasi ya juu ya haki ya Mungua.

Katika mashitaka yake mbele ya kuhani mkuu kwenye **Math 26:63-65** (**Marko 14:61-63; Luka 22:66-71**), majibizano yafuatayo yaliendelea: *"Kuhani Mkuu akamwambia, Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu.Yesu akamwambia, Wewe umesema; lakini nawaambieni, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni. Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake, akisema, Amekufuru; mna haja gani tena ya mashahidi? Tazameni, sasa mmesikia hiyo kufuru yake.'"* Craig Blomberg anajadili kwanini Yesu alidai kuwa "Mwana wa Adamu" kwenye hili yako wazi: "Hili la kusema ni 'Mwana wa Adamu', badala ya kudai kwamba alikuwa namna ya Masihi, ndicho kilichomfanya Kuhani mkuu kurarua vazi lake na kutangaza kwamba Yesu amekufuru (26:65). Kujitangazia Umasihi halikuwa kosa kubwa; hata hivyo, Wayahudi wasingempokea Masihi kamwe! Lakini kudai kuinuliwa, Mwanadamu wa mbinguni, mtu ambaye alikuwa Bwana na wa pili kwa Baba

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwenyewe mbinguni, kutenda dhambi ya kuvuka mipaka ambayo wengi wa viongozi wa Wayahudi waliona kuwa hairuhusiwi kwa mwanadamu wa kawaida wa kufa." (Blomberg 2007: 93)

**F.** ***Yesu alijiita mwenyewe "Mwana wa Mungu" na alikubali aitwe "Mwana wa Mungu" na wengine***

Hilali anaeleza kwamba "Kama nijuavyo mimi Yesu hakuwahi kujiita mwenyewe *Mwana wa Mungu* . . . ingawa mwenyewe alisikia akiitwa kwa jina hilo hakuona kama ni kitu . . . na hakukiona cheo hicho kama kitu cha maana kwake" (Al-Hilali 1998: 905, nukuu ya **Math 5:9, 45** pale ambapo neno"Mwana [au mtoto] wa Mungu" lilitumiwa kwa kila "mtu mwenye haki anayemcha Mungu"). Hilali hayupo sahihi. Wakti ambapo msemo ungeweza kuwa na maana pana, limetumika wazi wazi kwa Yesu kwa kumaanisha kwamba Yesu alikuwa Mungu aliyekuja duniani kama mwanadamu (i.e., alikuwa "Mwana wa Mungu" kwa maana maalum, mwenye mahusiano ya *kipekee* na Mungu Baba).

Kwanza, Yesu alijiita mwenyewe "Mwana" kuuelezea uhusiano wake wa *kipekee* na Mungu Baba. Kwenye **Math 11:27** (**Luka 10:22**) Yesu alisema, *"Nimekabidhiwa vyote na baba yangu; wala hakuna amjuaye Mwana, ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia."* Kile anachokisema Yesu hapa ni kwamba ni *Yeye pekee* ambaye kwa uhakika anamjua Mungu, na *njia pekee ya kumjua Mungu* ni kumpitia Yeye! Kumbuka kwamba *Wana* wanaopaswa kufanya au kumwelekeza mtu amjue Baba. Haya ni madai mazito ambayo yanapaswa kuchukuliwa kwa umakini, hasa wale wanaomwita Yesu Nabii mkuu. Kwa kusema maneno haya kwenye **Math 11:27** kuhusiana na uhusiano wake wa kipekee na Baba, Yesu anadai Uungu kwa ajili yake mwenyewe na kujiweka kwenye daraja la juu kuliko Mohamedi au mtu mwingine yeyote. Kwa kuwaambia wanafunzi wake wakawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wake, Yesu aliwaambia wawabatize waamini *"kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu"* (**Math 28:19**). Tena, anajiita mwenyewe "Mwana" kwenye mahusiano ya kipekee na Baba.

Kwenye **Yohana 3:16-18** Yesu anajiita mwenyewe *"Mwana mzaliwa pekee,"* "Mwana," na *"Mwana mzaliwa pekee wa Mungu."*[30] Kwa kazi alizokuwa akizifanya, Yesu alijiita mwenyewe*"Mwana wa Mungu"* kwenye **Yohana 5:25; 10:36; 11:4**. Kwenye mazingira hayo alifanya kile ambacho ni Mungu pekee mwenye nguvu za kufanya (kufufua wafu).

Kwenye mfano wa shamba la Mzabibu (**Math 21:33-46; Marko 12:1-12; Luka 20:9-19**), Yesu alijilinganisha mwenyewe na manabii waliotumwa kabla yake, kutabiri kifo chake mwenyewe, kuonyesha kwamba yeye ndiye njia pekee ya Wokovu, alisema kwamba ufalme haukuwa wa Wayahudi tu, na kujitaja mwenyewe kama "Mwana" ni njia ambayo alikataa madai Kiislamu kwamba Mohamedi ndiye nabii wa mwisho. Kwenye mfano, Mungu Baba aliwatuma manabii kwenda Israeli ambao waliwatenda jeuri; hivyo baadaye aliamua kumtuma mwanaye (Yesu). N. T. Wright kwa usahihi anahitimisha, kwamba "mara Baba alipomtuma mwana shambani, asingemtuma mwingine yeyote. Kumkataa Mwana ni kukataa nafasi ya Mwisho." (Wright 1996: 362, 365)

Pili, *Mungu Mwenyewe* kwa zaidi ya tukio moja alimwita Yesu "Mwanae" kwenye mazingira ambayo pekee yanaweza kuonesha Uana wa Kiungu wa Yesu. Kwenye ubatizo wa Yesu *"sauti kutoka mbinguni ilisema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa,ninayependezwa naye"* (**Math 3:17; Marko 1:11; Luka 3:22**). Tena, wakati Yesu alipowatokea wanafunzi wake watatu, *"sauti ikatoka kwenye lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye!'"* (**Math 17:5; Marko 9:7; Luka 9:35**).

Tatu, *Malaika Gabriel* alimwita Yesu*"Mwana wa Mungu."* Alipokuwa anamueleza Mariamu kwamba Yesu atazaliwa, Gabriel alieleza, *"Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu"* (**Luke 1:32**). Wakati Mariamu alipouliza *"Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?"* (**Luka 1:34**), Gabriel akajibu, *"Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu"* (**Luka 1:35**). Kwenye hali hiyo, maelezo ya Gabriel kwa *"Mwana wa Mungu"* yaweza kuelezea tu Uungu na Uana wa Yesu.

**G.** ***Maadui wa Yesu walitambua kwamba alidai kuwa yeye ni Mungu na walitafuta kumwua kwa kukufuru kwa sababu ya madai yake kwamba ni Mwana pekee wa Mungu***

Kwenye **Math 9:2-3; 26:63-66; Marko 2:6-7; 14:61-64; Luka 5:20-21; 22:66-71; Yohana 5:17-18; 8:53, 59; 10:30-33, 39; 19:7** Maadui wa Yesu walitambua kwamba Yesu alidai kuwa Yeye ni Mwana pekee wa Mungu na walitafuta kumwua kwa sababu ya madai hayo. Sheria za Musa zinaeleza adhabu ya kifo kwa kukufuru (**Walawi 24:14, 16, 23;** angalia **Yohana 19:7**). **Yohana 5:18** inasema kwamba Wayahudi walitafuta

[30] Kwa kuwa maandiko ya awali hayatumii nukuu au zinazofanana, kunao ushindani kama ni au siyo **Yohana 3:16-21** ni maneno ya Yesu (i.e.,mwisho wa majibu yake kwa Nikodemu yanayoanzia mstari wa**. 10**) au ni maoni ya mwandishi wa injili ya Yohana (angalia Carson 1991: 203-04; Burge 1989: 851). Kuhusiana na maana ya "mzaliwa pekee," angalia majadiliano kwenye sehemu ya **2.II.D.** ***Kulingana na Uislamu, Yesu ni nabii lakini siyo mwana wa Mungu***, hapo juu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kumwua Yesu *"sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivunja sabato tu,[kwa kumponya mtu siku ya sabato] bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu.* Yusuf Ali anakiri kwamba "Yesu alihukumiwa na Wayahudi kwa kukufuru kama madai ya kuwa Mungu au Mwana wa mungu" (Ali 2006: Q. 3:55n.395). Bernard Ramm anaonyesha, "Kwenye hali hiyo, kutokana na mtazamo wa kibinadamu, kulikuwa na jambo moja tu la Yesu kufanya. Alipaswa kuikana hukumu na kuonyesha sababu ya Yeye kumponya mtu siku ya Sabato. Hili hakulifanya. Alisema kwamba Wayahudi walikuwa sahihi. Yeye yuko sawa na Mungu. Kwenye aya zifuatazo Yesu anaonyesha vitu ambavyo ni Mungu pekee ambaye angevifanya lakini bado Yeye angevifanya. Hivyo Yeye ni sawa na Baba." (Ramm 1985: 43)

**H.** ***Watu humwabudu au kuomba kwa Yesu kama Mungu, na Yesu hukubali ibada hiyo***

Biblia imeliweka hili wazi kwamba ni Mungu pekee apaswaye kuabudiwa (**Kut 20:3-5; 34:14; Kumb 4:19; 5:7-9; 8:19; 1 Wafal 9:6-7; Isa 42:8**). Yesu mwenyewe alieleza kwamba ni Mungu pekee apaswaye kuabudiwa (**Math 4:10; Luka 4:8**). Kumwabudu mtu au hata malaika ni kuabudu sanamu na ni dhambi (**Kut 20:1-5; Kumb 5:6-9; Warumi 1:18-23**). Wanafunzi wa Yesu walilijua hilo.

Hata hivyo, kwenye **Math 2:11; 14:33; 28:9, 16-17; Luka 24:51-52; Yohana 1:1-14; 5:22-23; 9:35-38; 20:28; 28:9; Matendo 2:36; 7:59-60; 20:28; Warumi 9:3-5; Wafil 2:5-11; Tito 2:13; Waeb 1:5-10; 2 Pet 1:1; 1 Yohana 2:23; Ufu 5:1-14** watu humwabudu au kuomba kwa Yesu kama ambavyo wangefanya kwa Mungu mwenyewe. *Yesu hukubali Ibada yao.* Majibu ya Yesu ya kukubali kuabudiwa yangekuwa kufuru na ibada ya sanamu kwa kila mmoja, hata nabii, kama angekuwa tu ni mwanadamu. Ukweli kwamba Yesu hakukataa, bali alikubali watu wamwabudu, inaonyesha kwamba alijua kwamba Yeye ni Mungu aliyekuja Duniani kama mwanadamu—kwa sababu ni kwa kuwa Mungu aliyekuja duniani kama mwanadamu kulimpa Yesu haki ya kisheria ya kukubali kuabudiwa.

Ni kweli, kumwabudu Yesu kulijulikana kuwepo hata kabla ya Agano Jipya kuandikwa. Hili linajulikana kwa sababu mbalimbali, kwa sababu kuabudiwa kwa Yesu kwa ujumla kulianzia **Wafil 2:9-11**, ambayo ni Imani ya awali ya Kikristo ambayo ni ya kabla ya Paulo kuandika Waraka kwa Wafilipi (angalia majadiliano ya Imani ya Kikristo kwenye kipengele cha **2.IV.B.** ***Mwanzo wa Imani ya Kikristo***, hapo juu). **Wafil 2:9-11** inaashiria kutoka **Isa 45:22-23** inayohusisha kumwabudu Yahweh; hili tena, linaonyesha kwamba Yesu ni sawa na Mungu.

Kuna mguso wa muhimu wa ukweli kwamba Yesu alikubali kuabudiwa mwenyewe. Mwanazuoni wa Kiislamu Shaikh Abdul-Aziz bin Abdullah bin Baz anaeleza kwamba "kumwabudu Allah kunaonyesha kwamba Allah ni Mungu wa kweli ambaye pekee yake anastahili kuabudiwa, kama alivyo ni muumba na mwezeshaji wa wanadamu wote" (bin Baz 2002: 250; angalia, e,g., **Q. 2:21-22; 11:1-2; 16:36; 21:25; 51:56-58**). Kwa kuwa Yesu alikubali kuabudiwa Yeye mwenyewe na Uislamu na Korani wanatambua kwamba Yesu alikuwa safi asiye na dhambi, ulazima huu unamaanisha kwamba Yesu kukubali kuabudiwa mwenyewe *haikuwa dhambi.* Hili lingeweza kuwa kweli pekee kama alikuwa, kwakweli, ni Mungu aliyekuja duniani.

**I.** ***Yesu hasa aliitwa "Mungu" au "Bwana" kwenye matukio mengi ya Agano Jipya***

Kwa Zaidi ya tukio moja kwenye Agano Jipya linampa Yesu jina "Bwana" au "Mungu":

- **Math 7:22-23:** *Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana . . ." Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu."*
- **Luka 1:42-43:** *akapaza sauti [Elisabeti] kwa nguvu akasema, Umebarikiwa wewe katika wanawake, naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa. Limenitokeaje neno hili,hata mama wa Bwana wangu anijilie mimi?"*
- **Yohana 1:1, 14:** *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. . . . Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.*
- **Yohana 20:28:** Baada ya kuambiwa anyooshe mkono ili kugusa makovu kwa vidole vyake kwenye mikono ya Yesu na ubavuni mwake, Thomaso alisema, *"Bwana wangu na Mungu wangu!"* Yesu hakumkemea Thomaso kwa kukufuru bali alikubali hivyo vyeo na Uungu.
- **Matendo 7:59-60:** *Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake.*
- **Matendo 10:36:** *Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo (ndiye Bwana wa wote),*
- **Matendo 16:31, 34:** *Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako." . . . Akawaleta juu nyumbani kwake, akawaandalia chakula, akafurahi sana, yeye na nyumba yake yote.*

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

- **Matendo 20:28:** *Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe***.**
- **1 Wakor 2:7-8:** *iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu.*
- **1 Wakor 11:26:** *Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*
- **Warumi 9:5:** *ambao[akimaanisha Waisraeli] mababu ni wao, na katika hao alitoka Kristo kwa jinsi ya mwili. Ndiye aliye juu ya mambo yote, Mungu, mwenye kuhimidiwa milele. Amina.*
- **Wafil 2:5-7:** *Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu.*
- **Wakol 2:9:** *Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.*
- **Tito 2:13:** *tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu.* Kwa nyongeza kuitwa "Mungu," ni wazi kwamba Yesu pia aliitwa "Mwokozi," kwa sababu kwenye Agano la kale Mungu kwa hakika alisema, *"Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi"* (**Isa 43:11**).
- **Waeb 1:8-9:** *Lakini kwa habari za Mwana asema, Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio."* Hili limenukuliwa kutoka **Zab 45:6-7** ambalo lilisemwa kwa Mungu na hapa linatumiwa na Yesu.
- **2 Pet 1:1:** *Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika hali ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo.*
- **1 Yohana 5:20:** *Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele.*

### J. *Majina yale yale, vyeo, na sifa nyingine ambazo zilitumiwa na Mungu kwenye Agano la Kale au Agano Jipya zinatumiwa na Yesu kwenye Agano Jipya*

Wakati mwingine mistari ambayo ilimzungumzia Mungu imetaja au imenukuliwa moja kwa moja na kumtaja Yesu (kwenye jedwali lifuatalo, [x, y, z] linaashiria nukuu za moja kwa moja):

| Jina/Cheo/Sifa | Kutumika kwa Mungu | Kutumika kwa Yesu |
|---|---|---|
| NIKO | **Kut 3:13-14** | **Yohana 8:24, 28, 58; 18:5-6** |
| Bwana | **Isa 40:3[x]; 45:23-24[y]; Yoel 2:32[z]** | **Marko 1:2-4[x]; Wafil 2:10-11[y]; Matendo 2:36; Warumi 10:13[z]** |
| Mungu | **Zab 45:6-7[x]** | **Waeb 1:8-9[x]; Yohana 1:1, 14, 18; 20:28; 2 Pet 1:1** |
| Mwanzo na Mwisho | **Isa 41:4; 44:6; 48:12** | **Ufu 1:17; 2:8; 22:13** |
| Alpha na Omega | **Ufu 1:8[x]; 21:5-6[x]** | **Ufu 22:13[x]** |
| Kuinuliwa juu sana kupita mbingu | **Zab 57:5, 11; 108:5** | **Waeb 7:26** |
| Mwokozi | **Isa 43:3, 11; 1 Tim 4:10** | **Math 1:21; Luka 2:11; Yohana 4:42; Tito 2:13** |
| Mkombozi | **Zab 130:7-8** | **1 Wakor 1:30; Waef 1:7; Tito 2:13-14** |
| Mhukumu | **Mwanzo 18:25; Zab 50:4-6; 96:13** | **Yohana 5:22; 2 Wakor 5:10; 2 Tim 4:1** |
| Mfalme | **Zab 95:3** | **Ufu 17:14; 19:16** |
| Mfalme wa Israeli | **Isa 43:15; 44:6; Zef 3:15** | **Yohana 1:49; 12:13** |
| Mtakatifu | **1 Sam 2:2; Yohana 17:11** | **Matendo 3:14; Heb 7:26** |
| Mwema[31] | **Zab 34:8** | **Yohana 10:11** |
| Nuru | **Zab 27:1; Isa 60:20; Mika 7:8** | **Yohana 1:4-5, 9; 3:19; 8:12; 9:5** |
| Mwamba | **Kumb 32:4; 2 Sam 22:32; Zab 89:26** | **1 Wakor 10:4; 1 Pet 2:4-8** |
| Mume | | |
| Mchungaji | **Isa 54:5; Hos 2:16** | **Marko 2:18-19; 2 Wakor 11:2; Ufu 21:2** |

[31] Sifa ya Mungu ya "wema" inaashiria kile alichokitaka Yesu alipomwuliza yule kijana tajiri, *"Kwanini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema isipokuwa Mungu mwenyewe"* (**Marko 10:18; Luka 18:19**). Hakukana kwamba alikuwa Mungu, kama Hilali (1998: 906-07) anavyodai. Badala yake, aliuthibitisha Uungu wake kwa kuuliza swali la wazi. Kwa msisitizo, alimwambia yule mtu, "Kwa uhakika unamjua unayeongea naye?" Kama Victor Babajide Cole alivyoliweka, "Yesu hakukana kwamba Yeye siyo 'mwema'. Badala yake, alikuwa anamkazia huyo mtu kuona ukweli uliopo kwa kumwita Yeye kama 'mwema', Kuonyesha kwamba yeye ni Mungu!" (Cole 2006: 1189)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

| | | |
|---|---|---|
| Muumba | **Zab 23:1; 80:1; Isa 40:11** | **Yohana 10:11, 16; Waeb 13:20; 1 Pet 2:25; 5:4** |
| Mwezeshaji | **Mwanzo 1:1; Zab 102:25-27**[x]**; Isa 40:28** | **Yohana 1:3, 10; Wakol 1:16; Waeb 1:2, 10-12**[x] |
| Mwendelezaji | **Ayubu 34:14-15; Zab 3:5; 2 Pet 3:7** | **Wakol 1:17; Waeb 1:3** |
| Mtoa uzima | **Kumb 32:39; 1 Sam 2:6; Zab 36:9** | **Yohana 5:22; 10:28; 11:25** |
| Chanzo cha "maji ya uzima" | **Yer 2:13** | **Yohana 4:10, 14; 7:37-38** |
| Mwenye kusamehe dhambi | **Kut 34:7; Isa 55:7; Dan 9:9** | **Math 1:21; Marko 2:5; Matendo 26:18; Wakol 2:13** |
| Mtawala juu ya vyote | **Neh 9:6; Isa 44:24-27; 45:22-23**[x] | **Math 28:18; Waef 1:20-22; Wafil 2:9-11**[x]**; 3:21** |
| Ajuaye vyote | **Ayubu 21:22; Zab 33:13-15** | **Yohana 16:30; 21:17** |
| Mchunguzi wa moyo na mawazo | **1 Nyak 28:9; Zab 7:9; 139:1-4, 23; Yer 17:10** | **Marko 2:8; Yohana 2:24-25; Ufu 2:23** |
| Mtuzaji kulingana na matendo ya watu | **Zab 62:12**[x]**; Yer 17:10; 32:19** | **Math 16:27**[x]**; Ufu 2:23** |

**K.** ***Nabii na maandiko ambayo yanahusika kumtaja Mungu au Bwana kwenye Agano la Kale yamenukuliwa na kumtaja Yesu kwenye Agano Jipya***

- *Nimemweka Bwana mbele yangu daima, Kwa kuwa yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa.* (Zab **16:8**; imemtaja Yesu kwenye **Matendo 2:25**)
- *Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele, Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili.* (Zab **45:6**; imemtaja Yesu kwenye **Waeb 1:8**)
- *Hapo mwanzo uliutia msingi wa nchi, Na mbingu ni kazi ya mikono yako. Zaburi 102 26 Hizi zitaharibika, bali Wewe utadumu Naam, hizi zitachakaa kama nguo; Na kama mavazi utazibadilisha, Nazo zitabadilika.* (**Zab 102:25-26**; Imemtaja Yesu kwenye **Waeb 1:10-12**)
- *Jiwe walilolikataa waashi Limekuwa jiwe kuu la pembeni*. (**Zab 118:22**; Limetumika kwa Yesu kwenye **Matendo 4:11**)
- **Isa 6:1-13:** Kwenye **Isa 6:5** Isaya anasema, *"Ole wangu! Kwa maana nimepotea;. . . . na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi."* Kwenye **Isa 6:8-13** *"Kisha nikaisikia sauti ya Bwana"* kisha ikamwagiza Isaya kwenda kuwatabiria watu wa Israel. **Yohana 12:40** imenukuu **Isa 6:10**. **Yohana 12:41** kisha ikatumika kwa **Isaya 6** yote kwa Yesu kusema, *"Mambo haya Isaya aliyasema kwasababu aliuona utukufu wake [Yesu], na alimwambia Yeye."*
- *Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.* (**Isa 7:14**; limetumika kwa Yesu kwenye **Math 1:22-23**, ambalo ni dhahiri kwamba "Immanueli" maana yake ni *"Mungu pamoja nasi"*)
- *Bwana wa majeshi ndiye mtakayemtakasa; na awe yeye hofu yenu, na awe yeye utisho wenu. Naye atakuwa ni mahali patakatifu; bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili, na mtego na tanzi kwa wenyeji wa Yerusalemu.* (**Isa 8:13-14**; limetumika kwa Yesu kwenye **Warumi 9:33; 1 Pet 2:8**)
- *Sikiliza, ni sauti ya mtu aliaye, Itengenezeni nyikani njia ya Bwana; Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu."* (**Isa 40:3**; limetumika kwa Yesu kwenye **Math 3:3; Yohana 1:23**) kejeli
- *Nyumba yanguitaitwa nyumba ya sala.* (**Isa 56:7**; limetumika kwa Yesu mwenyewe kwenye **Math 21:13**)
- *Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele.* (**Mika 5:2**; limetumika kwa Yesu kwenye **Math 2:6**. Lugha ya mstari wa pili wa **Mika 5:2** ni lugha ya Agano la Kale ambayo wakati wote huelezea Mungu wa Milele kama vile mistari ya **Zab 74:12; 90:2; 93:2; Isa 43:13; 63:16**)
- *Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.* (**Zek 12:10**; limetumika kwa Yesu kwenye **Yohana 19:37; Ufu 1:7**)

**L.** ***Hitimisho***

Watetezi wa Kiislamu mara zote hung'ang'ana kwamba kumwabudu Yesu Mwana wa Mungu kama

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

sehemu ya Ukuu wa Mungu baadaye kuliendelezwa "chini ya ushawishi wa wanafalsafa wa Kigiriki usio wa kweli" (A'la Mawdudi n.d.: Q. 4:171n.212; angalia pia ibid.: n.216; Ali 2006: Q.4:171n.676 ["Alexandrian na Gnostic mysticism"]; Dirks 2008: 68-69). Kwa kinyume, takwimu zote za hapo juu zinaonyesha kwamba "uwezekano mkubwa wa Elimu ya Kikristo, uwepo wa Yesu na upekee wa utambulisho wa Kimungu, ulikuwa msingi wa Imani ya Kanisa la kwanza hata kabla ya Agano jipya kuandikwa, kwa kuwa ilianzia kwao wote. Ingawa kulikuwa na mwendelezo kwenye ufahamu huu na uwepo wa Yesu kwenye utambulisho wa Mungu, hatua za udanganyifu wa hilo na yeye mwenyewe akihusika ulifanyika mwanzoni mwa Elimu ya Kikristo. . . . Waandishi wa Agano jipya hawakuuona urithi wa Imani ya Kiyahudi kwa namna yoyote kwa kuwa kwenye njia yoyote kikwazo kikiwa uwepo wa Yesu kwenye utambulisho wa KiMungu; walivitumia vitu vyao vyote kwa umakini mkubwa ili kwa uhakika wamjumuishe Yesu kwenye utambulisho wa Kimungu; na waliona kwenye uwepo wa Yesu utambulisho wa Kimungu utimilifu wa matarajio ya Imani ya Kiyahudi juu ya nyakati za mwisho kwamba Mungu mmoja atatambulikana kwa wote kama ambavyo utakavyojulikana utawala wake kwa kila kitu." (Bauckham 1999: 27)[32] Msingi wa hitimisho hili kimsingi ulikuwa ni kile Yesu mwenyewe alichokisema na kile Yeye mwenyewe alichokifanya.

Kwa hiyo kama ambavyo mtazamo wa Kiislamu kwa Yesu kwamba ni Nabii asiye na dhambi ambaye hawezi kusema uongo, maneno na matendo ya Yesu yanawakabili (na kila mmoja) kwa jambo hilo hilo kwamba awakabili Wayahudi wa karne ya kwanzaYesu ni nani? Kwa kuangalia ushahidi, wengi wa Wayahudi wa karne ya kwanza walikubali kuwa Yesu alikuwa kile alichodai kuwa, Mwana wa Mungu, i.e., Mungu aliyekuja duniani, na maisha yao yalibadilika. Madai ya Yesu yanafikirisha kwamba kila mmoja anatakiwa kuangalia kwenye ushahidi na kufanya uchaguzi, kwa sababu kama madai ya Yesu ni ya kweli, basi kumkataa Yesu *kama Bwana* ni kumkataa Mungu na hivyo kuyakosa maisha yenyewe, lakini kuwa na Yesu kama Bwana ni kuwa na Mungu Baba pia na hivyo kuwa na uzima wa milele (**Yohana 8:19; 1 Yohana 2:23; 4:15; 2 Yohana 9**).

## VII. Matokeo ya ukweli kwamba Yesu Kristo ni Mungu kamili na mwanadamu kamili

### A. *Mungu aweza kuwa kweli na kujulikana kibinafsi ndani ya Kristo*

Kwenye imani nyingine za Kidini Mungu ni nadharia ya wazo muhimu. Kwenye dini zinazoamini miungu wengi, miungu ni roho tu. Kwenye suala la Mungu (au miungu) yawezekana kwa asili yake ya kweli kujulikana wakati wote na kwa njia ya kipekee. Hata hivyo, Kristo*"naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana"* (**Wakol 1:15**). Kwa Kristo *"Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili"* (**Wakol 2:9**). *"Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake"* (**Waeb 1:3**). "Yesu alikuwa mwanadamu ili kwamba wanadamu wapate kumjua Mungu asiye na mwisho. Sababu ya pili ya Mungu kuchagua kuwa mtu ni ili kujenga ufa uliokuwepo baina Mungu na mwanadamu. Kama Yesu angekuwa mwanadamu tu au kiumbe kilichoumbwa tu, basi ufa mkubwa kati ya Mungu na mwanadamu—asiye na mwisho na wenye mwisho, Muumbaji na viumbe, Mtakatifu na asiye mtakatifu—yangebakia. Kwetu sisi

---

[32] John Gilchrist anatuonyesha, "Hakuna kumbukumbu za kihistoria zenye maelezo yoyote yanayosema kwamba zinamtambua Yesu wa injili kwamba alikuwepo kwenye kipindi chochote kabla ya karne ya kwanza" (Gilchrist 2015: 23). Oskar Skarsaune anaonyesha kwamba, baada ya kusimama kutoka kwaWagiriki au mawazo ya Gnostic, "Ushahidi uliopo unaonyesha, kwa utofauti, kwamba wengi walijiunga na Falsafa na mawazo ya wagiriki [Hellenists] walijibu kwa chuki na hasira kwa wazo la Mungu kuuvaa mwili, na mashitaka ya kukufuru waliposikia kwamba Mwana wa Mungu aliyeuvaa mwili aliteseka kwenye hali ya aibu ya kusulubiwa. . . . Na hili linamaanisha kwamba Fundisho la Kikristo juu ya Mungu kuuvaa mwili laweza kuwa ni zao la wale waliojiunga na falsafa na mawazo la kigiriki—ambayo yanaliona fundisho kama falsafa na theolojia hiyo ni uovu. Na wala haliwezi kuwa wazo jema la mtu anayejaribu kusema kama Hellenists wanavyopenda." (Skarsaune 2002: 323-25) Mapema karne ya nne, Arius alianza kueneza fundisho muhimu la [Gnostic] kuhusu mtazamo wa Kristo, kumwelezea "Mwana kama wa pili, mdogo kuliko Mungu, akisimama kwenyeti baina ya uwepo wa Mungu na kiumbe" ("Arianism" 2012: Fundisho). Mkanganyiko huo ulipelekea Imani ya Nikea na ya Constantinople mwaka 325 na 381 lililotambua kuwa Kristo ni Mungu kamili na Mwanadamu kamili. Richard Bauckham anahitimisha kwamba wazo kwamba fundisho la Kikristo kumhusu Kristo linatokana na falsafa ya Kigiriki kimsingi ni kinyume na ukweli. . . . Kwenye mazingira ya kujichanganya kwa Aria, Theolojia ya Nikea ilikuwa muhimu kujaribu kuzuia kuenea kwa falsafa ya Kigiriki kuuelewa Uungu na kukubalika tena kwa mazingira mapya ya Uwepo wa Yesu kwenye Agano jipya kwenye Utambulisho wa kipekee wa Kimungu." (Bauckham 1999: 78; angalia pia Skarsaune 2002: 325, 333 ["Sasa kama ungewauliza mababa wa Kanisa wenyewe kile walichokifikiri kilikuwa ni historia ya mafundisho ya Kristo na Imani ya Nikea wasingekuwa na shaka wangejibu, Imani hii ni ya Biblia kabisa kabisa na siyo tu kwa sehemu, lakini pia kwa kukaririwa. Na kwa 'Kibiblia' wangekuwa na maana kwamba kila neno na kifungu kwenye Imani kimetokana na Agano la Kale, siyo tu kutoka kwenye Agano Jipya. . . . Bila kusema kwamba elimu ya Kristo kama hii ingeibuka tu kwenye mipango ya Kiyahudi miongoni mwa wanafunzi kwa kuzama kwenye Agano la Kale na makundi ya mawazo ya Wayahudi."]).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kuweza kumjua Mungu, Ilimpasa Mungu atushukie. Hakuna kiumbe ambacho kingeweza kujenga ufa mkubwa baina ya Mungu na mwanadamu Zaidi ya kipande cha udongo kingeweza kutafuta kuelewa na kufikia kiwango cha sanamu. Kwa upendo, Mungu alichukua hatua ya kutushukia. Alitaka kufungua njia ambayo wote wangeweza kumfahamu." (McDowell na Larson 1983: 19) Ukweli kwamba Mungu alikuwa mwanadamu na kuishi kati yetu kwa njia ya Yesu Kristo kunamaanisha kwamba tunaweza kumfahamu *yeye pekee* na *kweli*. Hili linaufanya Ukristo kuwa wa pekee miongoni mwa dini za Ulimwengu.

**B.** ***Kristo anatuonyesha sisi asili ya kweli ya Mungu ilivyo na hivyo pia ni mfano wetu wa kweli wa jinsi ya kuishi***

Kwa sababu Kristo ni Mungu, inakubalika na ni lazima kumwamini yeye na kumwabudu. Hata hivyo, kwa sababu ni mtu, ni mfano wa kweli wa jinsi gani tunavyopaswa kuishi maisha yetu hapa Ulimwenguni: *"Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda"* (**1 Yohana 2:5-6**). Petro anasema kwamba uvumilivu subira mateso kwa ajili ya kutenda yaliyo mema *" huu ndio wema hasa mbele za Mungu. Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake."* (**1 Pet 2:20-21**) Ni hapa ambapo Uungu wa Kristo na Uanadamu wake vinapokutana kwa kina nakufanya njia. **Wafil 2:5-11** inaeleza jinsi ambavyo Kristo alikuwa Mungu (**2:5-6**) lakini alijivua mwenyewe na kuwa mwanadamu, hata kuwa mtumwa (**2:7**), aliyekuwa mtii hata mauti ya msalaba (**2:8**); kwa hiyo, Mungu alimwiinua kiasi kwamba kila mmoja atamwabudu kama Bwana wa vyote (**2:9-11**). "Kuinuliwa kwa Kristo kushiriki kwenye mamlaka ya kipekee ya Kiungu inamwonyesha akiunganishwa kwenye utambulisho wa kipekee wa Kiungu. Lakini kwa kuwa Kristo aliyeinuliwa ndiye Kristo aliyeaibishwa kwanza, kwa kuwa kwa kweli ni *kwa sababu* ya kujidhili kwake mwenyewe ndicho kilimfanya ainuliwe, kuaibishwa kwake kulimfanyia utambulisho kwa Mungu kama kwa kuinuliwa kwake kulivyofanya. Utambulisho wa Mungu—Mungu ni nani—kumefunuliwa kama kujidhili na kuhudumu kama ilivyo kuinuliwa na kutawala. Mungu ambaye ni mkuu aweza pia kuwa wa chini, kwa sababu Mungu ni Mungu hatafuti faida yake mwenyewe lakini kwenye kujitoa mwenyewe. Kujitoa mwenyewe kwenye kujidhili na kuhudumu kunathibitisha kwamba mamlaka yake juu ya vitu pia ni umbo lake la kujitoa mwenyewe. Ni mtumwa pekee anayeweza kuwa Bwana. Ni mtumwa pekee ambaye pia ni Bwana hupokea kutambuliwa kwa ubwana wake—kutambuliwa kwa upekee wa Uungu wake—kutoka kwa uumbaji wote." (Bauckham 1999: 61)

Mungu kujitambulisha nasi katika Kristo kunatuongoza sisi kujitambulisha na wengine, kwa kuwa tumepokea ufahamu wa Kristo (**1 Wakor 2:16**) na Roho wa Kristo (**Warumi 8:1-17**). Tunawatendea wengine kwa upendo na msamaha kwa sababu ndiyo njia Kristo aliyotutendea sisi (**Waef 4:32; 1 Yohana 4:7-21**). Maisha yetu na matendo yetu yafanane na ya Kristo kwa kuwa tumelichukuwa umbo na sura yake (**Warumi 8:29; 12:1-2**). Mungu wa Wakristo hafanani na mungu mwingine yeyote na Ukristo haufanani na dini nyingine yoyote ulimwenguni—na ni Kristo pekee aliyelifunua hili.

**C.** ***Ukombozi kutoka kwenye dhambi zetu inawezekana tu kwa sababu Kristo ni Mungu kamili na mwanadamu kamili***

Watu wote kwa ndani wanajua kwamba tunalo tatizo: tumetengwa na Mungu kwa sababu tu wenye dhambi na Mungu ni mtakatifu na mkamilifu. Kwa usahihi Biblia imeona kwamba mwanadamu anayo makosa ya kifo, na uharibifu wa ndani ujulikanao kama dhambi ituzingayo (e.g., **Mwanzo 6:5; Zab 51:5; Yer 17:9; Warumi 3:9-18, 23; 7:14-24; Wagal 3:21-22**).

Kwa sababu watu wote wanalo tatizo la msingi la dhambi ya asili, hatuwezi kubadilisha hili, na kwa sababu hiyo hatuwezi kujiokoa wenyewe, Biblia inafunua kwamba Mungu alichagua kufanya kwa mwanadamu kile ambacho mwanadamu asingeweza kujifanyia mwenyewe. Ndiyo sababu Mungu alikuwa mtu kwa kupitia ubinadamu wa Yesu Kristo. Kwa kuuchukua mwili wa mwanadamu *"katika mfano wa mwili ulio wa dhambi,"* (**Warumi 8:3**) na kuja ulimwenguni, "Kristo kwa asili asiye na dhambi akawa mwakilishi wa mwanadamu mwenye dhambi. Hivyo Mungu, kwa kumtoa Kristo afe, angeihukumu dhambi kwa kuuangamiza mwili wake , na hivyo kuifuta. Kristo aliuchukuwa mfano wa[mwili wa dhambi] ili kwamba Mungu katika Kristo aweze kuufikia uhuru wa mwanadamu kutoka dhambini." (Schneider 1967: 196) Kristo aliishi maisha ambayo tulipaswa kuyaishi. *"bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi"* (**Waeb 4:15;** angalia pia **2 Wakor 5:21; Waeb 2:18**). Hili lilimstahilisha kuwa mwakilishi wetu kwa Baba, kufa kifo ambacho tulipaswa kufa, na kulipia adhabu ya dhambi zetu ambazo tulipaswa kuzilipia (**Warumi 8:3-4**). Kama **1 Tim 2:5** inasema, *"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu."* Mpatanishi ni mtu ambaye huzileta pande zote mbili zinazopingana pamoja . Kwa hiyo mpatanishi hujitambulisha kwa kila upande. Kwa sababu ni Mungu, Kristo alijitambulisha kwa Mungu

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Baba. Kwa sababu ni mwanadamu, Kristo alijitambulisha kwetu,. Kwa sababu hakutenda dhambi, asingeweza kulipa kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe. Badala yake, Kristo angechukua dhambi zetu yeye mwenyewe, kulipia gharama ambayo tulipaswa kuilipia, na pia kulipia haki yetu ili tuweze kusimama mbele za Mungu (**Isa 53:5-6, 10-11; Warumi 10:4; 2 Wakor 5:21; Waeb 2:17-18; 1 Pet 2:4; 3:18**). Ni Yeye pekee anayeweza kutuunganisha na Mungu (**Wakol 1:19-20**).

Hakuna hata mtu mmoja aliyeishi—siyo Mohamedi, wala Buddha, hakuna hata mmoja mwingine—aliyedai kuwakomboa watu kutoka kwenye dhambi zao. Na hakuna mtu mwingine ambaye aliishi ambaye *alistahili* kuwakomboa watu kutoka kwenye dhambi hata kama angetaka kufanya hivyo, kwa sababu: (1) hakuna hata mmoja aliyewahi kuishi ambaye alikuwa Mungu na Mwanadamu kama Kristo alivyo; na (2) kila mmoja aliyewahi kuishi alikuwa na dhambi yake ya asili na dhambi ambayo inapaswa kushughulikiwa (**Matendo 4:12; Warumi 3:9-18**). Hivyo, Ukristo pekee yake unaotambua kwamba wokovu siyo *na hautakuwa,* wa kutokana na kile tunachokifanya, lakini ni, *na utaendelea kuwa,* kwa kile ambacho Kristo alikifanya kwa ajili yetu. Hatuwezi kuununua Wokovu lakini ni zawadi tuliyopewa kwa neema ya Mungu kupitia Kristo (**Warumi 5:18-21; 6:23; Waef 1:7; 2:4-5, 8-9**). Ni kwa Kristo tunapata ujasiri wa kusimamam mbele za Mungu, kwa sababu Kristo ndiye wakili wetu ambaye hutuombea kwa Baba (**Warumi 8:34; Waeb 4:16; 7:25; 1 Yohana 2:1**). Kwa hiyo, "Yeye, kama asivyo mwanadamu mwingine kwenye historia, ni wa kusikilizwa, kuheshimiwa, na hata kuabudiwa. . . . Kumchukulia Yesu kama mtu wa kawaida (au hata muungu [kwa mtazamo wa wale wanaoamini kwenye miungu mingi]) kwa mazingira hayo itakuwa kufuru. Kushindwa kuyabadilisha maisha ya mtu kwa mafundisho yake itakuwa ni kuyakosa maisha yenyewe." (McDowell na Larson 1983: 14-15)

## ORODHA YA VYANZO

Kumbukumbu kamili ya bibliografia kwa nukuu kwenye maandiko yameonyeshwa kwenye bibliografia ya *Ukristo na Uislamu: Mambo Muhimu* ambayo yapo kwenye Wavuti ya ECLEA website at http://www.eclea.net/courses.html#islam.

## MWANDISHI



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada yake ya B.A. kwa masomo ya sayansi ya siasa kutoka kwa Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, na taaluma ya heshima, mnamo mwaka wa 1974, baadaye akajumuika na Phi Beta Kappa kwa kuwa na heshima ya kijamii. Tena akapata J.D. kutoka kwa Shule ya Uanasheria cha Cornell, magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akawekwa kwenye mamlaka ya Kisheria ya Coif haki za heshima ya jamii. Akaitumia miaka iliyofuata 28 akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye akashirikiana na Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Alikuwa muumini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake kwenye Theolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu au Master of Divinity kwenye chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Na sasa yeye ni mkurugenzi wa Huduma ya Kuwawezesha Viongozi wa Kanisa Afrika Mashariki (Equipping Church Leaders East Africa. "ECLEA"): **www.eclea.com.** Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na tovuti hii, na barua pepe kwa anuani hii: **jonathanmenn@yahoo.com.**